# TASWIRA YA JAGINA KATIKA TENDI: ULINGANISHI WA FUMO LIYONGO NA NABII ISA

**NA**

**FRANCISCO KABIRA GATHARA**

**C50/69644/2013**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A) KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

**NOVEMBA, 2015**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na imetolewa kwa mahitaji ya shahada ya Uzamili (MA) katika Chuo Kikuu cha Nairobi na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.

Francisco Kabira Gathara

Sahihi --------------------------------- Tarehe -----------------------

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii wa Chuo kikuu Cha Nairobi.

Dkt. Evans Mbuthia.

Sahihi -------------------------. Tarehe ----------------------------.

Prof. Kineene wa Mutiso.

Sahihi ---------------------------. Tarehe ------------------------.

## TABARUKU

Kazi hii ninaitabarukia marehemu mamangu Gladys Nyambura. Japo haukusoma, ulifahamu fika umuhimu wa elimu, sio tu kwa wanao, bali kwa ulimwengu mzima kwa jumla.

## SHUKRANI

Ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa siha njema na fursa nzuri ya kuendeleza masomo yangu vilivyo, kwani bila yeye singefika nilipo sasa. Neema zake zilinifaa zaidi.

Nimeweza kutimiza kazi hii kwa ukarimu, juhudi na hisani za watu wengi. Ningependa kuwataja baadhi yao ambao ushauri, msaada, wema na uadilifu wao uliniwezesha kufikia kiwango hiki katika kazi hii.

Ningependa zaidi kuwatolea shukrani za dhati wasimamizi wangu Daktari Evans Mbuthia na Profesa Kineene wa Mutiso, kwa kuniongoza tangu mwanzo hadi tamati ya tasnifu hii. Mihadhara yako Prof Kineene ilinifungua macho na kuniwezesha kuiteua mada hii ya utafiti. Mliniongoza kupitia njia nyingi za kiusomi na za kipekee. Baraka nyingi ziwafikie popote mlipo.

Vilevile, ningependa kuwashukuru wahadhiri wangu katika idara ya Isimu na Lugha, Chuo kikuu cha Nairobi kwa kuniandaa kiakademia hadi kufikia kuweza kuzikabili kazi za kitaalamu: Mwenyekiti wa idara, Prof. John Habwe, Dkt. Iribe Mwangi, Prof. Kithaka wa Mberia, Prof Rayyah Timmamy, Prof Kyallo Wamitila, Prof Mwenda Mbatia, Prof Mohammed Abdulaziz, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Swaleh Amiri, Dkt Ayub Mukhwana, Dkt Tom Olali, Dkt Alfred Buregeya na Mwalimu B.Mungania. Ninawaombea baraka nyingi kwa kazi zenu.

Pia ningependa kutoa shukrani zangu kwa mke wangu Elenah Wachera, ambaye anatambua umuhimu wa masomo katika jamii ya kisasa. Amejitolea mhanga na kwa moyo mkunjufu kuhakikisha kuwa nimeendeleza na kukamilisha masomo yangu. Umekuwa rafiki wa karibu kwa

kunielewa na kunishauri, hasa, wakati mambo yaliniwia magumu. Asante sana mwandani wangu na Mungu akubariki. Aidha, sitamsahau mwanangu Gladys Nyambura Kabira ambaye alivumilia kwa muda mrefu ambao sikushikirikiana naye kwa mambo mengi kila aliponihitaji. Wote ninawaombea waweze kutambua dhima ya masomo maishani mwa  ya binadamu katika siku za leo na za halafu.

Aidha, sitawasahau wahadhiri mwenzangu katika Chuo cha Ualimu cha Kigari, ambao walinishikilia kazini wakati wote nilipokuwa masomoni. Kwa hisani yenu, mola awaruzuku na awaongeze neema maridhawa.

Shukrani zangu tele ziwaendee wazamili wenzangu tuliojikakamua kutafuta lulu ya masomo. Biasha Khamis, Evans Makhulo, Henry Idindi, Hezekiel Gikambi, Rita Magara, Rose Dama, Rose Kamwanza, Stephen Machira na Timothy Otuchi. Nimeshukuru kwa kuwajua na hata kufanya urafiki nanyi kwa muda huo wote. Mlikuwa wachangamfu hata mambo yalipotulemea kwa changamoto nyingi. Mola azidishe wema wake kwenu.

**ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA**

Bi....................... Bibi

B.K ....................Baada ya Kristo

Bw...................... Bwana

Khj..................... Kama hapo juu

K.K ....................Kabla ya Kristo

Mh..................... Mhariri

Na .....................Nambari

n.k .....................Na kadhalika

n.w.................... Na wengine

taz .....................Tazama

TUKI ................Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

T.Y..................... Tafsiri yetu

ub ......................Ubeti

uk ......................Ukurasa

# IKISIRI

Utafiti huu ulikusudia kufafanua taswira ya jagina katika utendi, kwa kumrejelea shujaa Fumo Liyongo kama alivyoelezwa katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* wake Muhammed Kijumwa (1913), na Nabii Isa kama alivyoelezwa katika *Utenzi wa Nabii Isa*, wake Musa Mshenga (1977). Madhumuni makuu katika utafiti huu yalikuwa ni kulinganisha na kutofautisha sifa za kijagina za Nabii Isa na Fumo Liyongo, kwa nia ya kudhibitisha kuwa, sira za majagina kutoka jamii mbili zinazotofautiana katika mazingira, mila na desturi, zinaweza kufanana sana.

Uchanguzi huu tuliufikia baada ya kutambua kuwa majagina wa kidini na wa kihistoria hawajatafitiwa kikamilifu. Tumeangalia historia na maisha ya Fumo Liyongo na Nabii Isa, pamoja na historia ya jamii zilizowazaa na kuwakuza, kisha tukalinganisha na kutofautisha sifa zao za kijagina kwa mujibu wa sifa bia za mashujaa. Aidha, tumeangazia umuhimu wa mashujaa hawa kwa jamii zao. Data ilikusanywa maktabani na mtandaoni, kuchanganuliwa na kubainishwa kwa msingi wa nadharia ya Uhakiki wa Vikale iliyoasisiwa na Carl Jung.

Matokeo ya utafiti huu yalilingana na nadharia tete zilizoongoza mchakato mzima wa utafiti huu. Ilidhihirika kuwa Liyongo na Nabii Isa ni mifano mizuri ya jagina wa kihistoria na wa kidini. Mashujaa hawa pia wametokea kuwa muhimu sana katika historia ya jamii zao, na kwa ulimwengu mzima kwa jumla, na kuwa wanaweza kuwekwa katika viwango sawa na mashujaa wengine ulimwenguni. Matokeo haya vilevile yalidhihirisha kuwa, sifa za mashujaa hawa kwa kiasi kikubwa zinafanana.

## YALIYOMO

UNGAMO ........................................ ii

TABARUKU ........................................ iii

SHUKRANI ........................................ iv

ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA ........................................ vi

IKISIRI ........................................ vii

YALIYOMO ........................................ viii

**SURA YA KWANZA** ........................................ 1

1.0 Utangulizi ........................................ 1

1.1 Tatizo la Utafiti ........................................ 5

1.2 Madhumuni ya Utafiti ........................................ 6

1.3 Nadharia tete ........................................ 6

1.4 Maswali ya Utafiti ........................................ 6

1.5 Sababu za Kuchagua Mada ........................................ 6

1.6 Upeo na Mipaka ........................................ 7

1.7 Msingi wa Kinadharia ........................................ 9

1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ........................................ 15

1.9 Mbinu za Utafiti ........................................ 22

1.10 Hitimisho ........................................ 22

**SURA YA PILI: HISTORIA YA FUMO LIYONGO NA SHUJAA ISA PAMOJA NA ILE YA JAMII ILIYOWAZAA NA KUWAKUZA** ........................................ 24

2.0 Utangulizi ........................................ 24

2.1 Historia ya Waswahili ........................................ 24

2.2 Historia ya Fumo Liyongo ........................................ 30

2.3 Misukosuko ya Kivita Iliyomzua Fumo Liyongo ........................................ 33

2.4 Historia ya Wayahudi hadi Kuzaliwa kwa Nabii Isa ........................................ 36

2.5 Misukosuko ya Kivita Iliyowakumba Wayahudi ........................................ 38

2.6 Historia Ya Nabii Isa ........................................ 40

2.7 Hitimisho ........................................ 46

**SURA YA TATU: KULINGANISHA NA KUTOFAUTISHA SIFA ZA KIJAGINA ZA NABII ISA NA FUMO LIYONGO** ........................................ 47

3.0 Utangulizi ........................................ 47

3.1 Kuzuka kwa Mashujaa ........................................ 48

3.1.1 Utabiri wa Kuzaliwa kwa Majagina ........................................ 48

3.1.2 Jagina kwa Kawaida ni Mwanamume ........................................ 50

3.1.3 Utoto na Ujana wa Jagina ........................................ 51

3.1.4 Shujaa Hutokana na Ukoo wa Kifalme ........................................ 52

3.1.5 Utetezi wa Cheo ........................................ 53

3.1.6 Maadui wa Shujaa ........................................ 55

3.1.7 Shujaa huwa Kipenzi cha Wanajamii ........................................ 57

3.1.8 Jina la Shujaa ........................................ 59

3.1.9 Shujaa Huwa na Akili Pevu ........................................ 60

3.2.0 Kugura kwa Shujaa ........................................ 63

3.2.1 Mashujaa kwa Kawaida Huwa ni Washairi ........................................ 64

3.2.2 Maisha ya Shujaa Huwa ni Dhiki Tupu ........................................ 65

3.2.3 Maisha na Matendo ya Shujaa Huwa ni ya Kimiujiza ........................................ 66

3.2.4 Shujaa Huwa Hawaeleweki kwa Uwazi ............................................................... 68

3.2.5 Mapenzi ya Mama kwa Shujaa ........................................................................ 69

3.2.6 Kimo na Nguvu za Shujaa ............................................................................... 70

3.2.7 Majagina Aghalabu Huwa Magwiji Katika Vita ............................................... 72

3.2.8 Shujaa na Suala la Ndoa ................................................................................. 74

3.2.9 Kifuasi cha Shujaa .......................................................................................... 75

3.3.0 Shujaa Huhusishwa na Zaidi ya Jamii Moja ..................................................... 76

3.3.1 Usaliti na Kifo cha Shujaa ............................................................................... 78

3.3.2 Anamoishi Jagina na Kurudi Kwake Safari ya Mwisho .................................... 800

3.4 Hitimisho.......................................................................................................... 82

**SURA YA NNE: UMUHIMU WA FUMO LIYONGO NA NABII ISA KWA JAMII ZAO.**

4.0 Utangulizi .........................................................................................................83

4.1.1 Kitambulisho cha Kitaifa/Kijamii ..................................................................... 89

4.1.2 Ukombozi na Muungano wa Jamii .................................................................. 83

4.1.3 Kioo cha Jamii/Historia ya Jamii ..................................................................... 85

4.1.4 Mabadiliko Katika Mfumo Mzima wa Jamii ..................................................... 84

4.1.5 Ruwaza Bora ya Kufuatwa na Wanajamii ........................................................ 88

4.1.6 Fahari ya Jamii Zao......................................................................................... 89

4.2 Hitimisho.......................................................................................................... 911

**SURA YA TANO: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ............................................ 92

5.0 Hitimisho.......................................................................................................... 92

5.1 Mapendekezo ya Utafiti ..................................................................................... 95

**MAREJEO**.......................................................................................................... 96

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Mada tunayochunguza inahusu taswira ya jagina katika tendi mbili teule; *Utenzi wa Nabii Isa* ulioandikwa (1977) na Musa Mzenga, Almaarufu, Ustadh Shirazi, na *Utenzi wa Fumo Liyongo*, wake Mohamed Kijumwa, kama ulivyoelezwa katika *Tenzi Tatu za Kale* (1999), kitabu kilichohaririwa na Mulokozi. Tumewalinganisha na kuwatofautishaa Fumo Liyongo na Nabii Isa, ambao ndio majagina wakuu wa tendi hizi, kwa mujibu wa sifa bia za mashujaa. Kazi hii vilevile imelenga kuonyesha umuhimu wa majagina hawa kwa jamii zao.

Jamii tofauti zina mitazamo anuwai kuhusu taswira ya jagina. Taswira ni neno lenye matumizi mbalimbali katika uhakiki wa fasihi. Kulingana na Njogu na Chimera (1993), taswira ni mkusanyiko wa picha zinazotokana na ufundi wa msanii katika kuteua na kupanga maneno yake ya kazi fulani ya kifasihi. Wanasema pia, taswira ni mkusanyiko wa picha anazozipata msomaji au msikilizaji wa kazi fulani ya kifasihi. Picha hizi huwa na mafunzo au jumbe fulani. Katika *Kamusi ya Kiswahili sanifu* (2002), tunaelezwa taswira ni picha ya mambo au vitu vinavyomjia mtu akilini mwake; maono, picha. Pia ni mchoro au sanamu.

Kutokana na maelezo yaliyotolewa hapo juu, tunaweza kusema kuwa maana ya kijumla ya neno hili ni mkusanyiko wa picha zinazoundwa na maelezo ya msanii katika kazi yake ya fasihi. Katika utafiti huu, tumejikita katika tendi hizi mbili kufafanulia picha za majagina hawa wawili kama kielelezo, hata ingawa tumerejelea matini zingine ambazo zinawazungumzia, ili kujenga taswira pana ya majagina hawa. Sifa za kimsingi za majagina nyingi ila zinajitokeza kwa viwango tofauti, kwa majagina wa aina mbalimbali na wa mazingira mbalimbali. Majagina

wanaweza kutofautiana kimaeneo, lakini ukweli ni kwamba zipo sifa ambazo ni bia kwa majagina wote.

Wamitila (2003) amejadili utendi kama shairi refu la kisimulizi linalozungumzia kwa mapana na kwa mtindo wa hali ya juu, matendo ya mashujaa au shujaa mmoja. Anasema kuwa utendi huwa na sifa nyingi na huweza kuleta pamoja hadithi ya shujaa, visasili, historia, pamoja na ndoto za taifa fulani. Fasili hii inatupatia utata inapoeleza utendi kama shairi refu la kisimulizi. Utata unajitokeza katika kupima urefu wa ushairi ulio katika masimulizi.Tutatumia kipimo gani kupima urefu huo? Na mpaka wa ushairi mrefu na mfupi unaanzia wapi na kuishia wapi? Fasili hiyo inahitaji maelezo zaidi ya kipimo kipi kinafaa kutumika.

Mulokozi (1996), anaeleza utendi kama ushairi wa matendo. Ni utungo mrefu wenye kusimulia matukio ya kishujaa yenye uzito wa kijamii au kitaifa. Matukio hayo yanaweza kuwa ya kihistoria na visakale. Ufafanuzi huu wa Mulokozi umepiga hatua mbele kwa kueleza utendi kama ushairi wa matendo. Utendi hufungamana na matendo wakati wa utendaji wake. Matendo hayo huathirika utendi unapokuwa katika maandishi.

Kutokana na fasili za wataalamu hawa, tunaweza kusema kuwa utendi ni ushairi unaosimulia tukio fulani kwa matendo. Usimuliaji wa tukio huambatana na matendo ambayo hufanywa na msimuliaji. Utenzi unaweza kuhusu tukio lolote la kijamii ambalo laweza kuwa la kishujaa au lisiwe la kishujaa. Utafiti huu unakusudia kufafanua taswira ya jagina katika utendi kwa kumrejelea Nabii Isa, ambaye ni shujaa wa kidini (anayefahamika kama Yesu miongoni mwa Wakristo), kama alivyoelezewa katika *Utenzi wa Nabii Isa,* na Fumo Liyongo (ambaye ni shujaa

wa kihistoria), kama alivyoelezewa katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Nia yetu katika utafiti huu ni kuthibitisha kuwa sira za majagina katika ulimwengu mzima zinafanana sana. Nitaangalia maisha ya majagina hawa wawili na kuangazia sifa zao za kishujaa kwa kuzilinganisha na sifa bia za mashujaa.

Kulingana na Gaster, kama anavyonukuliwa na Gichamba (2005), jagina ni mtu ambaye humiliki uwezo zaidi kuliko uwezo wa watu wa kawaida na hutumia uwezo huu kiujasiri na huwa tayari kuyahatarisha maisha yake kwa manufaa ya watu wengine. Nayo *Kamusi ya Tuki* (2004), inasema kuwa, shujaa ni mtu mwenye moyo thabiti anayeweza kukabili mambo, hata kama ni hatari. Ni jasiri, nguli, jogoo, jabali, abtali, ghazi, nyamaume.

Kwa jumla, tunakubaliana na maoni ya wataalamu hawa na kufafanua shujaa kama kiumbe aliye na sifa za kiajabu, anayekuzwa na wanajamii na pia kujikuza mwenyewe ili ajinufaishe na kuwanufaisha watu wengine.

Mutiso (1999:1), anaainisha majagina katika makundi matatu. Anasema jagina wa kwanza ni kiumbe wa kweli ambaye amekuzwa na amejikuza mwenyewe hata akaonekana kiumbe wa ajabu. Kiumbe huyu huwa ni mashuhuri na husifika kwa ujasiri, nguvu, (hata kama amelemaa ulemavu huu ni onyo kuwa baadaye atakuwa na nguvu za ajabu) na kwa kila jambo lionekanalo kubwa au la ajabu katika jamii husika, hata kama jambo hilo twaliona ni la kipuuzi. Mabadiliko yote mazuri yatokeayo katika jamii, jamii husika huamini ya kwamba yameletwa na jagina wao, hata kama jagina huyo hahusiki kamwe. Kwa kawaida, jagina huyu hutokana na familia maskini lakini jamii yake huamini ya kwamba ametokana na familia tajiri ya kifalme. Maisha yake huwa

ni ya taabu na dhiki na ya kutangataga. Yumkini, watu humwabudu baada ya kifo chake (kwa kawaida hata akifa huaminika ya kwamba yu hai na anayaona yote tuyatendayo).

Mutiso (khj), anaendelea kufafanua aina ya pili ya jagina kama kiumbe wa kihurafa, ambaye ameumbwa na jamii yake. Kiumbe huyu pia huwa na sifa ambazo si za kawaida na ghalibu awe ni Mungu au yote mawili. Yumkini iaminike ya kwamba jagina huyu ndiye mzazi wa jamii husika.

Jagina wa tatu ni mhusika mkuu katika utenzi, tamthilia, riwaya, hadithi, ngano, sinema, kitendo au jambo. Mpaka kati ya aina hizi tatu za majagina ni mwembamba, kwani mhusika mkuu anaweza kuwa ni mmojawapo wa aina mbili zingine za majagina. Kwa sababu hii, tunapomjadili jagina Isa ambaye ni shujaa wa kidini na kulinganisha sifa zake na za Fumo Liyongo ambaye ni jagina wa kihistoria na majagina wengine, hatunuii kukuza au kumdunisha shujaa wa jamii yoyote ile, bali kwa maoni yetu, sifa za majagina wote, wa kidini au la ni karibu sawa.

Utendi ni ushairi unaosimulia tukio fulani kwa matendo. Usimuliaji wa tukio huambatana na matendo ambayo hufanywa na msimuliaji. Utendi unaweza kuhusu tukio lolote la kijamii ambalo laweza kuwa la kishujaa au lisiwe la kishujaa. Katika makala haya, istilahi ambayo imetumika ni tenzi ambayo ina maana sawa na tendi. Hivyo, istilahi zote zimetumika sawa.

Tendi nyingi huwajenga mashujaa wake katika hali ya kuwafungamanisha na matatizo ya kijamii yanayoikabili jamii husika. Hufanya hivyo kwa malengo mbalimbali. Kwanza, kwa lengo la kuonyesha kuwa shujaa ni zao la jamii, na kama ni zao la jamii hana budi kukumbana na

matatizo kama wanajamii wengine. Pia, hufanya hivi kwa lengo la kuwaonyesha wanajamii ushujaa wa shujaa katika kukabiliana na matatizo mbalimbali, kwamba hutofautiana na watu wa kawaida. Aidha, hufanya hivyo kwa lengo la kuwaondolea wanajamii hofu na kuwahakikishia usalama wao pindi wapatwapo na matatizo, kuwa, wanaye mwokozi atakayewaokoa katika matatizo yao. Katika kuyathibitisha haya tutajikita katika kuchambua ujagina wa wahusika wetu kama unavyojitokeza katika *Utenzi wa Nabii Isa*, na *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

**1.2 Tatizo la Utafiti**

Suala la mashujaa ulimwenguni limefanyiwa utafiti na watafiti wengi kama anavyosema Mutiso (1985 na 1999). Anaeleza watafiti hawa kama: Carlyle (1924), Kunene (1971), Butler (1979), Raglan (1965), Mberia (1989), na Gaster (1987). Wengi wa watafiti hawa kulingana na Mutiso (khj), wamezungumzia majagina kwa jumla. Baadhi yao kama Mutiso mwenyewe, na Mberia wamejaribu kulinganisha majagina wawili wa kidini au wa kihistoria. Watafiti hawa wametoa sifa kadhaa, ambazo ni bia na ambazo zinadhihirika kwa mashujaa wa jamii mbalimbali ulimwenguni, na kwa viwango tofauti tofauti. Sifa za majagina walizozitoa watafiti hawa sio za pekee na nyingine zinaweza kujitokeza iwapo ulinganishi zaidi wa mashujaa wa aina tofauti, na kutoka tamaduni na mazingira tofautitofauti ulimwenguni ungefanywa. Mashujaa huwa na umuhimu mkubwa kwa jamii zao. Fumo Liyongo ambaye ni shujaa wa kihistoria wa jamii ya Waswahili, na Nabii Isa, ambaye ni shujaa wa kidini wa Wayahudi, ni mifano mizuri ya majagina ambao wanaweza kutuzulia sifa zaidi za majagina,  na ndio msingi wa utafiti wetu.

## 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni ya utafiti wetu ni:

a) Kubaini historia na mazingira ya kijamii yaliyowazaa na kuwakuza shujaa Isa na Fumo Liyongo.

b) Kulinganisha na kutofautisha sifa za kishujaa za Isa na Fumo Liyongo.

c) Kuchunguza umuhimu wa majagina hawa kwa jamii zao, na kwa ulimwengu mzima kwa jumla.

## 1.3 Nadharia tete.

Utafiti wetu uliongozwa na nadharia tete zifuatazo:

a) Liyongo na Isa ni mifano mizuri ya majagina wa kihistoria na wa kidini.

b) Sifa za kishujaa za majagina hawa kwa kiasi kikubwa zinafanana.

c) Mashujaa hawa wana nafasi muhimu sana katika historia ya jamii zao, na kwa ulimwengu mzima kwa jumla.

## 1.4 Maswali ya Utafiti.

a) Ni mazingira yepi ya kijamii yaliyowazaa mashujaa Fumo Liyongo na Isa?

b) Ni kwa kiwango kipi ambapo sifa za mashujaa hawa zinafanana na kutofautiana?

c) Majagina hawa ni muhimu sana kwa jamii zao na kwa ulimwengu mzima kwa jumla.

## 1.5 Sababu za Kuchagua Mada.

Majagina au mashujaa wa utendi wa Kiswahili wanaweza kuwekwa katika vikundi vitatu. Kikundi cha kwanza ni cha mashujaa wa kijadi wa Kiafrika, kwa mfano Fumo Liyongo katika

*Utendi wa Fumo Liyongo,* na Abushiri bin Salim katika *Utendi wa Vita vya Wadachi Kutamalaki Mrima*. Kikundi cha pili ni cha mashujaa wa kidini, kama mtume Muhamadi na masahaba wake katika *Utendi wa Rasil Ghuli.* Kikundi cha tatu kinajumuisha mashujaa wa kubuni kama vile Tajiri, katika *Utendi wa Masahibu.* Kuna uwezekano wa shujaa kuwa katika zaidi ya kitengo kimoja. Mpaka baina ya makundi haya ni finyu mno. Baadhi ya mashujaa wa kidini yumkini wawe ni wa kubuni kama Mungu na Shetani. Hata mashujaa wa makundi hayo mengine wanaweza kutiliwa chumvi sawa na ubunifu. Kama vile tumeonyesha hapa baadaye, tafiti ambazo tayari zimefanywa, zimewalinganisha majagina wa aina moja tu, wawe wa kidini, wa kubuni au wa kihistoria. Hakuna utafiti wa kina tuujuao unaomlinganisha jagina yeyote wa kidini na wa kihistoria au wa kubuni. Hivyo, utafiti huu umenuiwa kuliziba pengo hili. Utafiti huu ni wa kwanza kumlinganisha shujaa wa kidini na wa kihistoria, kutoa sifa zao kama majagina na umuhimu wao kwa tamaduni zao.

**1.6 Upeo na Mipaka**

Ujagina ni mada ambayo ni pana mno ya kufanyia utafiti. Kwa sababu ya wakati, imetuhalisi kujifunga katika kuangazia masuala maalum. Tumechunguza sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na shujaa Isa kwa mujibu wa sifa bia za mashujaa. Tumelinganisha na kutofautisha sifa zao na kuonyesha umuhimu wa kila jagina kwa jamii yake.

Kuna kazi nyingi ambazo zimeandikwa kuwahusu Fumo Liyongo na Nabii Isa. Kazi za kimsingi ambazo tulizirejelea na ambazo tuliamini zingelifaa katika utafiti huu ni pamoja na *Utenzi wa Fumo Liyongo,* ulio katika *Tenzi Tatu za Kale*, kitabu kilichohaririwa na Mulokozi (1999), Miehe na wenzake (2004), ambayo ni kazi iliyokusanya mashairi na nyimbo zinazodaiwa

kutungwa na Fumo Liyongo; *Takhmisa ya Liyongo*, *Utenzi wa Nabii Isa*, *Qurani* na *Biblia takatifu*.

Katika utafiti huu, japo jagina tuliyemrejelea ni Nabii Isa kama mhusika wa kifasihi katika *Utenzi wa Nabii Isa*, tumerejelea *Qurani* na *Bibilia* vilevile, ili kujaribu kutoa taswira pana ya ujagina wake, na hali kadhalika kuangazia umuhimu wake kwa jamii yake. Katika utafiti huu, hatujajiingiza katika mjadala iwapo Isa bin Maryamu wa *Qurani* ndiye Yesu Kristo, mwana wa Mungu wa *Bibilia*. Tumechukulia kuwa haya ni majina tofauti ya mhusika mmoja akitazamwa na Mkristo au Mwislamu.

Majagina huzuka katika mazingira fulani na katika kipindi maalum, ili kutekeleza jukumu maalum katika jamii. Hii ndiyo sababu wanajamii humtazama shujaa wao kama zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hivyo, katika utafiti wetu imetulazimu kuangazia mazingira ya kihistoria ambamo mashujaa hawa wanapatikana. Tumejaribu kufafanua usuli wa jumuiya wanamopatikana Fumo Liyongo na Nabii Isa, ili kuwaelewa majagina hawa kwa kina. Ni katika kuuelewa muundo na hali halisi za kijamii, ndiposa tunaweza kuelewa na kufasili masuala yanayomzunguka shujaa. Kutokana na uelewa wa hali halisi ya kijamii, tunaweza kupata majibu ya maswali yafuatayo: Ni kwa nini shujaa huzuka katika kipindi fulani katika historia ya jamii fulani? Ni sifa zipi ambazo jagina ako nazo na ambazo wanajamii wengine hawana? Mchango wa shujaa katika jamii yake ni upi?

**1.7 Msingi wa Kinadharia**

Katika utafiti huu tumeongozwa na nadharia ya *Uhakiki wa Vikale*. Nadharia ya vikale imetumikizwa katika ulinganishi wa sifa za shujaa Liyongo na Nabii Isa, kwa mujibu wa sifa bia za mashujaa, na vilevile katika kuelezea umuhimu wa shujaa Isa na Fumo Liyongo katika mfumo mzima wa jamii zao.

Kulingana na Wafula na Njogu (2007), vikale ni picha kongwe zinazotokea mara kwa mara katika kazi za fasihi.Vikale hivi vinaweza kuwa taswira, wahusika, miundo ya usimuliaji na kadhia zingine zinazopatikana katika fasihi popote pale ulimwenguni. Vikale humwezesha mhakiki wa fasihi kubainisha uhusiano uliopo kati ya fasihi za aina mbalimbali.

Abrahams (1981:11-12) kama alivyonukuliwa na Mutiso (2004:21), anaeleza nadharia ya uhakiki wa vikale kwa mitazamo miwili. Ameeleza kuwa chimbuko la nadharia hii ni kutokana na kazi ya James G.Frazer katika kitabu cha "*The Golden Bough*" (1890-1915), kilichotolewa katika idara ya Anthropolojia Linganishi, chuo kikuu cha Cambridge. Abrahams (khj), anaeleza kuwa kitabu hiki kilifuatilia ruwaza za kimsingi za visasili na za kitambiko ambazo alidai hujirudiarudia katika visakale na taratibu nyingi katika tamaduni anuwai. Kwa upande mwingine, ameeleza kuwa nadharia ya vikale ilitokana na maelezo ya Carl G. Jung kuhusaina na akili-laza. Jung alikuwa mwanafunzi wa Sigmund Freud, mtaalamu aliyeasisi taaluma ya Uchanganuzi nafsia, lakini walitofautiana kimawazo. Wakati ambapo Freud alisisitiza akili-laza ya kibinafsi, naye Jung alisisitiza kuhusu akili-laza jumuishi. Jung alitumia istilahi ya vikale kwenye taswira za asili za kumbukumbu zinazorudiwarudiwa kutokana na tajiriba katika maisha ya tangu mababu zetu wa kale. Alisisitiza kuwa, taswira hizi hurithiwa na kutiwa kwenye akili-

laza jumuishi ya jamii ya watu na ambazo hudhihirika katika visasili, ndoto, mawazo ya binadamu mathalan, katika vipengele vyote katika maisha ya binadamu wote duniani na pia katika kazi za kifasihi.

Nadharia ya uhakiki wa vikale kwa hivyo, inaeleza kuwa binadamu wote ni sawa popote walipo. Tofauti ni ndogo na za kufikirika ambazo husababishwa na tofauti za kihistoria na za kimazingira. (Mutiso 1999:2), anasema kwa jumla vikale hurejelea ruwaza za kimsingi. Ruwaza jumla au bia za aina moja au nyingine ambazo aghalabu hudhihirika katika jamii za watu mbalimbali duniani. Anashikilia kuwa vikale humvuta msomaji vikitumiwa vizuri katika kazi ya kifasihi (Mutiso 1996: 20 - 23 na Gichamba 2005: 6-7).

Kulingana na Wamitila (2002: xi na 2008: 45), fasihi huwa na sifa bia ambazo huzipa uwezo wa kiulinganishi. Anadai kuwa msingi wa fasihi zote duniani ni jamii kwani jamii mbalimbali zimeundwa na binadamu. Kwa hivyo, fasihi mbalimbali duniani huingiliana. Mwingiliano katika masuala anuwai katika maisha ya binadamu ndio huwezesha fasihi kulinganishika. Aidha, ulinganishi huu unatokana na sababu kwamba, fasihi zote ulimwenguni hutumia lugha kama malighafi yao na lugha zote duniani huwa na sifa zinzoshahibiana. Pili, fasihi zote duniani huchota maudhui yake kutoka katika jamii za wanadamu. Wanadamu wote duniani huwa na sifa zinazofanana. Tatu, fasihi hulenga kutekeleza dhima fulani katika jamii, kama vile kuelimisha, kuonya, kufariji, kuburudisha, kuzindua, kuadilisha, kuhamasisha, n.k. Isitoshe, fasihi ni zao la jamii fulani duniani ambayo hushabihiana na hivyo, huwezesha fasihi zote duniani kulinganishwa.

Ingawaje kutokana na maelezo ya Abrahams (khj:11-12) kuwa mtazamo wa kisaikolojia pia unaweza kutumiwa kuhalalisha kufanana kwa sifa bia na kushabihiana kwa umuhimu wa mashujaa wote duniani, somo letu limeegemea zaidi  katika upande wa anthropolojia. Hebu tujiulize hili swali, kwa nini ruwaza za visasili na matambiko hujitokeza katika visakale na taratibu nyingi za watu mbalimbali duniani? Kujibu swali hili ni sharti tuchukue mtazamo wa kijumla kuhusiana na uelewa wa hulka za kila binadamu katika dunia. Madai kuwa wanadamu wote duniani ni sawa ni ya wazi. Gichamba (2005:8-9) na Mutiso (1999:2) wanaeleza kuwa jamii zote duniani huwa na vipengele vya kimaisha vinavyolandana. Kwa mfano hakuna jamii ya watu duniani isiyokuwa na mavazi, lugha, dini, sheria, katiba (iwe imeandikwa au haijaandikwa) mapenzi, kilimo ⁄ ufugaji, wizi, utu, talaka, fasihi , elimu, uuguzi, ukahaba, uchochezi, ufisadi, utabaka, mayatima, ndoa, malezi, muziki, wajane, mapishi, namna ya kufanya mazishi, nk. Vipengele hivi huwa na umuhimu ulio sawa katika jamii zote. Kwa mfano, uamilifu wa mavazi ni kusetiri uchi wa binadamu. Sheria ipo kuhakikisha kuwa haki inatendeka katika jamii yeyote ile. Hata hivyo, ingawa uamilifu wa vipengele hivi ni sawa, tofauti ni katika utendakazi au utekelezaji wao. Kila jamii ina njia mahususi ya kutekeleza masuala na matamanio mbalimbali kutegemea kiwango cha teknolojia na mazingira ya jamii husika.

Werner (1968:18) katika kuchunguza visasili na visakale vya wabantu, alithibitisha uhusiano uliopo katika mila, desturi na lugha zao, dhana ya kuwepo kwa Mungu mmoja, licha ya kwamba wengine hawatofautishi baina ya mawingu au jua, kuamini katika maisha ya baada ya kifo, na kuwa na mawazo kwamba roho za waliokufa zinaweza kuaathiri hali zao za kimaisha kwa kiwango chochote kile. Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa katika kulinganisha visasili,

visakale na matambiko ya jamii tofautitofauti, kuna uhusiano katika ruwaza ya sifa za visasili na matambiko katika tamaduni za jamii mbalimbali.

Mutiso (1996:24), akimnukuu Eliade (1957:15–17), anadai kuwa visaasili hufichua muundo wa kweli na anuwai wa hali za wanadamu duniani. Kwa sababu hii, visasili huwa vielezo bora kwa tabia za wanadamu na zinafichua hadithi za kweli. Anashikilia kuwa kwa sababu hiyo, visasili haviwezi kuwa mahsusi, binafsi au vya pekee kwani huchukuliwa kama kielezo mwafaka kwa wanadamu wote duniani. Mutiso (1996: 23), na Gichamba (2005: 9), wanasema kuwa mashujaa, wawe wa kweli au wa kufikirika tu wana jukumu katika uumbaji wa vijana wa huko Ulaya na hasa kutokana na uigizaji wa sifa na tabia za wahusika kwenye ngano zilizo na vitushi vyenye hatari na majabari ya kivita miongoni mwa masuala mengine  sawa na hayo.

Eliade (khj: 27 – 29), anaendelea kudai kuwa, baadhi ya sherehe zinazoadhimishwa leo zingali zikihifadhi muundo na majukumu ya visasili, na binadamu hufanya hivi kupitia kwa akili laza bila yeye kujua. Kwa mfano, maadhimisho ya mwaka mpya, sherehe za kuzaliwa, ujenzi wa nyumba, sherehe za kupalilia, kuvuna, sherehe za nyimbo. Kwa mfano, Wabajuni kuimba nyimbo za vave, watu kuimba nyimbo za kazi, mazishi n.k ni ishara kuwa binadamu anarudia ya kale (za Adamu na Hawa) bila kujua, kwa jina la mwanzo mpya, mvuko mpya au kubatizwa.Binadamu huzaliwa upya hata wakati anapopewa jina. Katika uponyaji kwa mfano, anarudi kutumia miti shamba. Hata Amri kumi ambazo zimo katika *Bibilia* zimo katika sheria zetu za kitamaduni. Anashadidi kuwa, (uk. 9) kuna mambo mja anashindwa kuelezea na kwa hivyo anatumia visasili na visakale.

Njogu na Wafula (2007: 81 – 82) wakiwanukuu Jung (1972), Cuddon (1997) na Wamitila (2001) wanadai kuwa Jung, akifanya utafiti juu ya njozi na ndoto, alichukulia kikale kama aina ya mtiriko au picha kongwe inayojitokeza mara kwa mara katika tajiriba anayopitia mwanadamu. Wanashikilia kwamba, mtu na utamaduni wake ni nakala ya wanadamu wengine waliokuwepo kabla yake miaka mingi iliyopita. Maoni ya Jung ni kwamba hata kama utu na mtu ni wa kibinafsi, mtu huyu huathiriwa na jamii inayomzunguka. Hawezi kamwe kuepukana na athari zake. Matambiko muhimu anayopitia mtu katika maisha yake, kama vile, sherehe za kumpa mtu jina, za kuingia jandoni na unyagoni, za ndoa na sherehe zinazohusu maziko baada ya mtu kuaga dunia huathiri maisha ya mtu binafsi. Baadhi ya sifa kongwe za mtu zimeazimwa kutokana na wanyama wa porini kama vile, paka, sungura, mbweha, dubu miongoni mwa wanyama wengine. Katika fasihi, mtunzi ataonyesha utu wake, mambo anayopenda na mambo anayochukia kupitia vikale.

Kutokana na maelezo ya Gunnep (1960), matambiko mbalimbali ambayo hukumba binadamu wote duniani yana uamilifu sawa kutoka enzi za zamani za mababu zetu hata ikiwa huwa utekelezaji wao ni tofautitofauti kulingana na jamii mbalimbali husika. Matambiko haya ni kama ujauzito na kuzaliwa kwa watoto, kipindi cha utotoni, kushiriki kwa wanadamu katika hafla mbalimbali katika jamii, tohara au jando, kuoa au kuolewa na hata kifo. Kutokana na madai haya, tunaweza kuchukulia kuwa kila jamii duniani huwa na shujaa wao ambaye mara nyingi hupewa sifa zilizo karibu sawa. Tujuavyo ni kuwa, shujaa ni mtu wa kawaida. Lakini kutokana na fikra zilizo katika akili laza za wanajamii mbalimbali tangu jadi, anachukuliwa kama kiumbe asiye wa kawaida na mwenye sifa za kiajabu ajabu. Sifa hizi apewazo shujaa kutoka jamii mbalimbali wengine wote (Gichamba 2005: 9-10 na 1996: 20-23).

Meyer (1993 na 2010), anaeleza kuwa nadharia hii huhusishwa sana na uhakiki wa visasili. Anadai kuwa wahakiki wa visasili hujishughulisha na ruwaza ambazo hujirudiarudia na ambazo hudhihirisha maana bia na tajriba za kimsingi za binadamu licha ya wakati au mahali wanamoishi. Kwa jumla, sifa, taswira, na mada zinazojumlisha maana na tajriba hizi ndizo hujulikana kama vikale. Vikale hushirikisha ishara bia ambazo huibua hisia na athari nzito kwenye akili laza ya msomaji wa fasihi.

Katika uhakiki wa kifasihi, vikale hutumiwa katika ruwaza ya aina za wahusika au taswira ambazo zinafanana katika tungo mbalimbali za kifasihi na pia katika visasili na mitindo anuwai ya kijamii. Kufanana katika maswala haya anuwai huchukuliwa kuakisi seti ya ruwaza bia ambazo zimekuwepo tangu jadi. Nadharia ya uhakiki wa vikale kwa hivyo inaeleza kuwa binadamu wote ni sawa popote walipo. Tofauti ni ndogo za kufikirika ambazo husababishwa na tofauti za kihistoria na za kimazingira.

Kwa mujibu wa Mutiso (1999:2), vikale kwa jumla hurejelea ruwaza za kimsingi. Ruwaza za jumla au bia za aina moja au nyingine ambazo aghalabu hudhihirika katika jamii za watu mbalimbali duniani. Anashikilia kuwa vikale humvuta msomaji vikitumiwa vizuri katika kazi ya fasihi.

Waitifaki wa nadharia ya vikale wanashikilia kwamba umaarufu wa kazi ya sanaa unatokana na wahusika, maudhui na taswira zinazorudiwarudiwa katika kazi husika. Baadhi ya wahusika wanaotumiwa kudhihirisha vikale ni kama: jaribosi au nguli anayeandaa safari ambayo mara

nyingi huanzia utotoni hadi anapofika utu uzima ambapo safari hii inaweza kuwa ya kikweli pale nguli anajizatiti kukisaka kitu au kujisaka mwenyewe. Katika nadharia ya vikale, mkinzani wa nguli huwa ni mhusika wa kikale ambaye hujifunga kibwebwe kuiharibu mipango ya nguli kwa kujaribu kumwangamiza. Aghalabu mhusika huyu huwa mzinzi, mlafi na wakati mwingine huwa tajiri. Hii inaafikiana na sifa za mkinzani wa mhusika mkuu katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* ambaye ni Daudi Mringwari na kwa kiasi fulani Wafarisayo na Wayahudi waliompinga ,kumkataa na hata kumfanyia njama ya kumuua Nabii Isa.

Kwa mujibu wa nadharia hii, jamii zote duniani huwa na mashujaa ambao aghalabu hupewa sifa zilizo karibu sawa. Shujaa, kwa kawaida, huwa ni kiumbe wa kawaida. Walakini, kutokana na mawazo yaliyo katika akili laza za wanadamu kutoka jadi,shujaa huchukuliwa kama kiumbe asiyekuwa wa kawaida.Yeye huchukuliwa kuwa kiumbe aliye na sifa za kiajabuajabu na za kipekee tofauti na wanajamii wengine wote. Kwa hivyo, sifa wapewazo mashujaa katika jamii mbalimbali duniani hushabahiana sana.

Nadharia ya vikale kutokana na ubia wake imekuwa yenye umuhimu katika utafiti huu kwa vile imetuongoza katika kulinganisha sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na za Nabii Isa na umuhimu wao kwa jamii zao.

### 1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Kuna data kubwa ya yaliyoandikwa kuhusu majagina duniani. Nyingi za kazi hizi ni za kinadharia na zimefafanua masuala anuwai kuhusiana na majagina kwa jumla. Kunazo tendi nyingi ambazo zina wahusika ambao wamesawiriwa kama majagina. Majagina au mashujaa wa

utendi wa Kiswahili ni kama vile Fumo Liyongo katika *Utendi wa Fumo Liyongo* wa Mohamed Kijumwa (1913), na Abushiri bin Salim katika *Utendi wa Vita vya Wadachi Kutamalaki Mrima*, wake Hemed Abdallah (1895), mtume Muhamadi na masahaba wake kama *Utendi wa Rasil Ghuli* na mashujaa wa kubuni kwa mfano Tajiri katika *Utendi wa Masahibu*. Tendi hizi pamoja na zingine kama vile *Utenz*i *wa Katirifu, Utenzi wa Siri li Asilali,* na *Utenzi wa kutawafu Nabii*, zina wahusika ambao wamechorwa kama majagina. Kazi zingine ni mahsusi na zinawamulika mashujaa wa jamii fulani, kama vile Shaka Zulu, Fumo Liyongo, Sundiata, Gautama Buddha na kadhalika. Tafiti nyingi zinaelezea jamii zilizowazaa na kuwakuza majagina hawa. Kazi hizi zote ni muhimu katika kuzipambanua sifa za majagina wa utafiti wetu na kuelezea umuhimu wao kwa jamii zilizowazaa na kuwalea.

Katika utafiti wetu hatukupata makala yaliyoandikwa yakimuangazia Nabii Isa kama shujaa. Makala ambayo tulipata kuyarejelea na ambayo yalitufaa sana katika kuelezea mazingira ya kuzaliwa, kukua na matendo ya Nabii Isa bali na *Utenzi wa Nabii Isa*, ni *Qurani* na *Bibilia* takatifu.

Kazi za mwanzo zilizoandikwa kumhusu shujaa Fumo Liyongo zilifanywa na Steere (1870), ambaye alikusanya katika maandishi ngano za Waswahili kama zilivyosimuliwa kwake na wakaaji wa Unguja. Ngano alizozichapisha ni kama *Hadithi ya Liyongo* (uk 456-471), *Mashairi ya Liyongo (*uk 456-471) na *Utumbuizo wa Gungu* (uk 474-483). Kazi hizi zimeufaa utafiti huu kwa kutupambanulia sifa za Fumo Liyongo na umuhimu wake kwa jamii ya Waswahili.

Kulingana na Gichamba (2005) Werner (1968), ni kazi inayotoa mkusanyiko wa maelezo kuhusu visasili na visakale vya baadhi ya Wabantu, Waswahili wakiwa baadhi yao. Mwandishi anadai kuwa Wabantu, licha ya uhusiano katika lugha, wana mila na desturi nyingi zinazofanana. Kazi hii imetufaa katika utafiti huu kwani kufanana huku kumetuwezesha kuwatazama majagina wa utafiti wetu kiulinganishi. Katika kuirejelea *Hadithi ya Liyongo* (uk. 145-154), ametoa maelezo muhimu kwa utafiti huu kuhusu aila ya Liyongo na mgogoro uliokuwepo baina yake na nduguye Daudi Mringwari. Mgogoro huu ni muhimu katika kuiunda historia ya shujaa huyu. Werner (khj), vilevile amewazungumzia mashujaa wengine wa Kibantu na kuzungumzia shughuli na fenomena mbalimbali katika jamii ya wabantu anamotoka shujaa Fumo Liyongo.

Knapert (1979), ametoa maelezo kuhusu kipindi alichoishi Fumo Liyongo pamoja na maelezo mengine muhimu kumhusu Liyongo na tungo zake. Kazi nyingine ya mwandishi huyu iliyofaa utafiti wetu ni ile ya mkusanyiko wa visasili na visakale vya Waswahili *(Myths and Legends of the Swahili* (1970). Kazi hizi za fasihi simulizi ya hapo kale zilichota kwa upana maudhui yake kutokana na hali na migogoro ya kijamii iliyopo. Mtalaa wa kazi hizi umetupa taswira angavu ya jamii zinazopatikana.

Katika kuelewa kwa kina historia ya Pate alikotembelea Fumo Liyongo, tumerejelea *Utenzi wa Al- Inkishafi*. Utenzi huu unarejelea maanguko ya mji huo chini ya utawala wa Wareno. Vile vile, utenzi huu unatusawiria hali ya mji huu kabla ya maanguko na kutuonyesha ustawi wake. Hali hii imetusaidia kuelewa mfumo wa kijamii wa mji huu wakati alipoishi Liyongo.

Nurse na Spear (1985), kama walivyonukuliwa na Gichamba (2004), waliangazia historia ya Waswahili pamoja na lugha ya Kiswahili baina ya karne ya saba na kumi na nne (800-1400 B.K). Waandishi hawa wameelezea maswala muhimu kama vile, utamaduni asilia wa Waswahili, asili ya lahaja mbalimbali za Kiswahili, kuibuka kwa miji mbalimbali ya Waswahili kama vile Mogadishu, Kilwa, Pate, Lamu, Malindi na Mombasa kutokana na kupanuka kwa jamii ya Waswahili; miundo ya kijamii na kiutawala katika miji mbalimbali; hali ya kiuchumi katika jamii hii; na maingiliano baina ya Waswahili na watu kutoka jamii zingine za Kiafrika, za Mashariki ya Kati na sehemu zingine ulimwenguni. Kazi hii imefaa sana utafiti wetu kwani ilitoa mwanga kuhusu hali ilivyokuwa katika kipindi alichoishi Liyongo.

Tasnifu zinazotalii suala la majagina na zilizochapishwa katika lugha ya Kiswahili si nyingi. Mutiso (1985) aliangalia hurafa - linganishi juu ya majagina. Aliirejelea *Kasida ya Hamziyya* katika kumlinganisha mtume Muhammed na mashujaa wengine katika hurafa na uyakinifu katika kasida hiyo. Kazi hii ni muhimu kwetu kwani ni mojawapo wa kazi ambazo zimeorodhesha sifa bia za majagina, ambazo ndizo msingi tulioutumia katika kuwafafanulia majagina wetu Fumo Liyongo na Nabii Isa.

Mberia (1989), anamtazama Liyongo kama shujaa wa masimulizi katika ngano za Waswahili. Katika makala haya, mwandishi ametoa sifa tano za Liyongo na kudai kuwa sifa hizi ni bia kwa mashujaa wote na kwamba zinapatikana katika masimulizi ya mataifa mengine duniani. Sifa hizi ni ujasiri au ushupavu, nguvu za kimwili, nasaba au cheo, wepesi wa akili na usanii (stadi katika gungu na mwao). Aidha, anatoa ngano kumhusu Sundiata ili kuonyesha ulinganifu kati ya mashujaa hawa wawili. Utafiti wetu ni tofauti na utafiti huu kwa kuwa bali na sifa tano

alizoziorodhesha mtafiti huyu, tutadhibitisha kuwa zipo sifa nyingine za mashujaa kama urijali, kupenda haki, “uungu-mtu” n.k. Aidha, utafiti huu umemwangazia Liyongo kama mhusika wa kihistoria na wala si mhusika katika ngano, na ambaye tumemlinganisha na Isa, ambaye ni shujaa wa kidini.

Mutiso (1999), anatazama kiulinganishi maisha na sifa za majagina wawili wa kidini, Muhammadi na Buddha, huku akirejelea sifa bia za mashujaa. Katika kuwaangazia majagina hawa, makala haya yamewataja majagina wengine duniani kama vile Nabii Musa, Nabii Isa, Samshoni, Shaka Zulu na Fumo Liyongo miongoni mwa wengine. Utafiti wetu umelinganisha sifa za Fumo Liyongo kama shujaa wa kihistoria, na Nabii Isa kama shujaa wa kidini, na kuelezea umuhimu wao kwa jamii zao. Mambo haya hayajashughulikiwa na makala haya. Hata hivyo, makala haya ni muhimu kwetu kwani yameelezea kuhusu zawadi ya jagina kwa umma wake, kama mojawapo ya sifa za jagina. Anadai kuwa Waswahili waliachiwa gungu na Fumo Liyongo.

Miehe na wenzake (2004), wamekusanya nyimbo pamoja na mashairi ambayo yanadaiwa kutungwa na Fumo Liyongo. Mashairi haya pamoja na nyimbo hizi zilidondolewa kutoka kwa kazi za awali zilizochapishwa, ilhali nyingine walizitoa kutoka maktaba na hifadhi za nyaraka mbalimbali katika taasisi mbalimbali ulimwenguni. Kazi hii ni zao la warsha kadhaa zilizofanyika huko Bayreuth Ujerumani, kati ya mwaka wa 2003 na 2004. Lengo kuu la warsha hii lilikuwa ni kutalii na kuchambua mashairi na nyimbo zinazohusishwa na Fumo Liyongo ili kuibuka na toleo kamilifu ambalo lingekidhi mahitaji ya kiusomi kote duniani. Bali na kuzionyesha tungo hizo za Liyongo, wametoa maelezo kuhusiana na utamaduni wake, fani

zilizotumiwa katika tungo hizi, miongoni mwa masuala mengine muhimu katika utamaduni wa Waswahili. Kazi hii ilikuwa msingi mmojawapo wa kufafanulia masuala kadhaa kuhusiana na utamaduni wa Fumo Liyongo.

Gichamba (2004), amewalinganisha mashujaa wawili wa kihistoria - Fumo Liyongo wa Waswahili, na Shaka Zulu wa Wazulu. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu amewalinganisha mashujaa wawili wa kihistoria na wa kutoka katika eneo moja la Afrika. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa kuwa wetu unamlinganisha shujaa wa kidini, na mwingine wa kihistoria. Aidha, mashujaa hawa ni wa kutoka maeneo mawili tofauti kijiografia.

Achieng (2012), pia aliangazia sifa za mashujaa na umuhimu wao kwa jamii zao huku akimlinganisha Fumo Liyongo wa Waswahili  na Lwanda Magere wa Wajaluo. Katika uhakiki wake, aliweza kufafanua sifa za mashujaa wa kijamii na hii kazi yake ilitufaa zaidi katika kufafanua sifa za mashujaa wa kidini na wa kihistoria katika *Utenzi Nabii Isa.*

Ndumbaro (2013), ameshughulikia dhana ya shujaa wa tendi kwa jumla, na matatizo mbalimbali ya kijamii katika maisha ya shujaa. Katika utafiti huu, mtafiti anahitimisha kuwa shujaaa hupatwa na matatizo kama wanavyopatwa watu wengine katika jamii, ila sihiri au nguvu alizo nazo shujaa zisizoweza kuelezeka humfanya shujaa kuwa na upekee katika ufumbuzi wa matatizo hayo. Utafiti huu ulitufaa katika utafiti wetu kwa sababu ulitutolea mwanga kuhusu jinsi majagina huyakabili matatizo yanayowakuba.

Kalinjuma (2013), amejadili suala la jaala ya shujaa wa tendi za Kiafrika na shujaa wa tendi za Kimagharibi. Alizingatia jaala ya tendi na ukweli kuhusu mambo yanayofungamana na jaala yake. Mtafiti huyu anahitimisha kuwa jaala ya shujaa inaonekana kufanana kati ya majagina wa Kiafrika na wa Kimagharibi kwani matukio wanayofanya ni yaleyale ya kishujaa yenye kuambatana na matukio yanayofasiliwa kuwa si ya kawaida, na ni ya kushangaza kwa jamii zao. Kazi hii inatuthibitishia kauli kuwa mashujaa wote huwa sifa zinazokaribiana sana.

Katika utafiti wetu, kazi tuliyoipata inayomwangazia Nabii Isa kama shujaa wa kidini ni ile ya Achieng (2013), aliyeyahakiki maudhui katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Kazi hii Ilitufaa katika utafiti wetu kwa sababu, moja kati ya maudhui yalioangaziwa katika utenzi huu ni ujagina. Hivyo, kazi hii ilitutolea mwanga zaidi kuhusu ujagina wa Isa kama unavyojitokeza katika utenzi huu.

Aidha, bali na *Utenzi wa Nabii Isa*, tumerejelea mtandao pamoja na *Qurani* tukufu na *Bibilia* takatifu ili kuangazia sifa zaidi za ushujaa wa Isa pamoja na kujenga uelewa wa kina wa mazingira yaliyomzaa shujaa Isa, pamoja na umuhimu wake kwa umma wake.

Kwa jumla, kunazo kazi nyingi sana ambazo zimeandikwa kuhusiana na Fumo Liyongo na Nabii Isa. Kazi ambazo tumezirejelea ni baadhi tu ya kazi nyingi zinazowasawiri majagina wa utafiti huu. Kwa kuwashughulikia Nabii Isa na Fumo Liyongo kiulinganishi, utafiti huu umenuia kulijaza pengo la kiusomi ambalo limekuwepo. Hakuna utafiti tuujuao unaomlinganisha jagina wa kidini na jagina wa kihistoria, na kuelezea kwa kina umuhimu au mchango wao kwa jamii zao.

### 1.9 Mbinu za Utafiti

Utafiti wetu umekuwa ni wa maktabani. Tumesoma vitabu vya kihistoria kuhusu historia ya Waswahili, Wayahudi, hali za kijamii na mazingira yaliyowazaa Fumo Liyongo na Nabii Isa. Habari tulizozipata katika vitabu mbalimbali zimetusaidia kueleza historia ya Fumo Liyongo na Nabii Isa, ikifungamanishwa na historia ya Waswahili na Wayahudi mtawalia.

Pia, kupitia usomaji wetu wa makala mbalimbali maktabani, tumejaribu kutambua, kuchunguza na kujitokeza na sifa bia za kishujaa na umuhimu wa mashujaa wetu kwa jamii zao. Fauka ya hayo, tumezisoma tasnifu, makala, na majarida mbalimbali yanayohusiana na somo letu la utafiti.

Aidha tumeyasoma mashairi na nyimbo zilizotungwa na watu mbalimbali kuhusu Fumo Liyongo, na hata yale yanayodaiwa kutungwa na yeye mwenyewe. Mashairi haya yametusaidia kumwelewa Fumo Liyongo kwa kina. Tumeelewa sifa zake za kishujaa, historia yake ikifungamanishwa na ya Waswahili, na hata umuhimu wake kwa jamii ya Waswahili. Tumetafuta habari pia katika mitandao na tovuti mbalimbali ambazo tumeweza kuzifikia na ambazo zinasheheni habari kuhusiana na utafiti wetu.

### 1.10 Hitimisho

Mada yetu ya utafiti inahusu taswira ya jagina katika tendi za Kiswahili, ambapo tunamlinganisha Nabii Isa ambaye ni shujaa wa kidini, na Fumo Liyongo ambaye ni shujaa wa kihistoria. Hawa ni mashujaa wa vipindi, jamii na maeneo tofauti. Ulinganishi wa jagina wa kidini na wa kihistoria haujafanywa hapo mbeleni, na tafiti za aina hii zitachangia katika

kuthibitisha kuwa sira za majagina katika ulimwengu mzima zinafanana sana. Pia, utachangia katika kudhihirisha umuhimu wa mashujaa hawa kwa jamii zao, na kwa ulimwengu mzima kwa jumla.

# SURA YA PILI

# HISTORIA YA FUMO LIYONGO NA NABII ISA PAMOJA NA ILE YA JAMII ILIYOWAZAA NA KUWAKUZA

## 2.0 Utangulizi

Majagina huzuka katika mfumo na hali fulani mahsusi za kijamii, kama tulivyodokeza katika sura ya kwanza. Hivyo, ni muhimu kuielewa historia za jamii walimopatikana Fumo Liyongo na Nabii Isa. Historia hii itachangia katika kuwaelewa mashujaa hawa kwa kina hususan, maisha yao, mazingira na hali zilizowazaa pamoja na vipindi vya wakati walipozuka. Hivyo, katika sura hii tumeangazia vipengele vya maisha yao, kama vile miondoko yao, vitushi walivyovitenda na mahusiano kati yao na wanajamii wengine. Tumemulika mitafaruku ya kisiasa ya jamii zilizowazaa. Tumeangazia vilevile, historia ya Waswahili, na pia ile ya Wayahudi, katika vipindi mbalimbali kama vile, kabla ya kuzuka kwa majagina hawa, vipindi walimoishi na hata baada ya vifo vyao.

## 2.1 Historia ya Waswahili

Historia ya Waswahili imeundwa kutokana na visasili pamoja na visakale vilivyopitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya utambaji. Fasihi simulizi kama vile visasili na visakale vilisaidia pakubwa kuunda historia ya Kiswahili. Aidha, wazungu kama vile Werner (1915), Dammann (1940), Sutton (1966), Nurse (1994), Knappert (1970 na 1970) Lyndon (1962), Greenville (1954 na 1955), Allen (1977), Spear (1985), miongoni mwa wengine walikusanya tamaduni za Waswahili kutoka kwa wenyeji wa pwani na kuzihifadhi katika maandishi. Vilevile, mwanaakiolojia Chitick (1984), kutokana na uchimbaji wake wa kitaalam wa maeneo kama Gedi, Manda na Pate yaliyoachwa kama mahame au magofu kutokana na misukosuko mingi

iliyotokea katika eneo la pwani hapo awali, pia umechangia pakubwa katika uelewaji wa baadhi ya tamaduni za watu waliokuwa wakiishi katika maeneo hayo. Chittick (1984) katika uchimbaji wake alikusanya vyombo kama vile, vyungu, mifupa, mbao, vyombo vya mawe, vioo, shanga, vifaa vya vyuma, sarafu n.k.Vifaa hivi vinasaidia katika uelewaji wa tamaduni za jamii za pwani na Waswahili wa awali pamoja na historia zao.

Visasili vya jamii jirani na Waswahili kama vile, Wapokomo, Wasegeju na Wamijikenda na hata maandishi ya awali ya watalii wa kwanza kabisa kuzuru maeneo ya pwani na Afrika Mashariki yalichangia pakubwa. Mathalan, kijitabu cha *The Periplus of the Erythrean Sea,* kilichoandikwa baina ya karne ya kwanza na ile ya tatu baada ya Kristo na Mgiriki asiyejulikana kwa jina, kilichangia pakubwa katika uelewaji wa historia ya Waswahili. Kitabu hiki, kwa mujibu wa Sutton (1966:6), kinaelezea baadhi ya sehemu za upwa na bahari ya Hindi zikiwemo sehemu za bandari zilizoko katika bahari ya Shamu na Ghuba la Aden, pamoja na maelezo kuhusu safari za mashua kuelekea Uhindi zikitegemea pepo za misimu (pepo za Kaskazi na Kusi). Mgiriki huyu aliurejelea Upwa na Upembe wa Afrika kama Azania. Kijitabu hiki kilikuwa nguzo muhimu katika maelezo ya Ptolemy kuhusiana na Jiografia ya Upwa wa Afrika Mashariki.

Waswahili ni Wabantu. Asili ya Wabantu ni katika eneo ambalo hivi sasa linakaliwa na nchi ya Cameroon na eneo la Mashariki mwa nchi ya Nigeria. Nurse na Spear (1985) wanadai kuwa baadhi yao walihamia katika janibu za Kusini mwa Afrika, ilhali wengine wakiwemo Waswahili, walihamia Mashariki na kukalia eneo la Shungwaya.Wanadai kuwa Khoisan (Bushmen na Hottentots) ndio walikuwa jamii ya awali kabisa katika eneo la Afrika Masharaki, kabla ya Wabantu, Wakushi na Wanailoti kuhamia kutoka hivyo, kabla ya kuwasili kwa Wabantu katika

maeneo ya Afrika Mashariki, Wakushi wa kusini tayari walikuwa wakimiliki maeneo haya kwa mujibu wa Nurse na Spear (khj 45) .

Walsh (1987:21), akinukuliwa na Gichamba (2005:26), anaeleza kuwa wazungumzaji wa lugha ya Sabaki waliotoka katika sehemu zilizoko kwenye meaneo ya Kaskazini Mashariki ya Tanzania, walipokuwa wakipitia kwenye maeneo yaliyokuwa yamekaliwa na kumilikiwa na Wakushi hao, hawakuwa na maathiriano wala maingiliano kati yao. Walsh (khj: 21) anadai kuwa Wasabaki walitengana na Wabantu wengine katika eneo la Kaskazini mwa nchi ya Tanzania na kuelekea katika maeneo ya Kaskazini katika kipindi cha karne ya kwanza baada ya Kristo. Mwishoni wa karne ya kwanza, kutoka eneo la Wasabaki lilitengana katika makabila tofauti tofauti kama vile, Waswahili, Wapokomo, Waelwana na Wamijikenda. Baada ya kipindi kifupi, Waswahili walihamia sehemu za Kusini mkabala wa bahari ya Hindi. Hata hivyo, Wamijikenda, Wapokomo waliwafuata tu baadaye. Ni katika kipindi hiki ambapo Wakushi waliokataa kumiliki maeneo ya kusini waliingiliana na Wabantu na baadhi yao wakasilimishwa kuwa Wabantu.

Tamaduni za jamii mbalimbali za Waswahili zinadai kuwa kugura kwao hadi katika maeneo ya Pwani kulitokana na mashambulizi ya mara kwa mara ya Wagalla. Stilahi (1981:858) akinukuliwa na Gichamba (2005:26), anadokeza kuwa Wabajuni katika tamaduni zao wanadai kwa yakini kuwa Wagalla ndio waliowafukuza kutoka eneo la Shungwaya. Aidha, Werner (1915:328) anashadidia kwa kusema kuwa mashambulizi mara kwa mara ya Wagalla ndiyo yaliyowafanya Wasabaki kukimbilia katika sehemu za Kusini. Hata hivyo, mashambulizi haya hayakusita hata baada ya kuhamia pande za kusini. Nurse (1994:48) anadai kuwa magurio ya Waswahili na Wabantu wengine kusini zaidi yalizidishwa na vamio la ghafla la Waarabu.

Mashambulizi haya yaliwafanya Wabantu kuhamia katika eneo lililoko baina ya Juba kati ya eneo la kusini mwa Wabantu, kuhamia katika eneo lililoko baina ya Mto juba, ulio kati ya eneo la Kusini mwa Somalia na mto Tana.

Katika maeneo ya pwani, Waswahili walijikusanya katika makundi madogomadogo kwenye visiwa na sehemu nyingine mbali kidogo na ufuko. Walitapakaa pwani kote kuanzia Somalia na kuteremka hadi Msumbiji, mazingira yao ya bahari na mito ikiwatumbukiza katika shughuli za uvuvi. Kwa hivyo, walijingiza katika utengenezaji wa mitumbwi, jahazi, makasia, nyavu, nyugwe, nk. Bali na uvuvi, kama njia ya kiuchumi, shughuli zingine za asili za kibantu zilikuwa pamoja na ufugaji wa wanyama kama vile, mbuzi, ng'ombe, kondoo na kuku. Kilimo cha mpunga, malenge, mtama, nazi, mboga na matunda, mawele na jamii ya kunde kama vile njegere na maharagwe, pia kiliendelezwa na Waswahili. Ndizi na yugwa zililetwa hapo baadaye kutoka sehemu za kusini mashariki ya bara la Asia. Shughuli za uhunzi ziliwawezesha kuunda na kutengeneza zana za kilimo kama vile mashoka, majembe, panga na visu. Vifaa hivi vilitumiwa kufyeka mashamba bikira, kupanda, kuvuna na kupalilia. Isitoshe, walishughulika na uudanji wa zana za kivita kama mishale, nyuta, mafumo, vitara, jambia, ngao, misu na panga. Baadhi ya vifaa vingine walivyoviunda ni pamoja na vinu, mchi, kamba, vyano vya kupepetea na vinoo/tupa. Useremara pia uliendelezwa ili kuunda baadhi ya vifaa vya nyumbani.

Mandhari ya bahari yaliwezesha usafiri au safari ya Waswahili kutoka sehemu moja hadi nyingine katika shughuli mbalimbali kama vile, shughuli za kibiashara na kuwatembelea jamaa zao. Aidha, wageni kutoka maeneo mengine ya ulimwengu walifika hadi pwani ya Afrika Mashariki, Mazingira haya yalileta mabadiliko makubwa katika utamaduni na muundo wa

kijamii ya Waswahili, kisiasa na kiuchumi. Wageni wa awali katika maeneo haya walikuwa ni wafanyi biashara, wasomi (wanajiografia), wamishenari na watalii walioabiri mashua. Hao wageni walitoka sehemu kama vile, Uarabuni, Ghuba ya Uajemi, Uhindi, Ugiriki, Ureno zikiwemo sehemu nyingine ulimwenguni haswa maeneo ambayo yamepakana na fukwe za bahari. Wareno walifika baadaye, na mwisho kufika walikuwa Waingereza waliokuwa na nia ya kujitwalia maeneo muhimu pamoja na kusambaza dini.

Miongoni mwa waandishi na wanajiografia wote wa kiarabu wa enzi za kati (baina ya miaka 1100 – 1500) wanaoirejelea Afrika Mashariki, Freeman Greenville (1954 – 1955:1) akinukuliwa na Gichamba (2005:28), anadai kuwa hakuna mwandishi aliyeitembelea pwani ya Afrika Mashariki ambayo kwa sasa inajumuisha pwani za Somalia, Kenya na Tanzania ila tu Muhammed ibn Abdallah ibn Batuta ambaye aghalabu hujulikana kama ibn Batuta. Uhusiano wake na wenyeji, ustaarabu wake na uelewa wa mandhari ya Afrika Masharaki ulisaidia pakubwa kuelewa historia ya watu wa pwani ya Afrika Masharaki.

Wafanyi biashara walisaidiwa na pepo za Kusi na Kaskazi katika safari yao ya kuja na kuondoka pwani mtawalia.Waarabu,Wahindi na Wajemi walitumia msimu wa pepo za Kaskazi zilizokuwa zikianza kuvuma katika mwezi wa Novemba hadi mwezi wa Februari ili kufika pwani ya Afrika Mashariki. Baada ya shughuli zao za biashara kukamilika, walirudi makwao kwa pepo za Kusi zilizoanza kuvuma baaada ya pepo za Kaskazi kutua.

Bidhaa kama mbao, dhahabu, pembe za ndovu, magome ya kobe, watumwa waliotekwa kutoka bara, rangi za nguo, manukato, miongoni mwa bidhaa zingine zilinunuliwa na wageni waliofika

pwani ya Afrika Mashariki kwa shughuli ya biashara. Waswahili nao, walinunua bidhaa kama majora ya vitambaa, vyungu, shanga za vioo, vitara, vyombo vya vioo vya nyumbani, mvinyo, shaba na ngano miongoni mwa bidhaa zingine kutoka kwa wageni hao.

Vijiji vilianza kupanuka na kuwa miji tu biashara ilipozidi kushamiri. Miji ilikuwa kama vile Mogadishu, Lamu, Pemba, Unguja, Malindi, Barawa, Kilwa, Gedi, Pate nk. Baadhi ya wageni kama vile Waarabu walikuja na familia zao na kustakimu katika eneo la pwani. Allen (1993:7), anadai kuwa Waajemi na Waarabu ndio waliokuwa waasisi wa ustaarabu katika eneo hilo. Walikuwa wakitumia pepo za misimu katika bahari ya Hindi ili kufika pwani ya Afrika Mashariki kwa muda wa miaka elfu mbili au zaidi. Fauka ya biashara, Waarabu walichukua Waswahili kuwa makafiri kwa sababu ya imani zao katika mapango, sayari za anga ya juu, nyota jua hata mwezi. Kwa sababu hiyo, walisambaza dini ya kiislamu. Dini ya kiislamu ilikuja na athari zake katika janibu hizo ambapo hadi sasa baadhi ya watu hawawezi kubainisha kati ya Uislamu (dini) na Uswahili (utamaduni wa Waswahili), matambiko na sherehe nyingine, mathalan, Maulidi zinahusishwa na Uislamu.

Katika mpito wa vipindi mbalimbali vya kihistoria, jamii ya Waswahili imekuwa na hali, misukosuko ya kila aina na mafarakano yaliyozuka na kusababisha vita kati ya jamii ya Waswahili wenyewe. Vita hivi vilisababisha vifo na uharibifu mkubwa wa mali. Aidha, mashambulizi ya mara kwa mara kutoka kwa majirani hasa walioishi bara kama vile Wasanye (Waboni), Walangulo, Wadahalo, Wagalla na Wasegeju yalikithiri. Mitafaruku hii ilitokea baina ya karne ya kumi na mbili na karne ya kumi na tano ambapo Waswahili walikuwa na taabu na

maisha yao kuvurugika kiasi cha kumtaka mtu wa kuwaongoza na kuwaunganisha. Ni kwa sababu hii, ndipo shujaa wao, Fumo Liyongo akazuka.

### 2.2 Historia ya Fumo Liyongo

Fumo Liyongo alizuka kutokana na misukosuko ya kivita iliyokuwa imeshamiri katika upwa wa Afrika Masharaki kwa muda mrefu. Maelezo yake yanapatikana hapa na pale na yametokana na tamaduni za jamii mbalimbali za pwani. Hata hivyo, kuna ukuruba au uwiano wa aina fulani kuhusiana na maelezo tofautitofauti ambayo yalipitishwa kwa muda mrefu kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya utambaji. Kuna maandishi chungu nzima ambayo yameandikwa na maulama mbalimbali kumhusu Fumo Liyongo. Isitoshe, kumekuwepo na mijadala mirefu kuhusu iwapo shujaa huyu wa Waswahili aliwahi kuishi na ikiwa kweli aliishi, kama alikuwa na sifa ambazo amepewa. Kwetu sisi, hatuna shaka kwamba Fumo Liyongo aliwahi kuishi na kwamba alikuwa na sifa za kipekee - sifa zilizokuwa tofauti na zile za wanajamii wengine. Yumkini, sifa hizi zinaweza zikatiliwa chumvi katika maandishi ya kifasihi yanayomsawiri na hii ni kaida ya mashujaa wote duniani. Shujaa hukuzwa na wanajamii ambao humwona kama kiumbe wa ajabu mno. Licha ya hayo, tumeyadokeza mazingira na hali ya kijamii ambayo ilimzua Fumo Liyongo. Hali kama hii hudhihirika katika uzukaji wa majagina wengine duniani.

Mengi ya maandishi ya awali yanayomhusu Liyongo yalikusanywa na Wazungu kana vile: Werner (1915), Dammann (1940), Sutton (1966), Nurse (1994), Knappert (1970 na 1970) Lyndon (1962), Greenville (1954 na 1955), Allen (1977), Spear (1985) miongoni mwa Wazungu wengine. Waafrika wa awali walioandika masuala kumhusu Liyongo, kwa mfano Muhammad Kijumwa (katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*), walifanya hivyo kwa hisani ya Wazungu ambao

walikuwa wakifanya utafiti kuhusu Liyongo. Wazungu walikusanya fani mbalimbali za fasihi simulizi ya Kiswahili na kuzitia katika maandishi. Miehe na wenzake (2004:8) wanaeleza kuwa, licha ya juhudi za Wazungu za kukusanya tamaduni kumhusu Liyongo na kuziweka katika maandishi, Waafrika wachache kama vile Ahmed Nabahany na Ahmed Nassir pasipo utegemezi wa Wazungu wamefanya juhudi za kukusanya na kuweka katika maandishi baadhi ya tamaduni za watu wa Lamu na Mombasa zikiwemo tamaduni kumhusu Liyongo.

Haijulikani kwa yakini ni lini Liyongo alizaliwa lakini wasomi wanakisia kwamba aliishi takribani kati ya karne ya kumi na tatu na kumi na tano. Liyongo hakuwa shujaa wa Waswahili tu, bali anatajwa pia katika utamaduni, kwa mfano wa Wapokomo. Ikumbukwe kwamba, Waswahili walioona na baadhi ya majirani zao na kwa hivyo, mengi ya makabila yalidai kuwa Liyongo alikuwa shujaa wao. Ni kawaida kwamba, mwanadamu yeyote duniani hupenda kujihusisha na mtu ambaye ni maarufu. Mamake alijulikana kwa jina Mwana Mbwasho ilhali babake alikuwa Mringwari wa kwanza. Kijakazi wake alikuwa Saada na anadhihirika mno katika tungo ambazo zinadaiwa Liyongo amezitunga. Mpenzi wake alijulikana kwa jina Kundazi. Kwa mujibu wa Miehe na wenzake (khj: 5), tamaduni kumhusu Liyongo na jamaa wake wa karibu kama vile mamake, kijakazi chake, mpenziwe na mpinzani na adui wake mkubwa kwa jina Daudi Mringwari, zimehifadhiwa akilini mwa watu wa pwani, na zimekuwa sehemu muhimu ya urithi wa utamaduni wa kitaifa wa Kenya na hata Tanzania, Isitoshe, kiini cha utamaduni wa Liyongo huhusishwa na nyimbo za sifa na uchezaji ngoma na nyingi za nyimbo hizi bado zipo kwenye fikra za wazee waliokoma wa Mombasa na Lamu.

Wapokomo katika tamaduni zao wanadai kuwa Liyongo alikuwa mtawala wa dola ya Ozi (katika karne ya kumi na tano) iliyokuwa katika upande wa chini wa Mto Tana, (kuna madai kwamba Liyongo alikuwa akitembelea ufuko wa mto Tana ili kufua nguo zake pamoja na kuoga), lakini baadaye alipinduliwa na dola ya Pate na ufalme wake kutwaliwa (Allen 1993:95). Mji mkuu wa dola hii ulikuwa Shaka kwa mujibu wa *Tarihi ya Pate*, Inadaiwa kuwa Liyongo alipanua ufalme wake kutoka Malindi hadi janibu za Wapokomo, eneo ambalo ni mkabala na hori la kisiwa cha Pate. Liyongo mwenyewe, kama mtawala wa dola hii, hakupendwa na Wapokomo. Jambo hili lillitokana hasa na kodi aliyowatoza. Vijiji vikubwa vilitozwa kodi ya wasichana wawili na wavulana wawili, ilhali vijiji vidogo vilitozwa kodi ya msichana mmoja na mvulana mmoja kutoka kila kijiji, miongoni mwa kodi zingine na hasa kutoka kwa mazao ya kilimo. Hali hii ya kumchukia inadhirika katika maelezo ya *Hadithi ya Liyongo* (Steere 1970:339 – 452). Katika hadithi hii anasawiriwa kama mtu mbaya-aliyekuwa anawaudhi watu sana. Hadithi hii ilisimuliwa kwake Steere na Hamisi wa Kayi (Khamis bin Abubakar) huko Unguja.

Hata hivyo, utamaduni wa Waswahili unadai kuwa Liyongo alipendwa sana na watu. Hali hii inadhihirika katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, pale ambapo baada ya kifo chake, watu wengi walisikitika na kuhuzunika. Hata hivyo, kama ilivyo kawaida ya wanadamu kote duniani, si watu wote walihuzunika. Maadui zake walifurahia kwa vile tisho lao kubwa lilikuwa tayari limeondolewa.

**2.3 Misukosuko ya Kivita Iliyomzua Fumo Liyongo**

Jamii ya Waswahili awali ilipitia taabu na misukosuko mingi. Vita mbalimbali vimeelezwa haswa katika visasili na visakale vya jamii ya Waswahili wakiwemo majirani zao kama Wagalla, Wasegeju na Wapokomo kuhusika.

Biashara ya watumwa iliyoendelezwa na Waarabu ilisababisha mitafaruku katika jamii mbalimbali zikiwemo za bara na za pwani. Waarabu waliokuwa na bunduki na panga waliwashika na kuwateka nyara Waafrika na kuwasafirisha hadi eneo la Mashariki ya Kati zikiwemo sehemu nyingine ulimwenguni. Aidha, Waarabu walishirikiana na baadhi ya Waafrika kuwasaidia katika shughuli zao za utekaji wa watumwa kutoka bara. Watumwa hawa walifunganishwa kwa kamba au minyororo shingoni. Hatimaye walisafirishwa kwenye mazingira yenye hatari mno wakiwa wametwikwa baadhi ya bidhaa kutoka pwani. Nyumba zao zilichomwa kwa moto na watoto wao kuuawa. Wengi wa mateka hawa walijifilia njiani. Waliokuwa hawajiwezi kwa sababu ya uchovu au ugonjwa walitumbukizwa baharini wakiwa wamefungwa kwa kamba na minyororo miguuni au mikononi. Maelezo haya ni kwa mujibu wa Mbotela (1934). Shughuli za utekaji wa watumwa ilikuwa ni sababu ya vita vya mara kwa mara kati ya Waarabu na wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki, Waswahili wakiwemo, na hata watu wa bara.

Licha ya hayo, jamii za Waswahili kutoka sehemu mbalimbali zilipigana vita.Wafalme wa dola mbalimbali walichukua kila hatua kuimarisha utawala wao. Kwa mfano *Utenzi wa Fumo Liyongo* unaeleza kuwa Daudi Mringwari (binamuye Liyongo), alihofia Fumo Liyongo angefanya mapinduzi dhidi ya utawala wake, kwa hivyo, alifanya njama zilizomwangamiza

Liyongo. Sutton (1966:18-19) anaeleza kuwa kati ya miaka 1200 na 1500B.K, kulikuwepo na ugomvi, mitafaruku na mashambulizi baina ya dola mbalimbali au baina ya makundi yaliyokuwa yakizozana katika dola hizo. Anaendelea kusema kuwa masultani wa awali wa Kilwa walikuwa na matatizo na majirani zao. Anadai kuwa hata *Tarihi ya Pate* inatueleza kuhusu mapigano, uporaji na mapinduzi katika visiwa vya Bajuni ukiwemo umwagikaji mwingi wa damu na uharibifu wa mali katika kisiwa cha Pate. Pia, Malindi ilizozana na Mombasa hadi baada ya Wareno kuingilia kati kwa kutumia bunduki ambapo uporaji mkubwa ulitokea katika mji wa Mombasa. Kumekuwa na madai kuwa kudorora kiuchumi na kisiasa kwa mji wa Kilwa mwishoni mwa karne ya kumi na nne kulilingana na kuinuka kwa mji wa Pate kulisababisha utekaji katika maeneo mbalimbali ya pwani kutoka Mogadishu hadi katika Visiwa vya Kirimba vilivyo pande za Kusini.

Majirani wa Waswahili pia kama tulivyodokeza awali, walikuwa tisho kwa usalama na utangamano wa Waswahili. Mashambulizi haya hayakutelelezwa dhidi ya Waswahili pekee bali pia Wapokomo, Wasegeju na makundi mengine ya Wamijikenda. Kwa mfano, Wagalla wanaelezwa katika tamaduni mbalimbali katika janibu za pwani kama watu wakatili. Hata baada ya Wagalla hao kuwatimua Waswahili na makundi mengine kutoka Shungwaya, bado waliwafuata hadi sehemu za Kusini na kuzidisha mashambulizi yao. Werner (1915:328) anatoa mfano wa Wasegeju na Wakauma waliotoroka makao yao ili kuhepa Wagalla waliokuwa wakatili na wenye nguvu za kivita. Anadokeza kuwa baadhi ya Wapokomo walitekwa na Wagalla na kufanywa watumwa wao. Tamaduni za Wapokomo hata hivyo, zinaeleza kuwa Wapokomo wengine walijificha mashimoni karibu na fuo za mito kisha Wagalla waliokuja kulisha mifugo yao walifumwa na mishale yenye sumu. Hatimaye, Wagalla walitorokea sehemu

za chini za mto.Wapokomo nao wakawafuata mara tu usiku ulipoingia kwa kutumia mitumbwi midogomidogo na kuwaua. Baada ya mauaji, walificha mitumbwi yao chini ya mto kwenye mchanga.

Baadaye Wagalla walichoka na vita kisha wakajaribu kufanya urafiki na Wapokomo. Kila kundi hatimaye liliapa kutolishambulia lingine. Kwa mujibu wa tamaduni za Wamijikenda na Waswahili, nyumba zao (Waswahili) awali zilikuwa zimeezekwa kwa nyasi kwenye paa na hata kwenye pande zake. Kwa hivyo, ilikuwa rahisi kwa Wagallla kuwafuma mikuki kutoka nje walipokuwa wakilala. Allen (1993:218), anadai kuwepo kwa hadithi mojawapo kuhusu kijiji cha hapo awali ya Wagiriama kwa jina *Kaya Murikwa* iliyokuwa na nyumba za sampuli hiyo ambayo ilishambuliwa na Wagalla kikatili, kisha ikabadilishwa jina kuitwa *Kaya Mwijo* (Kaya ya dhahabu). Wagalla waliwashambulia majirani zao kwa sababu nyingi. Kwanza ilikuwa ni fahari yao walipoona mikuki ikipasua ngozi nyororo na kisha kufanya maadui kuwa maiti. Pili, walitaka kutwaa mifugo yao. Werner (1915:335) anaeleza kwamba Wagalla walipowaona Wapokomo wakiwa na ng'ombe wengi, hawakufurahia hadi walipowachukua ng'ombe hao na kuwafanya Wapokomo kuwa watumwa wao.

Ni bayana kuwa misukosuko ya kivita iliyoshuhudiwa na Waswahili pamoja na jamii zingine kutoka pwani ilihitaji mtu wa kutoa uongozi au wa kujitambulisha naye na hata kuwakinga kutokana na mashambulizi ya maadui zao. Aidha, palihitajika mtu wa kuwaunganisha Wapokomo, Wasegeju na jamii nyingine za pwani kama familia moja ndiposa bali na Waswahili kujitambulisha na Fumo Liyongo, hata Wapokomo, Wasegeju na jamii zingine za pwani wanamtambua Fumo Liyongo kama shujaa wao hata katika tamaduni zao.

## 2.4 Historia ya Wayahudi hadi Kuzaliwa kwa Nabii Isa

Asili ya watu wa Israeli ambao wanaitwa Wayahudi pia ni Abraham, mwanawe Yitshak, na mjukuu wake Ya`aquub (Israili). Wote hawa waliishi nchi ya Kanaani, ambayo ilikuja kujulikana kama Israili.Jina Israil linalotokana na nabii wa Mwenyezi Mungu Ya`aquub. Mwenyezi Mungu aliwatumia wana wa Israeli mitume wengi sana, mmoja baada ya mwingine. Kati yao, nabii aliyejulikana zaidi kuliko wote alikuwa ni nabii Musa, ambaye aliteremshiwa kitabu cha *Taurati* ambacho kilikuwa na hukumu za dini yao na desturi zao kama vile umma wa Muhammad uliteremshiwa *Qurani* tukufu.

Baada ya nabii Musa, walifuatia mitume wengine wakihukumu kufuatia kile Kitabu cha *Taurati*.Baada ya Musa, akatumwa nabii Daudi na kuteremshiwa kitabu cha *Zaburi*. Wana wa Israil walikuwa wakaidi Mungu na mitume wake, wenye khiyana na vilevile walikuwa wadanganyifu. Hivyo, waliwakadhibisha baadhi ya mitume wao na baadhi yao wakawauwa bila haki.

Baada ya Nabii Musa kuwaokoa wana wa Israil kutoka kwa Firauni ambaye aliwaadhibu kwa adhabu za kila nui, walipokuwa njiani wakienda nchi ya ahadi (Falastina), walikutana na watu wakiabudu masanamu, na wakamwomba Musa awatengenezee masanamu kama hayo ili nao wapate kuyaabudu badala ya kumwabudu Mungu wao aliyewaokoa. Baadaye, walimwomba mtume wao awaonyeshe wamuone Mwenyezi Mungu wazi wazi ili wapate kumwamini mtume wao Musa. Ombi hilo liliwasababishia mola kuwaadhibu kwa kuwauwa na umeme wa radi na wengi wakafa. Lakini baadaye aliwahuisha wote ili wapate kumshukuru.

Allah alipotaka kuwafungulia nchi takatifu (L-Qudsi) kwa mikono yao kutoka kwa majabari, walikataa wakati kupambana nao kama walivyoamrishwa na badala yake wakamwambia Musa aende na mola wake akapigane na wao wangojee pale.Mungu alitaka kuwaangamiza lakini nabii Musa alimwomba awasamehe. Hivyo, Mungu akawaadhibu kwa kuwaharamishia wasiingie nchi takatifu kwa miaka arubaini.

Baada ya kukamilisha hiyo miaka arubaini, Mungu akataka waingie ile nchi takatifu chini ya uongozi wa mtume Youshua baada ya nabii Musa kufa huku wakiwa wamenyenyekea na kwa kuomba msamaha. Lakini walivunja amri ile na wakaingia kwa kiburi na ukaidi. Mwenyezi Mungu alighadhabika na akawaangamiza kwa kuwatumia ugonjwa wa tauni uliowauwa watu sabini elfu kwa saa moja kwa sababu ya ukaidi wao.

Wakati wa zama za Mtume Hezaqiil walipoamrishwa kupigana vita, walitoka idadi kubwa majumbani mwao wakakimbilia jangwani kwa kuogopa mauti. Mungu aliwaua lakini baadaye kwa fadhila zake juu yao, aliwahuisha baada ya mtume wake kuwaombea na wakapata kujua kwamba kufa si lazima kutokane na kupigana vita tu.

Kisha baadaye, Mwenyezi Mungu aliwatumia Nabii Ilyaas. Nabii huyu aliwaita katika ibada ya Mungu mmoja na kuwahimiza waache ile ibada ya masanamu. Waliukataa mwito wake na wakataka kumuuwa. Alipokata tamaa kwamba hawatamwamini, akamwomba mola wake na Mungu akawaadhibu kwa njaa kwa kuifunga mvua kwa miaka mitatu.

Mungu baadaye, aliwatumia nabii Al-Yasa`a aliyewaita katika ibada ya Mungu mmoja kwa sheria aliyokuja nayo Ilyaas na wakamwamini na kumtukuza.

Baada ya L-Yasa`a akaja nabii Dhil-Kifl. Wakaendelea na hali ile ile kama walivyokuwa kwa nabii L-Yasa`a. Lakini baadaye wakavunja ahadi zao na kumfanyia makosa. Wakati ule, walikuwa na *Tabuut* (Sanduku la Taurati) walilokuwa wakirithiana tokea wakati wa nabii Musa. Walipozidisha uasi wao, Mwenyezi Mungu akawapa nguvu L-`Amaalika wakawanyang`anya sanduku hilo mpaka wakati alipotumwa nabii Shamueli. Baada ya hapo Mwenyezi Mungu aliwatumia nabii Daud na nabii Suleiman na manabii wengi wengineo kama Nabii Uzeir na Nabii Zakaria na Yahya waliowaua, na mwishowe Nabii Issa waliyemuudhi na kutaka kumuuwa, lakini Mwenyezi Mungu alimpaza mbingu

**2.5 Misukosuko ya Kivita Iliyowakumba Wayahudi**

Abdilatif abdalla katika utangulizi wa *Utenzi wa nabii Isa* anakariri kuwa utenzi huu unahusu kuzaliwa kwake nabii Isa, kupawa kwake utume, misukosuko kadha wa kadha aliyoipata katika kuwalingania watu wake – Mayahudi, ili wamuandame na kuiandama njia ya uongofu, kuhitilafiana kwa mayahudi juuu ya kumuamini nabii Isa na kujaribu kwao kutaka kumuua.Wayahudi kama watu na taifa walipitia misukosuko mingi mikononi mwa mataifa mengine kama tutakavyoonyesha hapa chini.

Katika mwaka wa 587 K.K, jeshi la Babiloni walingia mji wa Jerusalem, wakaliharibu hekalu na kuwateka nyara Wayahudi na kuwahamishia nchi ya Babiloni. Mwaka wa ndio ulileta mabadiliko katika historia ya eneo hili. Kuanzia mwaka huu na kuendelea katika miaka iliyofuata, nchi hii ilitawaliwa na mataifa yenye uwezo zaidi, moja baada ya lingine kuanzia

Babiloni, Shamu, Ugiriki, himaya za Roma na Byzantini, Ufalme wa Ottoman na Uingereza. Katika mwaka wa 587 K.K, Wayahudi walitawaliwa na Babiloni, na chini ya utawala huu, hekalu la kwanza liliharibiwa. Kati ya mwaka wa 538–333 K.K, chini ya utawala wa Shamu, hekalu la pili lilijengwa baada ya Wayahudi waliotekwa nchini Babiloni walirejea makwao. Nchi hii ilitwaliwa na majeshi ya Ugiriki chini ya Alexander katika mwaka wa 333 K.K. Kati ya mwaka wa 333 na 63K.K, hekalu la pili.

Jeshi la Warumi likiongozwa na Tito lilivamia Jerusalem na kuliharibu hekalu la pili. Wayahudi walishikwa mateka na kuhamishwa ughaibuni. Katika mwaka wa 132, Bar Kokhba alipanga vita vya kuususia utawala wa Warumi, lakini aliuawa katika vita vya Bethar katika milima ya Judea. Kutokana na haya, Warumi waliamua kuumaliza utambulisho wa Wayahudi kabisa katika nchi yao. Walifanya hivi kwa kubadili jina la jiji la Jerusalem na kuliita Aelia Capitolina na Judea kuitwa Palestina (jina hili lina asili ya Kirumi). Wayahudi waliosalia walihamia katika miji ya Kaskazini ya Galilee. Baada ya utekaji wa Warumi, Wayahudi walihamia Uropa na Afrika Kaskazini. Wakiwa ughaibuni waliendelea na dini na tamaduni zao.

Masaibu haya waliyoyapitia Wayahudi wakiwa kwao nchini na ugenini kuliwafanya wamtamani shujaa aliyetabiriwa na Nabii Isaya katika *Agano la kale*. Walimtarajia Masihi ambaye walimwamini angekuwa shujaa wa kivita, ambaye angewapigania kutoka kwa maadui wao, na kuuanzisha ufalme ambao haungekuwa na kikomo.

**2.6 Historia Ya Nabii Isa**

*Utenzi wa Nabii Isa* ni kisa kinachohusu maisha ya Mariyamu Binti Imrani ambaye baada ya kuzaliwa katika familia ya Imrani na mamake waliabudu msikitini kila mara, alichukuliwa na mtume Zakaria aliyeishi naye kwa mafunzo mengi ya kidini na hata kumlea kwa ibada kila mara msikitini. Kabla ya Mariyamu kukutana na mtume wa Mungu aliyemtabiria kuhusu kuzaliwa kwa Nabii Isa na kumvivia nguo na baadaye akapata mimba ya mwana ambaye ndiye Nabii Isa bila kuonana na mume yeyote kimwili.

Utenzi huu ni utenzi uliojikita katika mafundisho ya dini ya Kiislamu kuhusu maisha ya mtume Isa. Hivyo, Nabii Isa katika utenzi huu amechorwa kwa njia sawa na alivyosawiriwa katika *Qurani tukufu*. Ingawa Waislamu sawa na Wakristo wanakiri pia vitabu vitakatifu vya *Torati*, *Zaburi* na *Injili,* katika ibada wanatumia *Qurani* tu na kwa kawaida ndiyo chanzo chao cha habari juu ya watu na matukio ya kabla yake. Mengi ya matukio haya yanaoana na jinsi yalivyoangaziwa katika *Bibilia*. Kwa mintarafu hii, tutaangazia historia ya Nabii Isa kama alivyosawiriwa katika *Utenzi wa Nabii Isa*, na vilevile kwa kurejelea *Qurani tukufu* pamoja na *Bibilia* ili kushadidia historia hii.

*Qurani* iliandikwa miaka 600 hivi baada ya Kristo na ina aya 93 zinazomhusu Nabii Isa, lakini haileti mfululizo wa habari za maisha yake wala za mafundisho yake maalumu. Nabii Isa kwa Waislamu ni mtume anayeaminiwa kuwa mmojawapo wa mfululizo wa mitume na manabii watukufu 124,000 wa Mwenyezi Mungu walioletwa ulimwenguni kuwapasha wanadamu ujumbe wa upweke na umoja wake, ili wamuabudu akiwa ndiye Muumba na mruzuku wao hapa duniani. Mitume na manabii hawa wameletwa katika zama mbalimbali na kwa watu, kaumu na umma

mbalimbali, na mfululizo huu ulianza na Adamu, baba wa wanadamu wote, hadi Mtume Muhammad akiwa ndiye wa mwisho.

Nabii Isa(anayefahamika kama Yesu Kristo na Wakristo) ni miongoni mwa mitume wakubwa kama Nabii Nuhu, Ibrahimu, Musa na Muhammad, ambao Mwenyezi Mungu amewasifu kwa subira yao na ustahimilivu wao mkubwa: Tena ni miongoni mwa Mitume waliopewa Kitabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu kiitwacho *Injili*.

Kuzaliwa kwa Nabii Isa, kama ilivyo kwa majagina wengi, kulikuwa kwa kulikuwa kwa kimiujiza. Nabii Isa alizaliwa na bibi Maryam bila ya baba, kwa amri ya Mola wake ambaye alimtuma malaika Jibrili, kumtangazia kumpata mtoto mtukufu. Kama tutakavyoona hapa baadaye, kuzaliwa kwa majagina wengi huwa kumetabiriwa. *Qurani* pamoja na *Bibilia* zinatoa maelezo kuhusu utabiri uliofanywa na nabii Isaya kuhusu kuzaliwa kwa Nabii Isa. Utabiri huu unatimia miaka mia nne baadaye. Kwa mujibu wa *Bibilia*, utabiri wa nabii Isaya ulitimia katika kitabu cha *Mathayo* 2:1, ambapo inaeleza kuwa shujaa alizaliwa huko Bethlehemu ya Uyahudi, zamani za Mfalme Herode.

Kama ilivyo desturi ya mashujaa wengi wa kidini, baada tu ya kuzaliwa, alikutana na kikwazo cha kutaka kuuawa na Mfalme Herode ambaye alihofia kunyang’anywa madaraka, shujaa huyu atakapokuwa mkubwa (*Mathayo* 2:13). Malaika wa Bwana alimtokea Yusufu (Babake Isa) katika ndoto na kumweleza amchukue mtoto Yesu na mama yake (Mariam), kisha wakimbilie Misri. Ndivyo ilivyo hata kwa mashujaa wengine misukosuko inapozidi, kugura au kukimbilia

uhamishoni. Baada ya Mfalme Herode kufa, shujaa Yesu alirudishwa na wazazi wake Galilaya katika mji wa Nazareti.

Baada ya kuzaliwa, Nabii Isa, kama walivyo baadhi ya majagina, alisema utotoni mwake akiwa bado mchanga, huu ukiwa ni muujiza mwingine kwa watu ili kuwaonyesha kuwa yeye si mtoto wa kawaida, na kuwa mamake hana dhambi ya kuja kwake bila ya baba. Huu ni mfano mmoja katika mifano minne ya uumbaji aliyoonyesha Mwenyezi Mungu, kwani Mwenyezi Mungu alimuumba Adamu bila ya baba wala mama, akamuumba Hawa bila ya mama, akamuumba Isa bila ya baba, na akawaumba wanadamu wote waliobakia kutokana na baba na mama. Habari za kuzaliwa kwake Nabii Isa zinapatikana katika *Qurani*, Surat "Maryamu" (19) kuanzia aya 16 - 35.

> *Na mtaje Maryamu katika Kitabu, pale alipojitenga na jamaa zake mahali upande wa mashariki.Na akaweka pazia kujikinga nao. Tukampelekea Roho wetu, akajifananisha kwake sawa na mtu.*
>
> *(Maryamu) akasema: Hakika mimi najikinga kwa Mwingi wa Rehema aniepushe nawe, ukiwa ni mcha Mungu.*
>
> *(Malaika) Akasema: Hakika mimi ni mwenye kutumwa na Mola wako ili nikubashirie tunu ya mwana aliyetakasika. Akasema: Nitampataje mwana hali mwanamume yeyote hajanigusa, wala mimi si kahaba?*
>
> *(Malaika) akasema: Ni kama hivyo! Mola wako mlezi amesema: Haya ni mepesi kwangu! Na ili tumfanye kuwa ni Ishara kwa watu, na Rehema itokayo kwetu, na hilo ni jambo lililokwishaamuliwa. Basi akachukua mimba yake, na akaondoka nayo mpaka mahali pa*

*mbali. Kisha uchungu ukampeleka kwenye shina la mtende; akasema: Laiti ningelikufa kabla ya haya, na nikawa niliye sahaulika kabisa! Pakatangazwa kutoka chini yake: Usihuzunike! Hakika Mola wako amejaalia chini yako kijito kidogo cha maji! Na litikise kwako hilo shina la mtende, utakuangushia tende nzuri zilizo mbivu. Basi kula, na kunywa, na litue jicho lako. Na pindi ukimwona mtu yeyote basi sema: Hakika mimi nimeweka nadhiri kwa Mwenyezi Mungu ya kufunga; kwa hivyo leo sitasema na mtu. Akenda naye (mwanawe) kwa jamaa zake amembeba. Wakasema: Ewe Maryamu! Hakika umeleta kitu cha ajabu! Ewe dada yake Harun! Baba yako hakuwa mtu muovu, wala mama yako hakuwa kahaba.Akawaashiria (mtoto).Wakasema: Vipi tumsemeze aliye bado mdogo yumo katika mlezi?*

*(Mtoto) akasema: Hakika mimi ni mtumwa wa Mwenyezi Mungu. Amenipa Kitabu, na amenifanya Nabii. Na amenijaalia ni mwenye kubarikiwa popote pale niwapo. Na ameniusia Sala Na Zaka maadamu ni hai, Na nimtendee wema mama yangu. Wala hakunifanya niwe jeuri, mwovu.Na amani iko juu yangu siku niliyo zaliwa, na siku nitakayo kufa, na siku nitakayo fufuliwa kuwa hai. Huyo ndiye Isa mwana wa Maryamu. Ndiyo kauli ya haki ambayo wanaifanyia shaka.Haiwi kwa Mwenyezi Mungu kuwa Na mwana, Subhanahu, Yeye ametakasika! Anapolihukumia jambo basi huliambia tu: Kuwa! Likawa*.

Nabii Isa aliletwa kwa wanadamu kufikisha ujumbe kwao wa kuwafahamisha kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja, hana mwenzake, na kuwa yeye pekee ndiye mwenye kustahili kuabudiwa kwa haki, na ujumbe huu ndio ujumbe uleule uliotumwa kwa Mitume na manabii wote kwa wanadamu ili kuwaongoza, naye alikuja kutilia mkazo na kusisitiza jambo hili na kuzipa nguvu

tume za mitume na manabii waliopita. Kadiri ya sura ya 3 aya ya 50 alisema ni *"msadikishaji wa yale yaliyokuwa kabla yangu katika Taurati, na ili niwahalalishieni baadhi ya yale mliyoharimishiwa, na nimewajieni na Ishara kutoka kwa Mola wenu, kwa hiyo mcheni Mwenyezi Mungu na mnitii"*.

Alitabiri kuwa baada yake atakuja mmoja ambaye atawafundisha wanadamu ukweli wote na kuwaongoza kwenye haki na kuwaeleza kila wanalolihitaji katika maisha yao. Ujumbe wake ulikuwa ni wa mwisho kabla ya ule wa mtume Muhammad ambao ndio wa mwisho kabisa kwa wanadamu wote.Mwenyezi Mungu ameleta mitume na manabii wengi ulimwenguni, lakini alichagua baadhi yao na kuwateremshia vitabu vya uongozi na sharia na hekima kwa wafuasi wao. Katika vitabu vilivyoteremshwa kwa Manabii mbalimbali ni *Taurati* kwa Nabii Musa, *Zaburi* kwa Nabii Daudi, *Injili* kwa Nabii Isa, na *Qurani* kwa Nabii Muhammad. Kitabu cha Nabii Isa kiliteremshiwa Wayahudi ambao ndio walengwa wake wa kwanza wa Nabii Isa, kama ilivyothibitishwa na Qurani wakati aliposema:

> *Enyi Wana wa Israili! Hakika Mimi Ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, ninayethibitisha yaliyokuwa kabla yangu katika Taurati, na mwenye kubashiria Mtume atakayekuja baada yangu jina lake ni Ahmad! Lakini alipowaletea hoja zilizo wazi, walisema: Huu ni uchawi ulio wazi!*

Majagina kwa kawaida hufanya miujiza au mambo ya ajabuajabu. Nabii Isa alipewa na Mwenyezi Mungu miujiza mbalimbali kumsaidia katika kazi yake ya kutangaza dini ya Mwenyezi Mungu, kwani ilikuwa ni kawaida kwa Mtume au Nabii kuonyesha miujiza kwa watu

au kaumu yake ili awathibitishie kuwa yeye kweli ni mjumbe aliyeletwa na Mola wa ulimwengu huu. Mitume waliomtangulia Nabii Isa, kama Nuhu na Ibrahim na Musa na wengine walikuja na miujiza mbalimbali. Baadhi ya miujiza ya Nabii Isa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu ni kuumba ndege kutokana na udongo, kuponyesha vipofu wakaweza kuona, na kuwaondoshea ukoma wale wenye ukoma, na kuhuisha mtu aliyekufa, na kuwateremshia wafuasi wake chakula kutoka mbinguni ili iwe ni dalili kwao wote. Ingawa Isa alichukua muda mwingi msikitini katika ibada (beti 289, 299), wengi bado hawakuacha kutenda maovu na kila asubuhi hao walitafuta njia ya kuhalalisha ibada haramu ya kuabudu masanamu (ubeti 310). Licha ya kufanya miujiza, wana wa Israeli walihitilafiana iwapo yeye ni nabii au la. Hili jambo lilileta upinzani mkali miongoni mwao na wengi walizua njama ya kumuua.

Moja kati ya sifa bia za majagina ni kwamba wanakumbana na usaliti kutoka kwa aila au watu walio karibu sana na wao. Shujaa Isa alifanya huduma kwa muda wa miaka mitatu kisha akafa. Wakati wa huduma ya kuwakomboa watu na dhambi zao, wapo Wayahudi waliomkubali na kumfuata na wengine walimchukia na kumshutumu kuwa alikufuru kwa kujiita mwana wa Mungu.Wale waliomchukia ndio waliofanya njama za kumuua. Hatimaye walimtumia mmoja wa wanafunzi wake aliyeitwa Yuda kwa kumpa vipande thelathini vya fedha ili amsaliti kisha wamkamate. Yuda aliwaambia, nitakayembusu ndiye, na hapo ndipo Wayahudi walipomkamata shujaa huyu na kumsulubisha hadi kifo chake (Marko 14:10-72 na 15:1-37). Baada ya siku tatu, alifufuka na kupaa juu mbinguni ambapo wakristo wanaamini kuwa anakaa katika upande wa kulia wa Mungu baba na kwamba atarudi hapa duniani kuwahukumu walio hai na waliokufa. Qurani inatoa maelezo tofauti kuhusu kifo cha Isa kwani inasema kuwa Isa alichukuliwa na mola

wake na kupandishwa kwake mbinguni baada ya Wayahudi kutaka kumuua, na kwa hivyo hawakuweza kumuua wala kumsulubu.

Waislamu pamoja na Wakristo wanaamini kuwa Isa atarudi tena ulimwenguni kukamilisha kazi yake aliyoiacha baada ya kupaa kwenda kwa Mola wake, na haya yanaelezwa katika vitabu vya dini vya Kiislamu na vya Kikristo.Muhimu hapa ni kujua kuwa sawa na umma wa majagina, waumini wa Isa katika dini zote mbili wanaamini kuwa atarudi tena duniani kukamilisha kazi aliyopewa na Mwenyezi Mungu.

**2.7 Hitimisho**

Katika sura hii, tumeangazia historia, vipindi walivyoishi na mazingira yaliyowazaa mashujaa Fumo Liyongo na Nabii Isa.Kama tulivyotangulia kusema shujaa huzuka ili kutatua tatizo fulani linaloisibu jamii au umma wake. Katika sura hii tumeonyesha ni kwa nini majagina hawa walizuka wakati walipozuka na matarajio ya umma wao. Katika sura inayofuata, tutalinganisha kufanana na kutofanana kwa majagina hawa wawili kwa mujibu wa sifa bia za majagina.

# SURA YA TATU

# KULINGANISHA NA KUTOFAUTISHA SIFA ZA KIJAGINA ZA NABII ISA NA FUMO LIYONGO

## 3.0 Utangulizi

Gichamba (2005:67) akiwanukuu Chiraghdin, Nabhany na Baruwa (1975:63), anasema kuwa tenzi ambazo huandikwa kuhusiana na mashujaa au tukio lingine lolote la kijamii, hufumbata na kusawiri kwa kina masuala muhimu ya kihistoria. Wanaendelea kusema kuwa, maudhui ya tenzi katika fasihi mbalimbali za ulimwengu ni kutukuza utaifa katika historia za jamii, na pia kuwatukuza watu waliotenda vitendo vikubwa (mashujaa) katika historia zao. Ni kwa mintarafu hii ambapo katika sura hii, tutaangazia sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na Nabii Isa. Tutaonyesha kushabahiana kwa sifa za kijagina za mashujaa hawa wawili, pamoja na kutofautiana kwao. Ili kupata sifa jumlishi za kishujaa za Fumo Liyongo, tumerejelea *Utenzi wa Fumo Liyongo* pamoja na tungo zingine zilizotungwa na waandishi wengine kumhusu. Aidha, tumerejelea tungo muhimu ambazo zinadaiwa kutungwa na Liyongo mwenyewe.

Katika kuainisha sifa za kishujaa za Nabii Isa, tumeangazia sifa zinazojitokeza katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Huu ni utenzi ambao msingi wake ni katika *Qurani*. Hivyo, shujaa Isa katika utenzi huu amesawiriwa kwa njia sawa na alivyoangaziwa katika *Qurani tukufu*. Hata hivyo, tumerejelea *Qurani*, na inapobidi, *Bibilia*, ili kuchangia sifa za kijagina za shujaa huyu ambazo hazijajitokeza kikamilifu katika utenzi huu. Aidha, tumetalii mitandao tofauti ili kuchangia historia, maisha na matendo ya kimiujiza ya shujaa Isa.

### 3.1 Kuzuka kwa Mashujaa

Jamii ni mfumo ambao huwa na mahitaji mengi. Mahitaji haya huzua taasisi mbalimbali, mojawapo ikiwa ni taasisi ya mashujaa. Taasisi hii ni muhimu katika kusawazisha hali zilizoenda kombo katika jamii. Shujaa wa kihistoria wa jamii huwa hazuki katika ombwe tupu, bali huzuka katika kipindi, mazingira na wakati maalumu katika jamii yake na huishi hadi pale ambapo atatekeleza dhamira yake. Ni kutokana na sababu hii ambapo wanajamii wanamtazama shujaa kama zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Wengi wa mashujaa, kama vile wa kidini na hata wa kihistoria, huzuka katika mazingira ambamo mna vita. Lwanda Magere alizuka kutokana na mashambulizi ya mara kwa mara ya Wanandi, Dedan Kimathi, kwa mfano, pia alizuka katika mazingira ya kivita, na vivyo hivyo Fumo Liyongo aliyezuka kwa sababu ya misukosuko ya kivita kati ya Waswahili wenyewe, na hata kati yao na majirani zao. Nabii Isa anazuka kama shujaa kwa Wayahudi ambao baada ya kutawaliwa na kulipishwa kodi na mataifa mengine na hata kutumika kama watumwa, walitarajia kutimizwa kwa ubashiri wa Nabii Isaya kuhusu kuzaliwa kwa mfalme wa wafalme ambaye angewakomboa kutoka kwa maadui zao. Wayahudi walitarajia kiongozi wa kijeshi.

#### 3.1.1 Utabiri wa Kuzaliwa kwa Majagina

Mutiso (1999:4), anasema kuwa kuzaliwa kwa jagina huwa kumebashiriwa na kusipobashiriwa, huthibitishwa baada ya jagina kuzaliwa. Hali hii ya ubashiri inadhihirika sana katika kuzaliwa kwa mashujaa wa kidini ambapo kabla hawajazaliwa, kunatokea mbashiri ambaye anawatia moyo wanajamii wazidi kuwa na ustahimilifu, huku akiwaambia kuwa jagina atazaliwa. Jagina huyu ataasisi ufalme ambao utakuwa mkubwa mno ukilinganishwa na falme zingine na kisha atawakomboa kutoka kwa dhiki zao.

Kuzaliwa kwa Nabii Isa kulibashiriwa katika *Agano la Kale* na kunathibitishwa na Yahya Mtakatifu. Unabii huu umedokezwa katika *Isaya* vii:14, xi:3 *Yeremiah* xxiii:5,*Micah* v:2. Tangu utabiri wa Isaya hadi kuzaliwa kwa Isa, inakadiriwa kuwa ni miaka 400. Utabiri wa nabii Isaya ulitimia katika kitabu cha *Mathayo* 2:1 ambapo inaeleza kuwa shujaa alizaliwa Bethlehemu ya Uyahudi, zamani za mfalme Herode.

Mutiso (khj) anasema kuwa hata kuzaliwa kwa mashujaa wengine wa kidini huwa kumetabiriwa. Kuzaliwa kwa Gautama Buddha kwa mfano, kulitabiriwa na watabiri sitini na wanne walioifasiri ndoto ya mamake hata kabla ya kuzaliwa kwake. Kuzaliwa kwa Samsoni aliyewakomboa Waisraeli kutoka kwa Wafilisti (taz kitabu cha *Waamuzi* 13:3 kwenye *Biblia*), kulitabiriwa na malaika.

Shujaa anapozaliwa kunakuwa na ishara inayoonyesha kuwa mtoto aliyezaliwa ni mtoto wa kipekee. Sifa hii inajitokeza vyema zaidi katika *Biblia*. Baada ya Yesu kuzaliwa, malaika wa Mungu aliwatokea wachungaji waliokuwa wakichunga makundi yao karibu na Bethlehemu. Malaika huyo alitangaza:

> *"Leo katika jiji la Daudi, Mwokozi ambaye ni Kristo Bwana amezaliwa kwenu."* (*Luka* 2:8-11) Kisha, *"..umati wa jeshi la mbingu ukawa pamoja na yule malaika, ukimsifu Mungu na kusema: 'Utukufu katika vilele vilivyo juu kwa Mungu, na juu ya dunia amani kati ya watu wa nia njema.' Luka* 2:13, 14.

Vilevile, Isa alipozaliwa, makuhani walienda kumwabudu wakielekezwa na nyota iliyong'aa kutoka Magharibi na kutua mahali alikozaliwa (*Mathayo* 2:1–3). Ishara hizi zinaoana na sifa kuwa majagina wanapozaliwa kunakuwa na ishara kuonyesha kuwa hawa ni watoto wa kipekee.

Katika utafiti wetu, hatukupata ushahidi wowote kuonyesha kuwa kuzaliwa kwa Fumo Liyongo kulikuwa kumetabiriwa. Utenzi huu pia haujazungumzia matukio yaliyozunguka kuzaliwa kwa Fumo Liyongo au ishara zozote zilizoonyesha kuwa Liyongo angekuja kuwa mtu wa pekee katika maisha ya baadaye.

### 3.1.2 Jagina kwa Kawaida ni Mwanamume

Aghalabu kote duniani majagina huwa ni wa kiume. Pale ambapo ni mwanamke, basi hana sifa bia za kishujaa kama walizo nazo wanaume ambao hurejelewa kama mashujaa (sifa za toka utabiri wa kuzaliwa kwao hadi kifo chao). Pengine mwanamke shujaa utapata kuwa alitenda tendo moja tu la kijisajiri. Hata hivyo, ujasiri ni sifa moja tu ya kishujaa wala haiwezi kumfanya mtu kuwa shujaa.

Shujaa Fumo Liyongo na Nabii Isa walikuwa mwanamume.Mashujaa wa kidini pia huwa ni wanaume. Kwa mfano Musa, Samsoni, Buddha, Mtume Muhammadi na wengine wengi. Aidha, waumini wa dini mbalibali duniani humchukulia Mungu (ambaye ni shujaa wa mashujaa) kuwa ni mwanamume.

Hali hii ya kumchukulia jagina kuwa mwanaume inatokana na akililaza kuwa mwanamume kwa wakati wowote yu juu ya mwanamke na kwa hivyo, uongozi pamoja na ukombozi ni lazima

utokane na mwanamume. Kadhalika, wanawake kote duniani husawiriwa kama watu waoga na wadhaifu, tofauti na mwanamume ambaye mara nyingi huwa mstahimilifu na hukabiliana na mambo na masaula magumu katika jamii.kama vile, vita na mambo mengine magumu. Ndiposa kukatokea msemo wa “jikaze kiume”.

### 3.1.3 Utoto na Ujana wa Jagina

Aghalabu utoto na ujana wa jagina huwa hauelezwi. Kama utaelezwa, utapata kuwa ni kwa kijuujuu tu na wakati mwingine utapata wanahistoria huchanganya utoto wa kuzaliwa kwa shujaa na ujana wake na kufanywa kuwa kitu kimoja. Hii ni kwa sababu shujaa anapozaliwa, hukua kama mtu kawaida tu. Lakini baadaye ndipo watu hugutuka kutokana na matendo, tabia na uwezo wake usio wa kawaida na ndipo watu huanza kumtukuza.

Kazi zinazohusishwa na Fumo Liyongo, kwa mifano hazielezi kuhusu utoto wake wala ujana wake. Mathalani, hutuelezwi mazingira ya nyumbani kwao, uhusiano wake na vijana wengine akiwa mtoto, maeneo aliyoyatembelea akiwa kijana, hulka na matamanio yake. Tunatajiwa katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* kuwa Liyongo alibaleghe na kuwa mwanamume mwenye haiba, kimo kirefu, mpana na maarufu hivi kwamba watu walienda kumwangalia. Katika *Utenzi wa Nabii Isa* hakuna mengi yanayosemwa kuhusu ujana na utoto wa Nabii Isa, ila tu kwamba alilelewa katika ibada na kwamba alisema akiwa mdogo sana.*Utenzi wa Nabii Isa* unatufafanulia kuwa mamake Maryam binti Imrani alipohisi njaa akiwa shinani mwa mtende punde tu baada ya kumzaa, mwanawe nalimuuliza autikise mtende ambao haukuwa na tende lakini Mungu alimruzukia akavuna tende tamu, maalum tena mbivu na vivyo kumwepusha na njaa.

Nabii Isa alifahamu toka utotoni mwake kuwa alikuwa na nafasi muhimu kama masihi na hivyo hakushiriki michezo kama watoto wengineyo:

288 Kwa wadogo si katiti,
Alikuwa tafauti,
Hakupoteza wakati,
Machezo kuhudhuria.

289 Mchezo wake dhabiti,
Alo akijisharuti,
Ni yeye ni msikiti,
Ibada kuhudhuria.

**3.1.4 Shujaa Hutokana na Ukoo wa Kifalme au nasaba bora.**

Mara nyingi shujaa hutoka katika ukoo ambao unachukuliwa kuwa ni ukoo ambao umetengwa na kuteuliwa na Mwenyezi Mungu, ili uongoze jamii na kuikomboa kutokana na shida na misukosuko inayowakumba wanajamii husika. Mutiso (1999:4) anaeleza kuwa kuzaliwa kwa jagina huwa kumebashiriwa na kusipobashiriwa huthibitishwa baada ya ya jagina kuzaliwa. Anadai kuwa ithibati kwamba atakayezaliwa au aliyezaliwa atatokana na ukoo au mlango wa kureshi, Sakya, Gandhi, Amaterasu. Omikami, Daudi, n.k. Kila jamii katika ulimwengu mzima huhusudu asili ya jagina ake na hutilia maanani umuhimu wa mambo ya kadimu. Kwa kuitaja shajara yake, mwanadamu hujihisi kama amezaliwa upya tena.

Baada ya kiongozi kufa, jamaa mmoja kutoka katika ukoo wa kiongozi huyo ndiye huurithi utawala. Kwa hivyo, kwa kawaida jagina hutokana ukoo bora au wa kifalme ambapo baba ya jagina aghalabu huwa mfalme au kiongozi wa jamii yake. Uongozi wa utawala huu hauji vivi hivi tu, lakini inabidi kuwe na utetezi wa cheo cha uongozi kama ambavyo tutathibitisha hapa baadaye.

Fumo Liyongo alitokana na ukoo wa Al Bauri (Allen: 1993:121). Ukoo ambao ulichukuliwa kuwa bora na kupewa jukumu la kuiongoza jamii, haswa jamii ya Waswahili wa Pate. Baba yake Liyongo, aliyeitwa Mringwari wa kwanza, alikuwa sultani wa dola ya Pate. Baada ya kifo chake, Daudi Mringwari aliyechukua hatamu za uongozi pia, alitoka katika ukoo wa Al Bauri.

Mashujaa wengine na hasa wa kidini, akiwepo Nabii Isa, mtume Muhammadi na Gautama Buddha, walitokana na ukoo bora. Nabii Isa alitokana na ukoo wa mfalme Daudi. Mashujaa wengine ambao wametokana na koo bora ni kama vile Mtume Muhammadi, aliyetokana na ukoo wa kabila la Kikureshi, na Gautama Buddha, aliyetokana na ukoo bora ulioitwa Sakya, ulioaminika kutokana na mayai yaliyoanguliwa na jua (Mutiso 1999:5).

### 3.1.5 Utetezi wa Cheo

Shujaa mara nyingi huwa hakipati cheo chake kwa njia ya urahisi. Huwa lazima akipiganie na akitetee dhidi ya maadui wake. Aghalabu shujaa akiwa kiongozi ndipo hupata nafasi nzuri ya mabadiliko na kuitumikia jamii yake jinsi atakavyo hadi katika ufanisi wa ukombozi. Shujaa kwa hivyo anaweza kufanya jambo lolote, bora tu litamsadia kuhifadhi kiti chake, anaweza hata kuua.

Utetezi wa cheo cha ufalme wa Fumo Liyongo unadhihirika vizuri sana katika *Takhmisa ya Liyongo* ambapo suala hili limeangaziwa kwa kina katika beti mbalimbali. Gichamba (2005:75), anatoa maelezo ya utetezi wa cheo kwa kurejelea jinsi Shaka Zulu alivyopigana ili kuona kuwa ameurithi uongozi wa Wazulu baada ya kifo cha babake. Anasema kuwa babake alipofariki, Sigujana (ndugu wa kambo wa Shaka) ndiye alichukua hatamu za uongozi. Hata hivyo, Shaka alijiona kama mrithi halali na kwa kibali cha Dingiswayo, alikichukua kikosi cha *Izichwe* na kuelekea hadi nyumbani kwao na kumwondoa Sigujana kutoka uongozini. Baada ya kushika hatamu za uongozi, wasaliti wake waliadhibiwa kwa mujibu wa sheria kali alizoweka.

Mberia (1989:25), anasema kuwa Liyongo wa takhimisa anadhihirika kama jabari na jasiri ambaye hakunywea mbele ya maadui zake hata walipokuwa wengi na wenye silaha kali. Daima alikuwa tayari kukabiliana nao kwa moyo wa ushupavu. Kwani woga ulikuwa kitu cha kuepukana nacho na waoga watu wa kuepukana nao. Msimamo wake ulikuwa kwamba Mungu pekee ndiye aliye na uwezo wa kuangamiza binadamu na wala sio binadamu wengine. Hivyo basi anashauri:

Wazi ata kicho na wachao sandaye nao
Nao fawithi umuri kwa Mungu anusurao
Siche ya ziumbe na zituko wakutishao
Kufa kwa Mungu na shabuka limkutao
Si kwa walimwengu mivi kikwi ingakufuma

Liyongo hakupigana kwa ajili ya kupenda kupigana au kwa kutaka kusifiwa. Sifa za namna hiyo aliziona ni mbaya. Alipigana kulipokuwa na sababu nzuri ya kufanya hivyo. Inaonekana kwamba miongoni mwa sababu hizi ni utetezi wa cheo. Pia, inaelekea kuwa, kwake, kutokuwa na cheo alichokuwa alichokuwa akipigania kulikuwa sawa na kuteremshwa katika ngazi ya hadhi. Alikiona cheo hicho kuwa ni stahiki yake. Tunaambiwa:

Ana ndimi simba mfiliye jaba na cheo
Naipiga kati kawanesa wajibagao
Siche aduizo kukutana kwa ungi wao
Sichi kikwi chao nami ume ndio nilio moyo
Wangu kikwi kwa ajili ya kushagama.

Hata hivyo, haijitokezi wazi iwapo Liyongo alikuwa anawekewa vikwazo ili asikipate cheo hicho au tayari alikuwa nacho akawa anapokonywa.

Japo shujaa Isa alitokana na ukoo bora na wa kifalme wa Daudi, hakutetea cheo chake kwa njia ya vita vya kimwili kama walivyofanya Liyongo na Shaka. Badala yake aliwakabili wapinzani wake kwa kutoa mafundisho, ambayo mengi yaliwasuta watawala pamoja na Wayahudi ambao walimpinga na kumkataa kama mtume huyu wa Illahi.

### 3.1.6 Maadui wa Shujaa

Njogu na Chimera (1999:156), wanasema kuwa hakuna jagina yeyote ulimwenguni ambaye hana adui. Kwa kawaida, mtu huwa na watu wanaompenda na wasiompenda.Hata Mwenyezi Mungu

(shujaa wa mashujaa, pia ana adui wake mkubwa ambaye ni shetani. Katika maisha ya kawaida, lazima ikumbukwe kuwa, ingawa mtu fulani anaweza kuwa mashuhuri na kipenzi cha watu au ambaye ana ufanisi mkubwa, hakosi watu wakumtakia mabaya, wanaomwonea wivu na hata wenye nia ya kumwua. Shujaa aghalabu anaweza kuwa na jamii nzima kama adui wake, mtu mmoja tu au watu wengi.

Kwa kawaida, maadui hawa ni muhimu kwa sababu mtu hawezi kuwa shujaa bila kuwa na waoga.Vilevile, mtu hawezi kuwa mzuri kama hakuna wale wabaya. Huenda shujaa naye asiwepo kama hakutakuwa na maadui wake. Shujaa huwa na jukumu la kuikomboa jamii yake kutokana na mashambulizi au maovu ya maadui. Mara nyingi maadui wa shujaa humwogopa na hufanya njama za kisirisiri ili kumwangamiza, kwa sababu shujaa huwa na sifa za kipekee tofauti na za wapinzani wake.

Fumo Liyongo kwa mfano, alikuwa na maadui wengi kama vile: Wagalla waliowashambulia Waswahili pamoja na jamii zingine za pwani, binamuye (Daudi Mringwari), na hata mwanawe ambaye katika *Uteuzi wa Fumo Liyongo* (Ub. 214), amerejelewa pia kama adui wa Mwenyezi Mungu. Kwa kawaida, maadui za jamii anayowakilisha au kuitawala shujaa huwa maadui wa shujaa huyo.Tunaweza kudai kuwa ushujaa pia huwa na ngazi mbalimbali, kwa mfano, Wagalla walikuwa mashujaa wa mwituni, lakini waliingiwa na hofu na hata kuogopa vibaya pindi walipomtazama Liyongo. Ngazi hizi za ushujaa huanzia kwenye matawi ya chini (shujaa wa kiwango cha chini) na kupanda hadi katika kiwango cha juu kabisa cha ushujaa kinachomilikiwa na Mungu. Shujaa wa chini kwa kawaida humcha shujaa wa kiwango cha juu.

Daudi Mringwari aliyekuwa binamu wa Fumo Liyongo, pia alikuwa ni adui wake mkubwa. Alipanga njama za kumwangamiza Liyongo kwani alimwona kama tishio dhidi ya utawala wake. Alimtumia mwanawe Liyongo kumsaliti baba yake. Kama alivyo Fumo Liyongo na maadui wengi, vivyo hivyo alivyokuwa Nabii Isa ambaye alipangiwa njama ya kuuawa, jambo ambalo Mola alilibadilisha kwa kumleta mtu ambaye alimfananisha na Nabii Isa kisura. Baadaye mtu huyu aliteswa, akauawa, akasulubiwa msalabani na wahalifu wale wakidai kuwa huyu alikuwa ni Nabii Isa mwenyewe. Kwa mujibu wa *Bibilia*, Wayahudi walifanikiwa kumsulubisha na kumuua Isa. Wayahudi, Waandishi na Mafarisayo waliona kama wamemkomoa kwa kuwa walidai kuwa alijikweza kwa kujifanya mwana wa Mungu. Pia watawala walifurahi maana watu wengi walimfuata na kumsikiliza, na hivyo kumuona kama hatari kwa utawala wao.

### 3.1.7 Shujaa huwa Kipenzi cha Wanajamii

Hata ikiwa majagina huwa na maadui zao, pia huwa kipenzi cha jamii (umma) na ladha maadui zake huwa na wivu kuona jinsi wanajamii wanavyomchukulia kama mkombozi wao na hivyo kumwenzi na vilevile kutarajia mambo makubwa zaidi kutoka kwake, hasa kuleta mabadiliko yana yotarajiwa kuwapeleka hadi katika ufanisi wa hali ya juu. Si ajabu kuwa wanajamii wengi huhusisha mambo yote mazuri katika jamii na shujaa wao, kwa hivyo, umaarufu wa jagina huenea kila mahali.

Fumo Liyongo, alikuwa maarufu sana miongoni mwa jamii Waswahili na hata miongoni mwa watu wengine kutoka jamii zingine. Tunaelezewa haya katika ubeti wa saba wa *Uteuzi wa Fumo Liyongo*.

7 Kimo kawa mtukufu
Mpaka sana mrefu
Majimboni yu maarufu
Watu huya kumwangaliya.

Fumo Liyongo alipokamatwa na kutiwa gerezani, Sultani aliomba ushauri kutoka kwa wanajamii kuhusu kuuawa kwake.Wanajamii walijaribu kumtetea kwa kila njia, walisema kuwa badala ya yeye kuuawa, aachiliwe huru na afanywe amiri jeshi. Walimwona kama mtetezi wao dhidi ya maadui zao (beti za 88 na 89 katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*.Habari za kifo chake zilipowafikia Waswahili, walihuzunika sana. Mshairi wa *Uteuzi wa Fumo Liyongo* ametumia fumbo kwa kusema, *imeanguka pazia* (ub.226) kumaanisha kuwa jamii imeachwa bila mtu wa kuongoza au kuwaunganisha. Maelezo haya yako katika *Uteuzi wa Fumo Liyongo* kama ifuatavyo;

224 Make Liyongo hakika
Matanga aliyaweka
Watu wakasikitika
Kwa Liyongo kuifiya

225 Liyongo silaha yetu
Kwa wut'e khasimu zetu
Alikuwa ngao yetu
Wut'e wakinena haya.

226 Mui walisikitika
Hakuna wa kutosheka
Kwa Liyongo kutoweka
Imeanguka paziya.

Kifo cha Isa kwa mujibu wa Bibilia, kilipoteza matumaini ya watu waliokuwa wakimwamini, ndugu zake pamoja na wanafunzi na wafuasi wake. Watu walilia na kuomboleza pale msalabani kwa kuwa mtetezi wao ametoweka japokuwa waliahidiwa kuwa siku ya tatu atafufuka.

**3.1.8 Jina la Shujaa**

Mara nyingi shujaa hupewa jina linaloakisi hulka, matendo na tabia yake. Huwa ni majina ya kimajazi pamoja na lakabu mbalimbali kwa kutegemea mitazamo ya wanajamii kuhusiana na sifa za jagina wao. Mutiso (1999:16) anasema jagina hupewa jina hili pindi tu anapozaliwa.Yumkini apewe jina la muda na wazazi wake, baada ya kuzaliwa, hadi kufikia pale ambapo ataweza kujitambulisha na kujipa jina mwenyewe au Mungu au kiumbe mwenye uwezo na utambuzi atakapompa jina. Mifano ya majagina wenye majina ya sifa zao ni kama vile, Achillesi (Ujasiri), Orkoiyot (Mwenye nguvu) na Musa (Aliyeokotwa).

Fumo Liyongo pia alipewa jina kulingana na sifa zake. Kwa mfano, jina “Fumo” linarejelea mkuki wenye ncha pana mno ambao hutumika kama vita. Fumo pia linaweza kuwa na maana ya kufuma. Alipokuwa kisimani alipatikana akilenga mshale kama anayetaka kumfuma adui wake huku akipiga magoti. Jina Fumo pia linaweza kuwa na maana ya mfalme, kwa sababu baba yake

alikuwa mfalme na hivyo, akapewa jina hilo. Katika utenzi huu pia, Liyongo anaitwa *simba wa miji* na *ngao*.

Allen (1993:228) kama alivyonukuliwa na Gichamba (khj), anaeleza kuwa neno “Fumo” linalofasiriwa kama mwana mfalme lilitumiwa na familia ya kifalme ya Pate kwa jina Nababani, kama neno la heshima na huenda walitoa jina hilo kutokana na jina Fumo Liyongo, baada ya ushindi wao dhidi yake katika karne ya kumi na tano. Liyongo mwenyewe alikuwa mwana wa mfalme na akawa mfalme wa dola ya Ozi.*Uteuzi wa Fumo Liyongo* pia unatueleza kuwa Liyongo alikuwa ni mtume wa heshima na adabu. Aliitwa na sultani wa Pate afike mjini Pate ili Wagalla wamtazame na alifanya hivyo. Si ajabu kuwa Nabahani walitumia neno “Fumo” kuashiria heshima. Kila jina la shujaa lina siri ya ushujaa kama vile urembo, umaarufu, uganga uchawi, ujasiri n.k.

Katika *Utenzi wa Nabii Isa*, Isa pia alipewa majina mengi kama Rasuli (ubeti 792), Rasili, Mtume (ubeti 347). Katika Bibilia Nabii Isa anitwa Simba wa Yuda, Mshauri mwema, Mwalimu, Emanueli (Mungu pamoja nasi). Sifa hizi zote zinamtambua sifa za nabii Isa Nabii Isa kama Shujaa halisi wa kidini.

### 3.1.9 Shujaa Huwa na Akili Pevu

Mashujaa ulimwenguni huwa wenye akili pevu na kung’amua mambo yaliyofichika. Vilevile, uwezo huu, mara nyingi huwasaidia kunusurika kutokana na njama za maadui zao na kwa hivyo huwawezesha kuishi hadi pale watakapokamilisha majukumu yao katika jamii. Fauka ya hayo, shujaa huweza kutabiri yale ambayo yatatokea baadaye. Isa, shujaa wa wakristo, kwa mfano

aliyatabiri mambo mengi ambayo hatimaye yalitokea, kwa mfano, alitabiri kifo chake, kufufuka na hata kupaa kwake mbinguni.

Fumo Liyongo naye, akili zake pevu zilimwezesha kuhepa mitego ya adui yake Daudi Mringwari. Sultani wa Pate (Mringwari) alitaka kumwangamiza kwa sababu alihofia kuwa Liyongo angempokonya ufalme wake. Liyongo aling'amua njama hizo na kuhamia mwituni. Maelezo haya yanapatikana katika *Uteuzi wa Fumo Liyongo* katika beti za 49 na 50. Wadaho na Wasanye walipewa ahadi na sultani ya reale mia moja baada tu ya kumwua Liyongo. Kwa sababu ya ushupavu wake katika vita, Wasanye na Wadahalo walijua kwamba haingewezekana kumuua Liyongo kwa njia ya ana kwa ana. Kwa hivyo walifanya njama ya kumuua kwa hila. Walipoenda bara, walimwendea kwa urafiki wakamwomba awe pamoja nao. Walipanga wawe wakila makoma, hivi kwamba, kwa zamu, kila mmojawao, (akiwemo Liyongo) angepanda juu ya mkoma na kuyatunda makoma. Kila mmoja miongoni mwao isipokuwa Liyongo alitekeleza tarajio la mpango huo. Ikabakia zamu ya Liyongo. Njama yao ilikuwa kwamba, akipanda mkoma wamfume mishale kwa pamoja. Liyongo alitambua nia yao na badala ya kukwea juu ya mkoma, alitumia mishale na kuyaangusha makoma mengi. (*Uteuzi wa Fumo* Liyongo beti za 136 na 140).

Kwa mara nyingine akili arifu ya Liyongo ilimwezesha kuepukana na kifo. Kwa ushairi, alimtuma kijakazi aliyekuwa akimletea chakula gerezani kwamba akamwambie mama yake aupike mkate wa wishwa na humo ndani afiche tupa ili aitumie kukereza minyororo aliyokuwa amefungwa kwayo gerezani. Kila alipotumwa kumpelekea Liyongo chakula kitamu, kijakazi Saada alipokonywa chakula kile na walinzi na kukila. Liyongo alifahamu fika kuwa mkate wa

wishwa si mtamu na walinzi hawangetaka kula chakula ambacho si kitamu. Saada alipouleta mkate ule (ukiwa na tupa ndani), askari walimtukana kwa dhihaka na kumruhusu Saada kumpelekea Liyongo mkate ule.

Japo ni bayana katika utenzi huu kuwa Liyongo alikuwa na akili pevu, haieleweki ni kwa nini anamfunulia mwanawe siri ya kifo chake, licha ya kung’amua ukweli kuwa mwanawe alikuwa na nia ya kumwua. Tunaambiwa:

136 Babake akamwambiya
Wewe kuuliza haya
Dhana nimekudhaniya
Kuniuwa huzengenya.

140. Akamwambia nayuwa
Kijana umefundiwa
Na wewe utahadawa
Hayo wamezokwambiya

Kupevuka kwa akili ya Nabii Isa kunaweza kuthibitishwa na mafundisho aliyoyatoa. Alifunza kwa kutumia vielelezo mbazi ambavyo viliufanya umati uliomfuata kuajabia mafundisho yake. Umati uliohutubiwa na Nabii Isa uliajabia mafundisho ambayo yalitokana na mtu ambaye mwandishi wa *Utenzi wa Nabii Isa* anadai kuwa hakusoma sana.

544 ‟Kwa maneno ya kutimu,
Fasaha na ya ilimu,
Kutujuza tufahamu
Kuwa yeye ni nabia.

546 " Ni mwingi wa taaluma,
Wala sana hakusoma
Na mambo chungu nzima,
Yeye yanamuelea.

**3.2.0 Kugura kwa Shujaa**

Mara nyingi shujaa hutoroka makwao na kuishi ugenini. Mashujaa hufanya hivi ili kuwahepa mahasimu wao ambao mara nyingi huwa ni viongozi. Kwa kuwa majagina mara nyingi huwa na uwezo usio wa kawaida, viongozi wengi huhofia kuwa majagina hawa huenda wakapindua dola zao. Safari ya jagina humtayarisha kutekeleza majukumu au dhima yake katika jamii. Hivyo, safari hizi ni muhimu sana.

Mutiso (1999:31), anaeleza kuwa safari ya shujaa inaweza kuwa ya kiwakati, kimahali, kifikra au kisaikolijia. Katika safari ya kisaikolojia jagina huzinduka kutokana na elimu au mawazo mapya anayopata. Baadaye, huwafunza wafuasi wake mambo wanayostahili kutenda na hivyo kubadilisha mfumo wa jamii. Aghalabu shujaa akigura huenda katika nchi au sehemu nyingine, huwa anapata mazingira au hali nyingine tofauti na ya nyumbani. Hivyo, anakuwa na mtazamo mwingine. Wakati mwingine huenda shujaa asirejee kwao baada ya kugura kama alivyofanya Mbega shujaa wa Washambaa aliyegura kutoka kwao Nguu, baada ya jamaa wake kupanga kumuua.

Daudi Mringwari yule Sultani wa Pate, alipanga njama ya kumwangamiza Fumo Liyongo. Liyongo alipotanabahi hatari iliyomkuba, alitorokea porini ambapo aliishi na Wasanye na Wadahalo. Sifa ya kugura kwa shujaa haijitokezi vyema katika utenzi huu lakini imeelezewa

kikamilifu katika *Bibilia*. Kama ilivyo desturi ya mashujaa wengi, punde tu baada ya kuzaliwa, Nabii Isa alikutana na vikwazo vya kutaka kuuawa na Mfalme Herode, ambaye alihofia kunyang'anywa madaraka, shujaa huyu atakapokuwa mkubwa (*Mathayo* 2:13). Malaika wa Bwana alimtokea Yusufu (Baba wa Isa) katika ndoto na kumweleza amchukue mtoto Isa na mama yake (Mariam) kisha wakimbilie Misri. Ndivyo ilivyo hata kwa mashujaa wengine, misukosuko inapozidi kukimbilia uhamishoni. Baada ya Mfalme Herode kufa, shujaa Isa alirudishwa na wazazi wake kwao Galilaya katika mji wa Nazareti.

### 3.2.1 Mashujaa kwa Kawaida Huwa ni Washairi

Mutiso (1999:21), anasema kuwa kila jagina ni mshairi,mwanafalsafa, mwenye elimu (hata kama hajasoma) na mwenye sifa zote za uzuri na ubaya. Ubaya wake huonekana na maadui wake tu. Baadhi ya sifa za jaginani kama vile urembo, ustahamala, usamehevu, umaasumu, ufukara, ujasiri, ufasaha wa kusema, ujanja, ufadhili na sifa zingine nzuri na mbaya. Mara nyingi mashujaa huwa na kipawa cha ushairi. Mshairi, kwa kawaida huwa na falsafa nzito kuhusiana na jamii. Mashairi huwa yanakubaliwa na wanajamii na hivyo hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mashairi haya huwa zawadi kwa wanajami kwani hudumu hata baada ya kifo cha jagina. Mashujaa wengi hutungiwa nyimbo za kuwasifu zikielezea historia na umuhimu wao kwa jamii.

Japo nabii Isa hakuwa mshairi, na hakuna mashairi au nyimbo alizozitunga, mafundisho yake yamesheheni jumbe zenye falsafa nzito. Alifundisha kwa kutumia vigano mbazi na mifano iliyooana na tajriba za aliowafunza na ndiposa kwingineko anadaiwa kama mwalimu kielelezo.

Fumo Liyongo alikuwa mshairi stadi. Miehe na wenzake (2004) walikusanya nyimbo na mashairi yanayodaiwa kutungwa na Fumo Liyongo. Mashairi haya yanatupa taswira na hulka ya mtunzi, uhusiano wake na jamii, tajriba yake maishani na hata mila na desturi za jamii ya mtunzi.Fumo alikuwa stadi wa gungu na mwao. Hata hivyo, kama tulivyoona hapo awali, chochote kizuri kinachotukia katika jamii huhusishwa na jagina. Hivyo, kuna uwezekano kuwa nyimbo na mashairi yanayohusishwa na Fumo Liyongo huenda kwa hakika iwe kwamba hakuyatunga mwenyewe.

### 3.2.2 Maisha ya Shujaa Huwa ni Dhiki Tupu

Lengo kuu la jagina huwa ni kuikomboa jamii yake kutokana na madhila yanayoikumba. Katika jitihada hizi, majagina hukumbana na upinzani na mateso ya kila nui kutoka kwa wapinzani wao. Mateso haya huwa ni pamoja na kuonewa, kudhulumiwa, kushtumiwa, kusingiziwa, kusalitiwa na hata kuuawa. Kawaida ulimwenguni majagina huishi maisha ya dhiki kutoka kuzaliwa kwao hadi kufa kwao kutokana na majaribio wanayoyapitia. Kama tulivyoona hapo mbeleni, majagina hutoroka makwao ili kuwaepuka maadui wanaowasaka ili kuwaua au kuwaangamiza.Wakiwa uhamishoni, wanaishi maisha ya upweke.

Shujaa huwa haoni raha hasa anapoiona jamii yake ikiteseka na anaweza kufanya lolote kadri ya uwezo wake kuhakikisha kuwa anaikomboa jamii yake kutoka mikononi mwa adui. Matarajio waliyo nayo wanajamii juu ya jagina wao, humkuza na kumtia shime zaidi jagina. Nabii Isa alizaliwa shinani mwa mtende kulingana na utenzi huu. Bibilia kwa upande mwingine, husema kuwa Isa alizaliwa horini mwa ng’ombe kwa sababu wazazi wake walikuwa wamesafiri Bethlehemu kwa sababu ya sensa iliyokuweko na hawangemudu kukodisha chumba cha malazi.

Hali hii ni mfano mmoja tu wa kutudhihirishia mazingira ya dhiki ya majagina. Majagina vilevile katika kupambana na wanaoendeleza dhuluma dhidi ya umma wao, inabidi waishi maisha ya mateso na dhiki kuu.

Madai ya wahakiki wengi kama Mberia (1989), na Achieng (2012), kuwa majagina wanakumbwa na masaibu mengi na vilevile wana maadui wengi ni ya kweli kwani Nabii Isa katika *Utenzi wa Nabii Isa* alikumbwa na matatizo mengi, sio kutofautiana kuhusu unabii wake kwa wana wa Israeli, Waisraeli walihitilafiana kuhusu iwapo Isa ni Nabii au sio (beti 528-630), sio njaa akiwa pamoja na wanafunzi wake, sio kusalitiwa kwake na mmoja wa wanafunzi wake (beti 785-790).

### 3.2.3 Maisha na Matendo ya Shujaa Huwa ni ya Kimiujiza

Mdee na wenzake (2011), wanaelezea muujiza kama jambo la ajabu; kioja, shali, nduli au dungudungu. Nayo *Kamusi ya Tuki* (2004) inasema muujiza ni jambo lisilokuwa la kawaida; shali, ajabu, kioja au dungudungu. Tunakubaliana na maelezo haya kuhusu maana ya neno hili,ila tunaongeza kuwa katika miujiza kuna sifa za uhalisiajabu. Katika *Utenzi wa Nabii Isa*, baadhi ya matendo ya Nabii Isa yamefanya utenzi huu kupata sifa za kiuhalisia ajabu. Uhalisia ajabu kulingana na Wamitila (2003:274), ni dhana iliyobuniwa na msanii wa Ujerumani, Franz Roh inayohusishwa na sifa mbalimbali za kuyaelezea matukio ya kifantasia au ya kiajabu au kichawi kwa namna ya moja kwa moja kwa namna inayoyafanya yaonekane kama ya kawaida. Anadai kuwa mpaka uliopo kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana huwa mdogo sana.

Nabii Isa alitenda matendo ya ajabu kama vile kuwawezesha vipofu kuona. Nabii Isa aliwaponya watu wenye macho pofu na kuwafunulia macho yao (ubeti 422, 425). Miujiza hii ya Nabii Isa pia umeangaziwa kwenye kitabu cha *Mathayo* 9:27-31 ambapo *Biblia* inaeleza kuwa Yesu alipoingia chumbani, alifuatwa na vipofu wawili waliomlilia na kumwomba kuwa, “Yesu mwana wa Nazareti, tuonee huruma”.Yesu alipowauliza kama walikuwa na imani kuwa angewaponya, walionyesha imani yao kwa kuitikia.Yesu aliwagusa kwenye macho na wakaweza kuona.

Nabii Isa aliwaumba ndege kwa udongo aliofinyanga na ndege hao wakaweza kupaa waliporushwa. Baadhi ya sifa hizi ni za kiuhalisia ajabu  na zilidhihirisha kuwa Nabii Isa alikuwa na uwezo zaidi kuliko binadamu wa kawaida (beti 452,472). Jambo jingine la kimiujiza alilolifanya Nabii Isa ni kumtajia yule jamaa aliyeuliza chakula alichokila wakati wa asubuhi na chajio, maji aliyoyatumia, pesa za mfukoni na hata akiba ambayo huyo jamaa alikuwa nayo nyumbani. Huyo mtu alipodhibitisha ukweli wa mambo aliyotajiwa, alikosa kinywa cha kusema na baadaye akakubali kuwa kweli Isa ni Nabii (beti 380-382).

Kule kuzaliwa kwa Nabii Isa bila baba pia ni jambo la kiajabu kwani ni kinyume na hali halisi katika jamii; Nabii Isa alizaliwa bila mama yake kuonana kimwili na mume, (ubeti 588) ila kwa mtume kumvivia tu Mariyamu nguo na akapata mimba ya mtoto Nabii Isa.

Nabii Isa na wanafunzi wake wakiwa jangwani waliomba ili wapate chakula na mwishowe walipewa kutokana na maombi aliyofanya Nabii Isa. Chakula chenyewe kikiwa kinaitwa Maida na kilikuwa kitamu kisichomithilika (beti 746-761).

### 3.2.4 Shujaa Huwa Hawaeleweki kwa Uwazi

Watu katika jamii mbalimbali huwa na mitazamo mbalimbali kuwahusu mashujaa wao. Jambo hili linakubalika haswa katika fasihi simulizi ambapo mtu ana huru wa kueleza masuala kwa namna ambayo anaona yanafaa. Mathalani, kila shujaa huwa na adui pamoja na wafuasi wake wanaompenda. Kila jamii kwa hivyo huchukua mielekeo tofauti kuhusiana na usawiri wa majagina. Kila jamii ina uhuru wa kumlimbikizia jagina wake sifa sufufu na hata kuna uwezekano wa wengine kuzitilia sifa hizo chumvi. Lakini maadui zake, huenda wakampatia jagina sifa chache na za kumkashifu na hivyo kuwafanya majagina kuwa na mitazamo mingi ya kuwasawiri. Hivyo basi, kuwafanya kutoeleweka kwa uwazi, maadamu, kuna mitazamo mingi kuhusiana na mashujaa. Hatuna budi kuelewa kuwa mashujaa watabaki katika hali ya kutoeleweka kwa uwazi jambo ambalo katika usomi lina kubalika.

Kuna masuala kumhusu Fumo Liyongo ambayo yanazua utata. Kuna baadhi ya watu wanaofikiria kuwa Fumo Liyongo hakuwahi kuishi duniani na kuwa ni mhusika tu wa kubuni katika simulizi za Waswahili. Suala la kipindi alichoishi, mwaka aliozaliwa, sifa alizo nazo yakiwemo masuala mengine ni baadhi ya mambo yanayochanganya hadi leo. Kila maulama anatoa maelezo yake kuhusiana na masuala haya kwa misingi ya mtazamo wake tu. Yumkini shujaa mwenyewe huenda asijulikane asili yake, malengo au dhamira yake, wazazi wake, hususan baba mzazi. Aghalabu mama wa shujaa awe siri pia (kama alivyo mama yake Fumo Liyongo).

Nabii Isa vilevile aliwakanganya Wayahudi ambao hawakumuelewa. Kwao walitarajia Masihi ambaye angalikuwa amiri jeshi mkuu ambaye angaliwaongoza katika vita vya ukombozi kutoka kwa Warumi waliokuwa wamewanyanyasa kwa muda mrefu.

### 3.2.5 Mapenzi ya Mama kwa Shujaa

Kwa kawaida jagina hupendana na mama yake kwa dhati na huwa wanashiriki katika mambo mengi ya siri ambayo wanajamii wengine hawafahamu. Mama yake jagina humpa motisha ili atekeleze dhamira yake na huwa kitulizo cha kumliwaza wakati ana dhiki. Wengine huchukulia kuwa mamaye jagina pia ni jagina kutokana na ukaribu wake na jagina. Hata hivyo, huenda asiwe na sifa bia za mashujaa. Kuna dhana ya kisaikolojia ambayo inadai kuwa mwana wa kiume huvutiwa kimapenzi kwa mama yake (Oedipal complex) ilhali mwana wa kike, huvutiwa kimapenzi kwa babaye (Electra complex). Hii humfanya jagina kumwona babake kama adui yake, kwa hivyo hana budi kumwangamiza panapo patikana nafasi.

Liyongo walipendana sana na mamaye kiasi cha hata mamaye kuelewa hisia zake za ndani. Liyongo akiwa gerezani, mamaye angemtayarishia chakula kitamu na kumpatia Saada ampelekee. Hata hivyo, kutokana na utamu wa chakula, maaskari walikuwa wakila na kumsazia Liyongo makombo. Baada ya siku kadhaa, Liyongo aligundua kuwa maisha yake yamo hatarini akamtuma Saada kwa kumtongolea shairi au wimbo uliofumbwa na ni mamake pekee ndiye aliweza kuelewa habari hiyo. Hata askari (“makozi” kwa mujibu wa *Utenzi wa Fumo Liyongo*), hawangeweza kutanzua fumbo lililogubikwa kwenye ufumbo huo. Hayo yote, yalidhihirisha kuwa mamaye Liyongo pia alikuwa mshairi kama mwanawe. Baada ya kupokea ujumbe huo, alifanya jinsi alivyoagizwa na kusaidia kukomesha jaribio la Sultani la kumwua mwanawe.

Baada ya Liyongo kupatikana kisimani na kuwafanya watu kutoteka maji, ni mama yake ndiye aliyeitwa ili aende kumrai ili atoke watu wapate kuchota maji. Mamake alimlongolea mashairi ya kumbembeleza akiwa mbali kwani aliogopa na kutetemeka kwa kutowahi kumwona Liyongo katika hali kama hiyo. Liyongo hakuwa na tabia ya kukaidi amri ya mama yake, ndiyo sababu mama yake aliogopa sana wakati huo.Mama yake hakujua kuwa alishakufa.Alifikiria kuwa wanajamii ndio waliokuwa wamekosea mwanawe. Mama yake alieleza (*Utenzi wa Fumo Liyongo* ub.197 na ub 198) kuwa Liyongo hukasirika kwa nadra sana, lakini akikasirika, hasira zake huwa ni za moyoni. Aidha, baada ya mamaye kugundua kuwa Liyongo alikufa, alilia sana na hatimaye aliandaa matanga ili waombolezaji watoe rambirambi zao.

Ukuruba baina ya Nabii Isa na mamake Maryamu unajitokeza kwa bayana zaidi katika *Bibilia* kuliko katika Utenzi na *Qurani.* Katika *Bibilia*, muujiza wa kwanza alioufaanya Isa ni kufuatia shinikizo kutoka kwa mamake. Walikuwa wamehudhuria sherehe ya arusi katika Kana ya Galileya na divai iliyokuwa imeandaliwa wageni ikaisha. Mamake alipoona hivyo akamuuliza asaidia na hapo akageuza maji kuwa divai. Tukio huli pamoja na kuwa Maryamu alikuwa mmoja waliokuwa wakiomboleza baada ya kifo cha mwanawe ni dhihirisho kuwa Nabii Isa alikuwa kipenzi cha mamake.

### 3.2.6 Kimo na Nguvu za Shujaa

Mashujaa kwa kawaida huzaliwa akiwa na nguvu nyingi.Hata hivyo, anaweza kuzaliwa akiwa dhaifu au mlemavu. Mutiso (khj: 12) anasema kuwa ulemavu huu ni onyo kwa wanadamu kuwa “huyu si kiumbe wa kawaida na atakuwa na nguvu nyingi za ajabu baadaye”. Majagina wa

kihistoria kwa kawaida huwa majitu amabayo yana nguvu na vimo virefu mno. Vimo hivi virefu ndivyo huwafanya wanajamii wamuajabie jagina wao. Majagina wengine huwa na vimo vifupi kuliko watu wa kawaida na hili ni jambo pia linalowafanya wanajamii kumuajabia pia. Sundiata, jagina wa jamii moja huko Mali alikuwa mwembamba na tena mlemavu lakini alikuwa na nguvu za ajabu.

Fumo Liyongo na hata Nabii Isa walidhihiri nguvu za ajabu. Liyongo alidhihiri nguvu za kimwili. Akiwaelezea Wagala kuhusu ushupavu wa Liyongo, mfalme wa Pate anamsifia kwa kusema kwamba alikuwa kama simba, na kwake kutembea usiku na mchana ni mamoja. Kumtokea mtu ghafla kungesababisha mtu huyo kutapa na kulia kwa woga. Kukodoa macho yake kungemfanya binadamu kuzimia. Wagala, ambao pia walikuwa mashujaa wa vita, walicheka kwa dhihaka wakifikiria sultani alikuwa anawafanyia mzaha. Walimwambia sultani kwamba wangependa kumwona Liyongo. Sultani alikubali na akamtumia Liyongo mwaliko. Liyongo alikubali mwaliko na kusafiri hadi Pate.

Katika maelezo ya ziara hiyo ya Pate, picha ya Liyongo tunayoipata ni ile ya mtu mwenye nguvu zisizo za kawaida. Kwanza, tunafahamishwa kwamba safari ya kutoka Shaka, ambako alikuwa akiishi Liyongo hadi Pate, ilimchukua siku mbili badala ya siku nne ambazo zingechukuliwa na binadamu wa kawaida. Pili, anafika Pate akiwa amebeba panda tatu ambazo anazipasua nguvu ya pumzi na mapafu yake:

Liyongo kenda muini
Akipata mlangoni
Panda katia kanwani
Kivuzia kapasua

Kiivuzia hakika

Muini wakashtuka

Panda ikapasuka

Wagala wakasikiya

Liyongo asimuhuli

Akaipiya ya pili

Pandaye isihimili

Na ya pili kapasuwa

Aidha, picha ya Liyongo kama mtu aliyekuwa na nguvu zisizo za kawaida inajengeka zaidi kutokana na maelezo ya vitu alivyovibeba mkobani katika ziara yake ya Pate. Tunaelezewa kuwa kwenye mkoba wake kulikuwa na vitu kama kinu na mchi, aina tofauti tofauti za vyungu, mafiga, kipeto cha mtama na nazi. Kwa kawaida, Wagala walikuwa mashujaa wa misituni na watu wenye vimo virefu. Lakini tunaelezewa kuwa waliokuwa warefu miongoni mwao walikuwa wanamfika Liyongo magotini.

Fumo Liyongo anatofautiana na Nabii Isa katika kimo kwa kuwa kimo cha Isa kilikuwa cha kawaida tu. Lakini alikuwa na nguvu za kufanya mambo ya ajabu kama tuliyoyaangazia katika sehemu ya miujiza ya jagina hapo juu.

### 3.2.7 Majagina Aghalabu Huwa Magwiji Katika Vita

Mashujaa aghalabu huwa magwiji katika vita kwa sababu wanazuka ili kukomboa jamii zao dhidi ya maadui zao. Mashujaa huwa hawaogopi chochote. Ni kutokana na hali ya kivita ndipo

ushujaa wao hudhihirika, hususan mashujaa wa kijamii. Samson katika *Bibilia*, kwa mfano, anasawiriwa kama shujaa wa kivita aliyetumia utaya wa punda na kuwauwa Wafilisti elfu moja (taz. Kitabu cha *Waamuzi* 15:14-17). Uwezo wake wa kivita uliwawezesha Waisraeli kujikomboa kutoka kwa wafilisti baada ya miaka mingi ya dhuluma na unyanyasaji. Vivyo hivyo, Lwanda Magare, Dedan Kimanthi na Fumo Liyongo miongoni mwa mashujaa wengine walifurahia vita. Fumo Liyongo, Shaka Zulu, Sundiata, Lwanda Magere walizuka katika kipindi cha misukosuko ya kivita. Liyongo aliweza kuwakabili watu wengi kwa wakati mmoja, (*Utenzi wa Fumo Liyongo* ub 12 na ub. 35).

Aidha, Liyongo anajitokeza kama gwiji katika ufumaji wa mishale. Anayafuma na kuyaangusha makoma kwa wingi akiwa chini Liyongo pia anakufa akiwa na mishale mikononi huku akipiga goti moja chini tayari kufuma (utenzi wa Fumo Liyongo beti za 65, 66, 180 na 181), unatoa haya maelezo. *Takhmisa ya Liyongo* inamsawiri Liyongo kama asiyeogopa mikuki wala mishale na anakiona kifo kama kitokanacho tu na Mwenyezi Mungu. Lakini si kutokana na kufumwa mikuki na mwanadamu. Aidha, Liyongo anasawiriwa kama mtu anayependa vita sana na anajilinganisha na "mwana kozi". Maelezo haya yanapatikana katika (*Takhmisa ya Liyongo* katika beti zifutazo: 8, 9, 14, 16, 22, 23 na 24.

Kinyume na alivyochorwa Fumo Liyongo, Nabii Isa hakutumia nguvu za kimwili kupigana na maadui wake. Japo amesawiriwa kama mtu jasiri, anapambana na maadui wake kwa vita vya kiroho.

### 3.2.8 Shujaa na Suala la Ndoa

Mashujaa duniani kote, kwa kawaida hawaoi na wakioa huwa hawatilii maanani sana swala la ndoa. Hii inatokana na sababu kuwa shujaa huwa na jukumu la kukomboa jamii kutokana na dhuluma pamoja na taabu mbalimbali. Kwa hivyo, ili shujaa atekeleze dhamira yake, ni sharti awe huru. Ndoa kwa kawaida haimpatii mtu nafasi ya kushughulikia mambo mengine lakini shujaa huwa kwa ajili ya jamii nzima. Ni vigumu mno kukosa kuitumikia kwa madai ya kumliwaza mtu mmoja (mke wake) pekee. Matamanio ya wanajamii kuhusu ukombozi wao yako kwa shujaa wao, kwa hivyo, huchukuliwa kuwa shujaa "huioa jamii". Isitoshe wanawake ndio huwa chanzo cha kuporomoka kwa mashujaa wengi, hata nguli katika kazi bunilizi.

Hata hivyo, kuna baadhi ya mashujaa ambao huoa, japo ndoa yao mara nyingi haiwi dhabiti kwa sababu, jagina huwa hatulii mahali pamoja. Kimathi shujaa wa Wakikuyu, kwa mfano alioa na kuacha familia yake alipoingia msituni kutetea jamii yake. Ajabu ni mpaka leo hakuna anayejua kaburi lake liliko, kwa sababu alishikwa na mabeberu kuuawa.

Fumo Liyongo kama alivyo Lwanda Magere alikuwa na wanawake wengi. Tunaelezewa katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* (ub. 45 na ub. 46) kuwa Wagalla walimpa mke aliyechukua mimba na hatimaye kujifungua mwana wa kiume. Katika mashairi yanayodaiwa kutungwa na Liyongo, tunaelezwa kuwa alikuwa na mpenzi wake kwa jina Kundazi. Pia tunaarifiwa kuwa Liyongo alitilia maanani sana umuhimu wa mwanamke katika maisha ya mwanamume.

Katika *Utumbuizo wa Mwana Mnazi*, Liyongo anatoa mfano kwa kumtumia mwanamke aliyekuwa mpenzi wake. Anasema kuwa yeye ndiye "mpangua hamu na simanzi". Tunaona

kwamba Liyongo anapochelewa kufika nyumbani kipenzi chake aliwaambia vijakazi Saada na Rehema waandae chakula kizuri na kisha waende wakamtafute. Aidha kipenzi chake alienda hatua ya kumlisha akisaidiana na kijakazi wake mwingine katika *Utenzi wa Mwana Ninga*, utenzi ambao unadaiwa kutungwa na Liyongo. Liyongo anasifu sehemu mbalimbali za mwanamke kuanzia utosini na kuteremka hatua kwa hatua hadi nyayoni. Inadaiwa kuwa mwanamke huyo pia alikuwa mpenzi wa Liyongo. Kinyume na Fumo Liyongo, Nabii Isa hakuoa wala kupata watoto na hivyo kuingiana na sifa kuwa majagina wengi huwa hawaoi.

### 3.2.9 Kifuasi cha Shujaa

Mara nyingi shujaa huwa na vifuasi ambavyo huandamana navyo. Vifuasi hivi ni muhimu sana maishani mwa mashujaa mbalimbali. Sahaba wa shujaa yumkini anaweza kuwa mnyama, kijana, dhana fulani, ndege, mti, mdudu, jiwe, kitu, mjinga na kwa nadra sana mwanamke. Kifuasi hawi na kazi muhimu sana bali kumsaidia shujaa kutekeleza lengo lake na yamkini apandishwe cheo kuwa shujaa baada ya shujaa kuwa mgonjwa, kufa au kupotea. Wanawake wengi huwa shujaa kwa sababu ya upelelezi au kwa mapenzi yao juu ya shujaa. Mashujaa halisi wa kike aghalabu walipatikana katika mfumo wa Ujima. Jambo hili linaonyesha vile wanawake wamekandamizwa kihistoria.

Vifuasi husaidia katika kumkamilisha shujaa. Werner (1968: 133) anaeeleza kuwa Mbega shujaa wa Washambaa, aliandamana na mbwa wengi kila mahali alipoenda. Alikuwa anawafundisha mbinu za usasi wa nguruwe, wakiwemo wanyama wengine wa porini. Kuna mbwa fulani aliyempenda sana aliyejulikana kama “Chamfuu”. Anaendelea kudai kuwa jina hili limehifadhiwa na wanajamii hiyo hadi leo. Mbwa huyo alimsaidia Mbega sana katika usasi wa

nguruwe. Baada ya usasi, aliwapa wanajamii nyama ya nguruwe kwa wingi. Wanajamii walifurahi na kumwajabia. Bali na hayo, Mbega alikuwa na mkoba uliokuwa na hirizi ambazo alitumia kutenda mambo yasiyo ya kawaida.

Mtume Musa shujaa wa Waisraeli naye alikuwa na kijiti alichokitumia kutenda miujiza katika harakati za kuwakomboa wana wa Israel kutoka huko Misri. Kijiti hiki hata kilikuwa kikigeuka nyoka wakati mwingine (taz kutoka 4:1–5 kwenye *Bibilia takatifu*). Aidha Yesu Kristo, alidaiwa kuandamana na Roho mtakatifu (taz *Luka* mtakatifu 3:22 kwenye *Bibilia*). Roho Mtakatifu alimwezesha kutenda miujiza pia.

Fumo Liyongo ni vivyo hivyo. Fumo Liyongo kwa mfano alikuwa na mkoba aliopenda kubeba kila mahali aliopenda. Ndani ya mkoba huu mlikuwa na vitu kadhaa ikiwemo mishale aliyotumia vitani. Tunaelezwa katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* kuwa katika ushirika wa kikoa, aliubeba mkoba ambao ulikuwa na uta na mishale (taz ub 65). Alipopatikana akiwa amekufa, alikuwa tayari ametia mshale kwenye uta huku akiwa tayari kufuma (*Utenzi wa Fumo Liyongo*) ub.180 na ub.181.

### 3.3.0 Shujaa Huhusishwa na Zaidi ya Jamii Moja

Jagina mara nyingi hatambuliwi na kuhusishwa tu na watu wake bali pia na watu kutoka jamii zingine. Hata hivyo, jagina wa kijamii hujitolea kufa kupona ili kuilinda jamii yake na mara nyingi huwa karibu na jamii yake kuliko jamii nyingine ile. Huitetea kwa vyovyote ingawa hushirikiana na wafalme wa jamii nyingine katika kuimarisha hali ya amani, utangamano na kuendeleza maisha ya raia wake hadi kwenye ufanisi. Ni jambo la kawaida kupata baadhi ya

watu wakidai kuwa shujaa fulani hutoka katika ukoo wao. Madai haya yanakuwepo kwa sababu kila mtu, kama kaida ya watu hupenda kujihusisha na mtu maarufu au yule ambaye anafanya vitu visivyo vya kawaida au miujiza na kwa sababu hiyo, kila jamiii pia hupenda kujihusisha naye.

Majagina wa kidini kwa mfano, Mtume Muhammadi, Isa (Yesu) na Buddha walikuwa si wa jamii moja bali wa ulimwengu mzima. Licha ya Yesu Kristu kutoka katika ukoo wa Daudi, alichukuliwa na Wakristo wote kama mkombozi wao. Aidha mtume Muhammad ni shujaa wa waislamu wote duniani naye Buddha ni shujaa wa wahindu wote duniani. Licha ya Fumo Liyongo kuwa shujaa wa Waswahili, Wasegeju, Wabajuni na Wapokomo pia hudai kuwa Fumo Liyongo alikuwa ni shujaa wao. Nurse (1994:69), anaeleza katika mahojiano yake na mmojawapo wa wabajuni, kuwa Fumo Liyongo alikuwa Mbajuni. Werner (1915:333) naye anadai kuwa alifahamishwa na mmojawapo wa kijumbe mtoa habari kuwa Fumo Liyongo alikuwa Msegeju.

Watu wa kawaida hufa na kusahaulika baada ya miaka michache. Wanajamii huwa hawaamini kuwa shujaa wao ameaga na wengi huchukulia kuwa ameenda safari na kuwa atarudi siku moja. Kwamba utafiti huu unahusu mashujaa walioishi zaidi ya miaka elfu mbili iliyopita ni idhibati tosha kuwa majagina huwa hai miongoni vizazi na vizazi. Fumo Liyongo na Nabii Isa watazidi kufanyiwa utafiti sio tu na watu kutoka jamii zao, bali pia na watafiti kutoka pande mbalimbali za ulimwengu.

Wengi wa majagina wa kihistoria na wale wa kidini kama Buddha, Muhammad na Isa miongoni mwa wengine, hukumbukwa daima. Kila jamii inawajibika kuwafunza watoto kuwahusu

mashujaa wao, ambao huzuka katika katika vipindi na hali mbalimbali katika jamii hiyo. Jamii moja huenda ikawa na zaidi ya jagina mmoja lakini ni muhali kwa mashujaa wawili kuzuka katika hali na kipindi kimoja katika jamii. Aidha, katika kukumbukwa mashujaa hutungiwa nyimbo, tenzi, mashairi, pia, maandishi chungu nzima hutungwa kwa maumbo mbalimbali na kuhifadhiwa kama kumbukumbu kwa minajili ya vizazi vijavyo. Inaaminika miongoni mwa wakristo na waislamu kuwa kuwa Nabii Isa atarudi ulimwenguni kuikamilisha kazi alioianzisha.

### 3.3.1 Usaliti na Kifo cha Shujaa

Dhana ya usaliti imejitokeza sana katika kazi za kifasihi na inaonekana kuwa ni silaha ya kumwangusha shujaa mfano Lwanda Magere katika kitabu cha *Lwanda Magere*, Samsoni na Yesu katika *Bibilia*. Mtoto wa Liyongo anamuuliza babaye siri ya nguvu zake, anapoambiwa kuwa ni kuchomwa sindano ya shaba kitovuni, anakubali kumchoma baba yake. Hatimaye Liyongo anakufa, kisha mwanawe naye anakufa kutokana na uovu wake. Baada ya shujaa Liyongo kufa watu walisikitika, waliomboleza na wengine walionekana kukata tamaa kwa kuwa shujaa huyu alikuwa ni mtetezi wa watu katika jamii. Beti za 224-226 zinaeleza vizuri jinsi watu walivyomwomboleza shujaa wao.

Kwa upande mwingine dhana hii ya usaliti ina sura mbili yaani faida (anayenufaika baada ya usaliti) na hasara (anayeathirika baada ya usaliti). Kifo cha shujaa pamoja na usaliti vinatupatia motifu ya dhambi na mapatilizi. Ingawa mtoto wa Liyongo alimsaliti babaye ili apewe zawadi nono, hakutimiziwa ahadi hizo. Alinyanyaswa na hatimaye alikufa kama alivyokufa baba yake. Hii inaashiria kuwa katika mapigano kati ya wema na uovu, siku zote wema hushinda.

Jagina hudhurika mahali pamoja tu, kwa silaha ya aina moja tu au kwa njia ya kipekee tu (pia mara nyingi huweza kuponeshwa kwa silaha ya aina moja au kwa njia ya aina moja tu). Kwa mfano, ni sindano ya shaba tu amabayo ingeweza kumwua Fumo Liyongo.

Katika *Utenzi wa Nabii Isa*, usaliti unajitokeza pale ambapo Nabii Isa pamoja na wanafunzi wake waliishi, kula na kunywa pamoja lakini baadaye mmoja miongoni mwa wafuasi wake ndiye aliyemchochea kwa kumtaja kwa wahalifu waliotarajia kumwua (beti 785-790). Nabii Isa alipangiwa njama ya kuuawa, jambo ambalo Mola alibadilisha kwa kuleta mtu ambaye alimfananisha na Nabii Isa kisura na baadaye mtu huyu akateswa, akasulubiwa msalabani na wahalifu wale wakidai kuwa huyu alikuwa ni Nabii Isa mwenyewe.

Mutiso (1999:37) anasema kuwa majagina huwa hawaamini ya kwamba wanaweza kudhurika. Anadai kuwa si ajabu wao kuamini ya kwamba wataishi milele. Wanapopoteza imani hii, (yakutodhurika au kufa) wao huamua ya kwamba hakuna lingine ila watafute kisingizio cha kufa kwao. Anasema wao huamua kufa kikondoo au kuhatarisha maisha yao kwa sababu kifo ni muhimu kuliko maisha. Husema ya kwamba kufa kwao kulikuwa kumebashiriwa au kifo chao ni wokovu kwa ulimwengu mzima na jambo hili ni sharti alitekeleze Mungu. Isa alipaa mbinguni kwa mujibu wa *Utenzi wa Nabii Isa*. Wakristo wanaamini kuwa kifo cha Isa kilitabiriwa kwa kuwa Mungu aliamua kuwarudia tena wanadamu, lakini Yuda Iskariote ndiye aliyepelekea kifo hiki kutokea. Alimsaliti Isa kwa Wayahudi kwa ahadi ya vipande thelathini vya fedha. Kama ilivyokuwa kwa shujaa Liyongo, Isa naye alisalitiwa na mtu wa karibu (mwanafunzi wake). Yuda aliyemsaliti Yesu, baada ya kupewa vipande thelethini vya fedha, alimbusu Yesu, na Wayahudi, Waandishi na Mafarisayo wakamkamata, wakamsulubisha mtini na kumtesa hadi

alipokufa. Wakristo huamini kuwa kifo cha Isa msalabani ndicho gharama ya dhambi na kwamba yeyote amwaminiye na kumfuata, atapata maisha ya milele. Baada ya Isa kuuwa msalabani, pazia la Sinagogi lilipasuka mara mbili na hata kukaingia giza mchana.Ishara hizi zinaingiana na sifa kwamba vifo vya majagina huwa vya kimiujiza.

Taswira ya kifo cha shujaa Isa kinajitokeza kwa namna mbalimbali kama ifuatavyo: Kwanza Wayahudi, Waandishi na Mafarisayo waliona kama wamemkomoa kwa kuwa walidai kuwa anajikweza kwa kujifanya mwana wa Mungu. Pia watawala walifurahi maana watu wengi walimfuata na kumsikiliza. Kifo cha Fumo Liyongo kinatofautiana na cha Nabii Isa katika *Bibilia* kwa kuwa Isa alifufuka baada ya siku tatu ilhali Liyongo hakufufuka.

### 3.3.2 Anamoishi Jagina na Kurudi Kwake Safari ya Mwisho

Shujaa Isa ni jagina wa kidini kama tulivyotangulia kusema. Mutiso (1999:39), anadai kuwa majagina wa kidini kwa kawaida huhubiri kuwa kuna ulimwengu mwingine ambao waliotenda matendo mema huenda baada ya mauko yao. Ulimwengu huu hauna matatizo, ila ni raha na shibe. Anaendelea kusema kuwa makazi haya katika dini ya Usiva huitwa Kilaisa, katika Ukristo ni mbinguni na katika Uislamu ni peponi.

Ulimwengu huu ni ruwaza ya utakatifu, utulivu, amani, raha, uhuru, maisha ya milele, umoja, upenda, kutosheka, utangamano, na kila jambo nzuri. Mutiso (khj), anasema kuwa mahali hapa ndipo makao ya miungu, Mungu na majagina (kabla na baada ya kufa). Ni majagina, miungu na Mungu ambao wanaweza kufika huko. Ni hadi siku ya mwisho tu ambapo waliofuata sheria za

jagina wataweza kuingia mahali hapo. Mahali hapa viumbe wote huishi kwa utangamano, kama hapo mwanzoni.

Wajibu wa jagina, hasa wa kidini ni kutoka katika ulimwengu huu wetu na kwenda katika ulimwengu mwingine au kuja katika ulimwengu wetu au kufanya yote mawili. Hii ni safari ya mwisho ya jagina. Ndio wakati wa kuwahukumu wale wote ambao hawakufuata sheria zae duniani na kuwaongoza wale waliomtii katika kuingia makazi ya raha mustarehe. Ndio wakati wa kuwafufua wafu na kuwaadhibu vikali wawi.

Wakristo na Waislamu wanaamini kuwa Isa atarudi tena duniani kuikamilisha kazi alioanzisha ulimwenguni.Wakristo huamini kuwa anakaa kwenya upande wa kuume wa Mungu na kwamba atarudi duniani kuwahukumu wanadamu kulingana na matendo yao. Waliomkubali na kufuata nyendo zake, wataungana naye mbinguni na walioenda kinyume na mafundisho yake wataenda Jahanamu. Fumo Liyongo hakuwa jagina wa kidini na katika utafiti wetu, hatukupata habari zozote zunazozungumzia habari zake baada ya kifo na kuzikwa kwake katika sehemu ya Kipini.

Kifo cha jagina ni sharti kionekane pigo kubwa kwa dunia nzima.Fumo Liyongo alipokufa Waswahili walisikitika sana kwa kumpoteza jagina wao. Kwa siku kadha Waswahili hawakuweza kuteka maji kisimani, kwa kuwa walidhani Fumo Liyongo alikuwa hai na alikuwa anawazuia kuteka maji. Wafuasi wa Isa pia walitamaushwa na kifo cha isa na *Bibila* inatoa maelezo kuhusu kusikitishwa kwa wanafunzi wake waliojifungia nyumbani na kuongea katika sauti za chini.

### 3.4 Hitimisho

Katika sura hii, tumebainisha kuwa shujaa Isa na Fumo Liyongo wanafanana kwa njia zifuatazo; kuwa wote wanatumia nguvu isiyokuwa ya kawaida kutenda mambo ya ajabu (miujiza), walikuwa na ushirikiano mzuri na jamii zao, walipendwa na watu kiasi cha watawala kuwachukia, walifanyiwa njama za kuuawa, wote walisalitiwa na watu wao wa karibu, baada ya kufa watu waliwaombolezea, wasaliti wa mashujaa wanaahidiwa kupewa fedha, vyeo na mali nyingine baada ya kukamilisha kazi ya usaliti mfano Mfalme anaahidi kuwapa Wasanye, Wadahalo, Waboni na Watwa reale mia iwapo watamleta kichwa cha Liyongo. Pia mwanawe Liyongo anaahidiwa mali, mke na cheo cha uwaziri. Pia Yuda aliahidiwa vipande thelathini vya fedha iwapo atafanikisha kukamatwa kwa shujaa Isa.Waliowasaliti shujaa Liyongo na Isa walikufa baada ya kifo cha mashujaa hao. Hawakuwa waoga, wote ni majasiri.

Kutofautiana kwao kunajitokeza kwa kuwa Fumo Liyongo alitumia nguvu ya uganga au sihiri. Hadhuriki kwa chochote isipokuwa kwa kudungwa sindano ya shaba kitovuni. (Ubeti 143 -144) Nabii Isa alitumia nguvu za Roho Mtakatifu kutenda mambo mbalimbali k.v, kutembea juu ya maji, kuponya watu wengine (*Mathayo* 3:13-17, *Mathayo* 4: 23 -25). Liyongo alioa mke na alikuwa na mtoto wa kiume, ana nguvu za kirijali ilhali Isa hakuoa wala hakuzaa.

Baada ya kufa, Liyongo hakufufuka. Nabii Isa kwa mujibu wa utenzi hakufa ila alipaa mbinguni. Katika *Bibilia*, Isa alifufuka na aliwatokea watu mbalimbali ili kuwadhihirishia kwamba yuko hai (*Marko* 16:1-14). Japo alikufa, wafuasi wa Isa wanaamini kuwa kazi ya kuwakomboa wanadamu ilikamilika kwa kuwa kila anayemwamini anaokolewa na kupatanishwa na Mungu.

## SURA YA NNE

## UMUHIMU WA FUMO LIYONGO NA NABII ISA KWA JAMII ZAO.

### 4.0 Utangulizi

Baada ya kutalii historia za mashujaa hawa wawili, kueleza salua za jamii zao na sifa zao na sifa bia za kimashujaa, itatubidi tupige hatua kwa kuangazia michango yao kwa jamii zao husika, na katika ulimwengu wote kwa jumla.

Jamii ni kama mfumo au kiunzi imara ambacho huwa na taasisi au mifumo midogomidogo mingi ndani yake. Taasisi hizi ni kama vile, taasisi ya utamaduni, ambayo pia, huwa na taasisi nyingi ndani yake. Ili mfumo mzima uwe mkamilifu, ni lazima kuwe na kila nia ya kudumisha na kusawazisha hali mbalimbali katika jamii. Taasisi ya ushujaa kwa hivyo, huwa na nafasi kubwa mno ya kurekebisha mambo na kuleta mabadiliko fulani katika hali ambazo zimeenda kombo katika jamii. Jagina huzuka kwa ajili ya wanajamii, kila kitu anachokitenda hulenga kuwanufaisha wanajamii kwa jumla. Fumo Liyongo na Nabii Isa walikuwa na umuhimu mkubwa kwa jamii ya Waswahili na Wayahudi Mtawalia.

### 4.1.1 Kitambulisho cha Kitaifa/Kijamii

Mara nyingi, shujaa huwa kitambulisho cha taifa au jamii yake. Shujaa mmoja kwa mfano, katika jamii husika huwa kipengele kikuu kinachowakilisha mfumo mzima wa jamii hiyo. Kwa kulitaja tu jina la Nabii Isa au Fumo Liyongo, itakuwa kana kwamba unarejelea kwa jumla jamii wanazoziwakilisha. Jamii ya Wakristo na Waislamu inatambulika kote duniani kutokana na jina la Nabii Isa na vivyo hivyo, jamii ya Waswahili kutambulika kwa kulitaja jina la Fumo Iyongo ni kipengele kimoja muhimu kabisa ambacho aghalabu kikitolewa, jamii husika itabaki “uchi”.

Huenda mtu yeyote asilijue jambo lolote lingine au hata mila za Waswahili au Wayahudi bila kuwataja nabii Isa na Fumo Liyongo.

Liyongo, kwa mfano, ana umuhimu mkubwa katika kutambulisha jamii ya Waswahili katika ngazi za kimataifa ingawa aliishi miaka mingi iliyopita, sifa zake, maumbile na matendo yake yaliwavutia watu wa kawaida na wengine wengi kutoka nchi za mbali (kimataifa). Edward Steere (1970), miongoni mwa wazungu wengine huwakusita kukusanya habari kuhusu Liyongo na kuziweka katika maandishi. Steere (1870; VI) anadai kuwa Waswahili wanajitambulisha pakubwa na Liyongo. Hata baada ya miaka mingi ya mauko yake, bado anaathiri nafsi za watu katika jamii ya Waswahili, hata ingawa, Wapokomo, Wajabuni, na Wasegeju wanadai kuwa Liyongo alikuwa shujaa wao, yeye sanasana alionekana kujihusisha na kujitambulisha na jamii ya Waswahili ambayo inampenda na kumwajabia mno. Wapokomo walidai kuwa Liyongo ni mbaya ilhali Waswahili kwa upande wao, wanamwonea fahari kwa vile aiwasaidia kujikomboa kutoka mikononi mwa maadui zao. Vivyo hivyo Nabii Isa alichukuliwa na adui zake kuwa mbaya kwa kuwa alikufuru kwa kujiita “mwana wa Mungu”, ilhali kwa wafuasi wake alikuwa Masihi aliyetabiriwa katika *Agano la Kale* na ambaye angewakomboa na kuwaelekeza katika ufalme usio na mwisho.

**4.1.2 Ukombozi na Muungano wa Jamii**

Kama tulivyotangulia kusema katika sura ya pili, hakuna jagina anayezuka katika ombwe tupu.Kila jagina huzuka katika hali na kipindi maalum katika jamii maalum ili kuikomboa kutokana na masaibu fulani.

Masaibu kuwa pamoja na uvamizi wa mara kwa mara na maadui, unyakuzi wa ardhi na rasilmali zingine za wanjamii kama walivyofanya mabeberu barani Afrika, mizozo katika utawala wa jamii, matatizo ya kiuchumi, dhuluma zinazojitokeza kutokana na ukabila katika jamii, matatizo ya kiuchumi, dhuluma zinazojitokeza kutokana na ukabila katika jamii. Kutokana na haya masaibu yote, ni lazima shujaa azauke ili kuleta umoja na kuunganisha wanajamii na kusawazisha mfumo ulioenda kombo. Pia ukosefu wa vitu au vifaa muhimu hurekebishwa na shujaa hata kuwaelekeza wanajamii kuhusiana na masuala ya kidini, miongoni mwa mambo mengine ambayo iwapo jagina hatazuka katika kipindi anapohitajika, kuna uwezekano kuwa jamii hiyo itabakia katika shida zizo hizo.

Wanaamii walijitokeza kwa wingi kila mara waliposikia kuwa Fumo Liyongo angezitongoa nyimbo zake, kwa mfano, alipokuwa gerezani akingojea kuuawa na Sultani (*Utenzi wa Fumo Liyongo* beti, 111, 112, 113, na 114), kuwa watu walijitokeza kwa wingi na mshairi alilinganisha hafla hiyo na ile ya harusi. Ngoma za gungu ziliendelea kuitambulisha jamii ya Waswahili na kuwaunganisha katika sherehe mbalimbali hata baada ya kifo cha Liyongo. Aidha, kifo chake kiliwahuzunisha watu wengi waliomwona kama ngao yao dhidi ya maadui zao. (*Utenzi wa Fumo Liyongo* ub 225 na 226).

Nabii Isa, kwa mujibu wa utenzi, alinusuriwa na mola wake kwa kupaa juu mbinguni lakini waislamu wanaamini kuwa atarejea kukamilisha kazi aliyoianzisha ulimwenguni. Wakristo wanaamini kuwa aliwakomboa waumini na wafuasi wake. Alipokufa, wengi walisikitikia kifo chake. Kutokana na kifo chake, wanaamini kuwa watarithi ufalme wa mbinguni. Ni kutokana na jukumu la kuwakomboa wanajamii ndiposa shujaa huchukuliwa kama zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu na hivyo, kuwafanya waabudiwe hata baada ya mauko yao.

### 4.1.3 Kioo cha Jamii/Historia ya Jamii

Tunaweza kudai kuwa shujaa, kama ilivyo fasihi, ni kioo cha jamii. Shujaa huwa kama kiwakilishi cha jamii haswa katika kipindi cha historia alichozuka na kuishi. Kwa kuelewa historia ya shujaa wa jamii fulani katika kipindi fulani, basi tunaweza kupata taswira kuhusu mfumo wa jamii ile. Kwa kawaida, madhila, mateso, dhuluma, ufanisi na masuala mengine yote yanayomkumba shujaa hutupatia picha kuhusu hali ilivyo katika mfumo mzima wa jamii yake. Mifumo kama ya siasa, mila, uchumi na masuala mengine ya kitamaduni hujulikana tu baada ya kumtalii shujaa wa jamii husika. Kwa vile shujaa huzuka katika jamii fulani katika kipindi na hali Fulani kutimiza malengo na dhamira fulani haswa ya ukombozi katika jamii yake, hivyo basi, kwa kuangazia shujaa huyo, kabla ya kuzuka kwake, wakati wa enzi zake na baada ya kifo chake, (maisha yake kwa jumla) kutusaidia kuelewa historia ya jamii yake.

Maelezo kuhusiana na sifa na historia ya mashujaa hawa wawili yametupatia nafasi nzuri ya kuihakiki jamii ya Waswahili pamoja na Wayahudi. Kwa kupitia kwao haswa, tumepata kuwa jamii hizo zote zilikumbwa na mizozo na mivutano ya hapa na pale ikiwemo ya kivita, kiuongozi, kiuchumi, kidini, kitamaduni n.k. mathalan, dola mbalimbali zilizotawaliwa na wafalme kulikuwa na ung’ang’aniaji wa madaraka ambao ulisababisha njama na hila mbalimbali za usaliti kutumiwa, uvuziaji na uvinjari pia, kulikuwepo na masuala mengi kama vile uvamizi, dini, biashara, tohara, mapenzi, mauaji, kilimo, ufugaji, sheria, ngoma na masuala mengine mengi ya kitamaduni ya jamii zilizowazaa mashujaa wetu wa utafiti.

Mashairi, misemo pamoja na nyimbo mablimbali zilizotungwa na waja wengine au hata zilizodaiwa kutungwa na mashujaa hawa ukwahusu hutusaidia kuelewa aina ya mazingira

yaliyomo katika jamii zao. Kwa mfano, tunapata kujua baadhi ya miji ambayo Fumo Liyongo aliwahi kutembelea katika harakati zake za kugura hapa na pale. Tumetajiwa miji kama vile Pate, Shaka, Ozi, miongoni mwa miji mingine. Aidha, tumeelewa kuwa kulikuwa na milima na mito. Mto Tana ni mojawapo ambamo Liyongo alienda mara kwa mara kuoga.

Bali na hayo, tunatajiwa majina ya vifaa mbalimbali kama vyungu, mafiga, mimea, miti na misitu katika mazingira ya Fumo Liyongo. Vilevile, hali za maisha za majirani wake Wasanye na Wadahalo pia zimeangaziwa. Tunaambiwa waliishi mwituni wakila matunda mbalimbali kama makoma.

Hata hivyo, utamaduni ya jamii yoyote ile unaweza kubadilika kutokana na hali mbalimbali katika jamii kama vile, vipindi mbalimbali, mpito wa wakati, utangamano na maingiliano na jamii nyingine, elimu, dini n.k.

Mara nyingi, kutokanana na nafasi ya hadhi ya juu aliyopewa jagina katika jamii yake pamoja na kutegemewa katika kila jambo maishani, yeye huwa na uwezo wa kubadilisha mkondo wa maisha ya jamii yake atakavyo (kwa sababu anategemewa katika kila kipengele cha utamaduni wao). Licha ya kuzikomboa jamii zao kutokana na tishio la maadui, Nabii Isa na Fumo Liyongo walileta mabadiliko makubwa katika vipengele mbalimbali vya utamaduni (maisha) vya jamii zao. Nabii Isa na Fumo Liyongo walijitokeza bayana kama watetezi na watekelezaji wa imani, mila na desturi mbalimbali za jamii zao. Kwa njia za mafundisho, nyimbo, mighani na ughani wa mashairi huku wakishirikiana na wanajamii wengine.

Liyongo mwenyewe alikuza, kuendeleza na kuimarisha utamaduni wa Waswahili kwa kuasisi gungu wa mwao, ngoma ambazo zimekuwa hai katika jamii ya Waswahili huku zikichezwa katika shrehe mablimbali na haswa wakati wa harusi. Frankl (1993:130). Akinukuliwa na Gichamba (2005:124), anaeleza kuwa ngoma ya gungu (ikijumlisha nyimbo za Liyongo), huwa inachezwa saa za asubuhi wakati wa kuamkia siku ya kila mwaka.

Nabii Isa kwa upande mwingine amekuwa kielelezo kwa jamii yake na ulimwengu mzima kwa jumla. Huyu ni shujaa wa kidini, ambaye maisha na matendo yake yameangaziwa katika dini mbili zilizo na ufuasi mkubwa ulimwenguni. Kitabu cha *Injili* alichokiachia umma wake kama zawadi ya jagina, kingali kinashikilia sehemu kubwa ya imani ya waumini wa imani zote mbili. Kwa hivyo, imani na shughuli za kitamaduni zilidumisha umoja, mashikamano na utangamano baina ya watu. Maadili pia yaliendelezwa. Fumo Liyongo na Nabii Isa walitumia tamaduni hizo ili kuziweka jamii zao katika mfumo mmoja imara.

### 4.1.4 Mabadiliko Katika Mfumo Mzima wa Jamii

Baada ya shujaa kutekeleza jukumu la kuikomboa jamii yake kutokana na misukosuko mbalimbali, huwa hachoki, bali huunda mikakati na sheria kabambe na mpya za kumwezesha kubadilisha maisha ya jamii yake kwa jumla. Kama kulikuwa na sheria ambazo ziliwafinya na kuwadhulumu wanajamii, huziondoa, na kuleta nyingine mpya. Hata hivyo, kuna wakati ambapo shujaa anaweza kuzua mikakati, sheria mpya na mabadiliko yasiyoungwa mkono na wanajamii. Kwa mfano, Liyongo aliwatoza Wapokomo kodi ya juu, jambo ambalo liliwasinya sana..

Mabadiliko ambayo yanaweza kuletwa na shujaa ni pamoja na mabadiliko katika mikakati ya kivita, uzalishaji mali, sheria, mahusiano na jamii zingine pamoja na kuleta amani na kufanya biashara n.k. Fumo Liyongo na Nabii isa walileta mabadiliko makubwa katika jamii zao.Mabadiliko haya ni kama kuleta umoja miongoni mwa jamii.

### 4.1.5 Ruwaza Bora ya Kufuatwa na Wanajamii

Kama tulivyodokeza hapo mwanzo, shujaa ni mtu ambaye yu tayari kuhatarisha maisha yake kwa manufaa ya jamii yake. Ni yule mtu ambaye ana mapenzi kwa wanajamii, jambo ambalo huwafanya wanajamii kutaka kujitambulisha naye hata baada ya mauko yake. Matendo, sifa na hulka za kiajabuajabu za jagina hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia za masimulizi na hata kupitia kwa watoto wengi ambao aghalabu huvutiwa na ngano katika maandishi na masimulizi na hata filamu zinazowasawiri mashujaa. Majagina hawa huwa ni ruwaza bora bora kwa watoto mbalimbali, ikiwa kazi hizi zitawasawiri katika uigizaji wa hadithi za kazi bunilizi au zile zinazowasawiri mashujaa wa kihistoria.

Bali na hayo, mashujaa huathiri maisha ya mtu binafsi, jinsi mtu anavyotazama mambo. Huenda mtazamo wake ukabadilika baada ya hisia zake kuvutiwa na shujaa wao. Shujaa kwa kawaida huyafanya mambo kwa ajili ya manufaa ya jamii nzima si kwa manufaa yake mwenyewe. Huenda mtu akapata mshawasha wa kufanya hivyo pia. Huenda baadhi ya wanajamii wakaiga vitushi vya shujaa wao, utaratibu wa mbinu zake.

### 4.1.6 Fahari ya Jamii Zao

Kama tulivyodokeza hapo awali katika sura ya kwanza, kila jamii huwa na shujaa wao, humkuza, humwona kama mkombozi wao, humwaajabia na kumwonea fahari. Juhudi za jagina,

mara nyingi, hufurahiwa na kukumbukwa milele. Si ajabu kupata wanajamii wakifunza vizazi vijavyo kuhusu matendo, historia na sifa za jagina wao hususan pale ambapo huyo jagina alitekeleza dhamira yake vizuri kwa umma. Jamii huajabia maisha yake yote hata baada ya mauko yake, kwa mfano katika kufundisha kuhusu jagina ulimwenguni, walimu wa Kiafrika katika shule hulinganisha majagina wa Kiafrika na kujaribu kuonyesha ukuruba uliopo baina ya vitushi na maumbile ya majagina hao wote.

Waama, Fumo Liyongo na Nabii Isa wakiwa majagina miongoni mwa wengine wa Kiafrika na wa kidini mtawalia, waliwatetea watu wengi kote duniani. Ni fahari kubwa wala sio tu kwa Waswahili na Wayahudi kwa kupitia uwezo wao, vitushi na maumbile yao, bali pia kwa ulimwengu mzima. Walitekeleza na kutimiza dhamira zao kwa kutumia nguvu, rasilimali na mbinu zenye taathira kubwa katika kutekeleza masuala makubwa na ya ajabu bila kutegemea usaidizi wa wageni kutoka ng'ambo. Kwa hivyo, Waswahili na Waafrika kwa jumla, bali na kujivunia utamaduni wao, wanaonea fahari juhudi za shujaa Liyongo hadi leo. Nabii Isa bali ni kuwa kuwakomboa Wayahudi, ni jagina ambaye ana ufuasi mkubwa sana ulimwenguni.

Hata kama wazungu waliwachukulia waafrika kuwa watu wasiostaarabika na washenzi, ni dhahiri kuwa ndani ya huu "ushenzi" mlikuwemo na ufahari na ustadi mkubwa na hasusan kwenye mifumo ya miundo misingi ya waafrika wenyewe. Utawala bora wa majagina, upanuzi wa milki zao, ulinzi wa watu, utangamano wa umma wake, matumizi ya mbinu na mikakati maridhawa ya kivita na ukuzaji wa utamaduni ya jamii zao ni masuala yanayoonewa fahari na wanajamii na watu wengine kutoka uga wa kimataifa. Waafrika walikuwa na taasisi na tamaduni zilizofuata utaratibu fulani uliokubaliwa na wanajamii wake.

Kwa, hivyo, kwa mujibu wa mbeberu, mwafrika ni mshenzi pamoja na tamaduni zake ilhali kwa jicho la mwafrika, yeye na tamaduni zake ni zenye ustaarabu wa hali ya juu, ambao kwa kiasi kiukubwa umetetewa na kuendelezwa na majagina wao. Kulingana na Kenyatta (1922:), Waafrika walikuwa na mfumo faafu wa utozaji kodi, uamuzi wa kesi, njia za kuabudu, njia za uzalishaji mali (kilimo, biashara, uvuvi, utamaduni, useremala n.k), ndoa, tohara, maziko, uhifadhi wa mazingira, njia ya kuwakumbuka mashujaa wao, miongoni mwa mbeko na tamaduni zingine.

Mzungu lazima atilie maanani uwezo wa mtu mweusi katika kujikomboa kutoka katika hali duni na kupaa juu hadi katika ngazi za ufanisi mkubwa uliodhihirishwa na sifa na matendo ya mashujaa Kiafrika, Fumo Liyongo na Nabii Isa wakiwemo.

**4.2 Hitimisho**

Kama tulivyotangulia kusema katika sura ya kwanza, tendi nyingi huwajenga mashujaa wake katika hali ya kuwafungamanisha na matatizo yanayoikabili jamii husika. Hufanya hivyo kwa lengo la kuonyesha kuwa shujaa ni zao la jamii, na kama ni zao la jamii, hana budi kukumbana na matatizo kama wanajamii wengine. Pia, hufanya hivi kwa lengo la kuwaonyesha wanajamii ushujaa wa shujaa katika kukabiliana na matatizo mbalimbali, kwamba hutofautiana na watu wa kawaida. Aidha, hufanya hivyo kwa lengo la kuwaondolea wanajamii hofu na kuwahakikishia usalama wao pindi wapatwapo na matatizo, kuwa, wanaye mwokozi atakayewaokoa katika matatizo yao. Katika sura hii, tumejaribu kuyathibitisha haya kwa kujikita katika kuchambua ujagina wa wahusika wetu kama ulivyojitokeza katika *Utenzi wa Nabii Isa*, na *Utenzi wa Fumo Liyongo.*

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Hitimisho

Katika sehemu hii, tutaangazia matokeo ya utafiti wetu, pamoja na masuala mengine ambayo yalijitokeza katika mchakato mzima wa utafiti huu, huku tukirejelea malengo ambayo tuliazimia kuyatekeleza mwanzoni mwa utafiti wenyewe.

Ni bayana kuwa suala la mashujaa ni pana mno na huhitaji uelewa wa kina wa mazingira yanayowazaa, pamoja na historia, na falsafa zao za maisha. Mada hii ya majagina ina mvuto wa kipekee hasa tunapowatazama kwa mkabala wa kiulinganishi. Shujaa ni asasi au taasisi ambayo ina mchango mkubwa katika jamii. Majagina wa kidini na wa kihistoria wako na wamechangia pakubwa katika kuwepo kwa hali mbalimbali katika jamii za sasa. Hivyo, wanapaswa kumulikwa kwa jicho pevu, ili kuuweka wazi mchango wao kwa vizazi vijavyo.

Utafiti wetu ulichukua mwelekeo ambao ulifumbata maswala kadhaa, ambayo, ni muhimu katika kutoa picha bayana ya jagina kwa jumla. Katika sura ya kwanza, tulitanguliza somo la utafiti wetu kwa kuangazia usuli wa utafiti na masuala muhimu na ya kijumla ambayo yangetoa mwongozo wa kufikia malengo ya utafiti wetu.

Katika sura ya pili, tulilenga kuiangazia historia ya Nabii Isa, na ile ya Fumo Liyongo katika mkabala mzima wa historia ya jamii zao, huku tukionyesha mazingira, vipindi na hali za kijamii zilizowazaa. Tulipata kuwa mashujaa hawa walizuka kutokana na mahitaji fulani. Mashujaa

hawa wawili walizuka katika kipindi cha misukosuko katika jamii zao na kuwa walizuka ili kuitatua misukosuko hiyo.

Katika sura ya tatu, tulitalii sifa za majagina hawa wawili kiulinganishi, na kupata kuwa shujaa Fumo Liyongo na Nabii Isa wana sifa zinazolingana kwa kiasi kikubwa. Tofauti zilizoko ni chache mno kama vile, kuhusu utabiri wa kuzaliwa kwao, swala la ndoa, kufa kwao na utetezi wa cheo. Hivyo, utafiti huu umechangia madai kuwa sifa za mashujaa duniani kote ni karibu sawa. Katika sura ya kwanza, Mberia (1989) na Mulokozi (1999) walitutolea baadhi ya sifa za kishujaa za Fumo Liyongo. Utafiti wetu umebaini sifa zaidi za Fumo Liyongo na Nabii Isa, ambazo zinaoana na za mashujaa wengine ulimwenguni ambao hatujawaangazia.

Fumo Liyongo na Nabii Isa, wana sifa za kishujaa ambazo ni karibu sawa. Tumeona kuwa sifa hizi za kiajabu ajabu ndizo ziliwakuza pamoja na kukuzwa na jamii zao. Hivyo, kila mwanajamii humsawiri jagina wake apendavyo na kulingana na mtazamo wake. Kwa mintarafu hii, kuna wanajamii ambao walitiilia chumvi sifa za majagina wao, na wengine kuzipunguza, hasa wale ambao jagina alikuwa adui kwao. Kutokana na jinsi Liyongo amesawiriwa kwenye *Utenzi wa Liyongo*, umefanya baadhi wa watu kutoamini au kutiilia shaka kuwa aliweza kuishi. Utafiti wetu umebaini kuwa wanajamii humsawiri shujaa wapendavyo na hivyo hiki hakipaswi kuwa kigezo cha kupima iwapo jagina aliishi au la.

Katika sura ya nne, tumepata kuwa shujaa huzuka ili kutekeleza wajibu fulani muhimu katika jamii. Hivyo, jagina ana umuhimu sana kwa jamii yake. Umuhimu huu unajitokeza siku nyingi

hata baada ya kifo chake. Hii ndiyo sababu sifa moja ya jagina ni kuwa ‘hafi’ na hukumbukwa daima na jamii yake.

Matokeo yetu yamelingana na nadharia tete ambazo zilituongoza katika mchakato mzima wa utafiti wetu. Ilidhihirika katika matokeo ya utafiti wetu kuwa Liyongo na Isa ni mifano mizuri ya majagina wa kihistoria na wa kidini. Mashujaa hawa pia wana nafasi muhimu sana katika historia ya ulimwengu kwa jumla kwa sababu wanaweza kuwekwa katika kiwango sawa na cha mashujaa wengine ulimwenguni. Matokeo haya vilevile yamedhihirisha kuwa, sifa za mashujaa hawa kwa kiasi kikubwa hufanana. Pia mtazamo kuwa mashujaa hawa ni muhimu kwa jamii zao umedhihirika.

Katika kuzipambanua sifa za kishujaa za Fumo Liyongo, tungo za kimsingi ambazo tulizirejelea ni pamoja na *Utenzi wa Fumo Liyongo*, *Takhmisa ya Liyongo* na mashairi na nyimbo zinazodaiwa kutungwa na Fumo Liyongo, miongoni mwa kazi zingine. Kwa upande wa Nabii Isa, tuliurejelea *Utenzi wa Nabii Isa* pamoja na *Qurani* na *Bibili*a ili kushadidia sifa, maisha na hata falsafa ya shujaa huyu. Pale tumemlinganisha shujaa huyu wa kidini na wengine wa kihistoria, si kwa nia ya kudhalalisha dini au imani ya mtu yeyote, bali ni katika kujaribu kuweka wazi sifa za kishujaa ambazo zinadhihirika kwa majagina wengine duniani.

Hakuna utafiti wa kina tuujuao uliofanywa hapo awali unaomlinganisha shujaa wa kidini na wa kihistoria, pamoja na umuhimu wao kwa jamii zao. Hivyo basi, ni imani yetu kuwa pengo lililokuwepo kiusomi litazibwa kupitia kwa utafiti huu.

## 5.1 Mapendekezo ya Utafiti

Katika utafiti wetu tumemlinganisha Isa ambaye ni jagina wa kidini wa jamii ya Wayahudi, na Fumo Liyongo ambaye ni jagina wa kihistoria wa jamii ya Waswahili. Majagina hawa wametoka katika janibu mbili ambazo ni tofauti kijiografia, kimila na kidesturi, na hata katika vipindi walivyoishi. Tungependekeza utafiti zaidi ufanywe unaowalinganisha mashujaa zaidi wa kidini kama vile Gautama Buddha au Mtume Muhhamad, na mashujaa wengine wa Kiafrika kama vile Kimathi, Magere, Mirambo, Kinjeketile, Kibwebanduka n.k ili kuonyesha ni kwa kiwango gani sifa zao za kijagina zinavyoambatana na sifa bia za mashujaa.

Mashujaa wengi wa kihistoria na wa kijamii wa Kiafrika hawajafanyiwa utafiti wa kutosha. Hili ni pengo kubwa la kiusomi ambalo linastahili kujazwa. Ni bayana kwamba mashujaa hawa walichangia pakubwa katika harakati za ukombozi na ufanisi wa jamii zao. Mchango huu unafaa kuwekwa wazi ili vizazi vya sasa na vijavyo viweze kuzifahamu juhudi za mababu zao katika kupigania uhuru, ili kuzikomboa jamii zao na hivyo, kufuata nyayo zizo hizo. Majagina hawa ni kama vile, Kimathi, Magere, Mirambo, Kinjeketile, Kibwebanduka miongoni mwa wengine wengi, wanaoshikilia nafasi muhimu sana katika historia ya Afrika, na ulimwengu mzima kwa jumla. Ni vema ulinganishi wa kina uweze kufanywa baina ya majagina hawa na kuzipambanua sifa zao za kijagina na pia kuweka wazi michango yao kwa jamii zao.

## MAREJEO


Abdulaziz, M.H (1979) *Muyaka: 19th Century Swahili Popular Poetry*.Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Allen, J. V (1977) *Al Inkishafi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

_________ (1993) *Swahili Origins: Swahili Culture and the Shungwaya Phenomenon*. London: James Currey.

Achieng, O.B (2012) Sifa za mashujaa na umuhimu wao kwa jamii zao: Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Lwanda Magere.Chuo kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Chiraghdin, S. Nabhany, A.S na Baruwa, A. (1975) Tarehe ya Ushairi wa Kiswahili, *Mulika Na. 7* uk 59-67.

Chittick, N (1984) *Manda Excavations at an Island on the Kenyan Coast.* Nairobi: B.I.E.A

Freeman-Grenville (1954-1955) Ibn Batuta's visit to East Africa A.D1332: A Translation.*Ugandan Journal*, uk 1-6.

Gichamba, J.M (2005) Sifa za mashujaa na umuhimu wao kwa jamii zao: Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu.Chuo Kikuu Cha Nairobi. Haijachapishwa.

Gunnep, A.V (1960) *Rites of Passage.*London: Routledge & Kegan Paul.

Http / google (2013) The Classic Literary Hero, Mswada ambao haujachapishwa.

Http / google (2005) Al Islam.Org/Kiswahili Vitabu: Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu. Mswada ambao haujachapishwa.

Jung, C. J (1968*) The Archetypes & The Collective Unconscious*. London: Routledge & Kegan Paul Ltd

Jung, C. J (1972) *Four Archetypes: Mother, Rebirth, Spirit, Trickster*. London: Routledge & Kegan Paul ltd

Kalinjuma, D. (2013) *Jaala ya Shujaa wa Tendi za Kiafrika na Ulaya*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Knappert, J. (1982) *Myths and Legends of the Swahili*.Nairobi: Heinemann Educational Books.

_______ (1979) *Four Centuries of Swahili Verse: A Literary History and Anthology*. London: Heinemann Educational Publishers.

Mbele, J.L (1986) The Liongo Fumo Epic and the Scholars'. *Kiswahili* 53/1 na 53/2 uk 128-145.

Mberia, K. (1989) Fumo Liyongo *Mulika Na 21*. Uk 25-43.

Mbotela, J.J (1959) *Uhuru wa Watumwa*.Nairobi: Nelson.

Mdee nw (2011): *Kamusi ya karne ya 21*.Nairobi: Longhorn Publishers.

Miehe,G.N.,Abdalla,A,Bhalo,A.N.J.,Nabhany,A.,Baschiera,A.,Dittemer,C.,Topan,F., Abdulaziz, M.H., Khamis, S.A.M., Omar, Y.A. na AL-Bakary, Z.M.F (2004) *Liongo Songs: Poems Attributed To Fumo Liyongo*.Koln: Grudiger Koppe Verlag.

Mulokozi, M.M. (1999) *Tenzi Tatu za Kale*.Dar es salaam: TUKI.

Mutiso, K. (1985) 'Hurafa na uyakinifu katika Hamziyyah' Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

______ (1990) Fumo Liyongo na kazi zake. Haijachapishwa.1999)

______ (1999) Sira ya Majagina Buddha na Muhammed. *Swahili Kolloquim Universitat,* Bayreuth. Mei 14-15, 1999.

Mzenga, M. (1977) *Utenzi wa Nabii Isa*.Nairobi: Fountain Books Ltd.

Ndumbaro, E (2013) *Shujaa wa Tendi na Matatizo ya Kijamii*.Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Njogu, K na Chimera, R (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: J.K.F.

Njogu, K na Wafula, R (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: JKF.

Nurse, D (1994) Historical texts from the Swahili Coast *"Swahili Forum 1 AAP* Nam. 37 uk 47-85.

Sheikh Abdullah Saley na Al farsy (1984). *Qurani Takatifu*. Nairobi: The Islamic Foundation Publication. Chapa ya nne.

Steere, E. (1870) *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar*: London

Sutton, J.E.G. (1966) *The East African Coast: A Historical and Archeological Review*. Nairobi: East African Publishing House.

TUKI (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la pili) Nairobi: Oxford University Press.

United Bible Societies (1952) *Bibilia*. Nairobi: Scripture Union.

Wamitila, K.W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix

Werner, A. (1915) The Bantu Coast Tribes of The East African Protectorate.*Journal of Royal Anthropological Institute* XLV, uk 326-345.